SUPA JACKPOT
TZS. 1,044,303,118
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 8

## IGP aunda timu ya kuchunguza mauaji Kilombero



Nipashe

# TESA

Jumanne Oktoba 25, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Asasi ya kuokoa wasichana dhidi ya mila potofu yajikita Pwani, shule 22 zaneemeka

Ukurasa 15

Haya yanawachochea watoto kuhama familia, kuishi mitaani

Ukurasa 16

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

KIRUSI HATARI CHA MAABARA

## Chuo Kikuu kilivyozua taharuki chazalisha toleo hatari la UVIKO-19

• Kinaua asilimia 80, ni mahiri kukwepa na kuharibu kinga za mwili kuliko vingine

MWEZI Oktoba, umekuwa wa kishindo kipya cha hofu ya kuibuka upya UVIKO-19 kufuatia taarifa kuwa Chuo Kikuu cha Boston cha Marekani kimetengeneza kirusi kingine cha COVID-19 hatari zaidi, kuliko kile cha Omicron.

Aidha, taarifa zinasema kuwa aina hiyo mpya ya UVIKO au COVID-19 ni mseto unaochanganywa na wanasayansi katika Chuo Kikuu cha Boston na kwamba kirusi kina nguvu nyingi na kinaua kwa asilimia 80 na kina mizungu au uganga zaidi wa kuzikwepa kinga za mwili.

Maelezo hayo yakiongeza kuwa miongoni mwa majaribio yake yalifanywa kwenye panya na kubaini kuwa ni hatari na tofauti na aina ya zamani ya Omicron kwa vile kwenye omicron, panya hao walipata athari kidogo tu walipoambukizwa virusi.

Wanasayansi na wataalamu wa matibabu wakiwa na nadharia tofauti wengi wakipinga kuwa utafiti kama huo kwenye popo ulifanywa katika maabara za jimbo la Wuhan nchini China ukawa chimbuko la corona duniani na kuanzisha janga la virusi waliokatishia uhai wa mamilioni bila sababu hasa watumishi wa afya.

Hatua ya Boston, ikikosolewa na wataalamu wanaosema: "Utafiti juu ya vimelea vya magonjwa vinavyoweza kutokea unahitaji kuongezwa na kulindwa ili kuepusha matatizo hatari yanayoweza kuibuka mbeleni." Dk. Richard Ebright wa Chuo Kikuu cha Rutgers na mtaalamu mkuu wa kemia anasema.

Anaongeza kuwa anaamini kwamba utafiti ukifanywa, husaidia kuelewa kinachoharibika na hapo ndipo wanaweza kuepuka janga linalofuata la maabara kuzalisha maradhi hatari.

Huko Boston, wanasayansi wanaotafiti aina mpya ya COVID-19 walitoa protini kutoka kwa aina ya Omicron. Protini hiyo ndiyo hung'ang'ania seli za binadamu na kisha kuzishambulia, watafiti waligundua kuwa panya walikipokea kirusi kwa njia tofauti na kuliko ile mpya, ambayo ilikuwa nyepesi kwa wanyama mamalia akiwamo binadamu.

Lakini aina mpya, Omicron S, ilishambulia panya wote na kuua asilimia 80 yao, waliandika katika ripoti zao watafiti hao wa Boston.

JUHUDI ZA KUKANUSHA

Baada ya taarifa kusambaa kuwa wameandaa kirusi hatari kwenye maabara zao, Chuo Kikuu cha Boston kikaingia kiwewe na kuanza kufafanua utafiti wake wa COVID-19.

wanajitetea kuwa aina mpya kitaalamu ikiitwa 'new variant' haikuwa mbaya sana.

"Gazeti la udaku la Daily Mail la Uingereza lilizua utata na taharuki kwa kusema Chuo Kikuu cha Boston kimeunda kirusi kingine hatari cha COVID chenye "kiwango cha kusababisha vifo kwa asilimia 80," gazeti la Boston Globe linabainisha.

Likazidi kukanusha kuwa chuo kikuu kimejibu kwa ukali na kikabaini kuwa majaribio yake yalifanya virusi kuwa hatari zaidi.

Boston University -BU inaripoti kwamba iliunda aina hatari zaidi ya COVID 'ya uwongo na isiyo sahihi' na kuongeza kuwa jarida la udaku la Uingereza lilipotosha matokeo ya utafiti wa virusi uliofanywa katika maabara ya BU ya South End.

Wanasayansi wa Chuo Kikuu cha Boston wakiwa maabara kuzalisha kirusi kipya. **PICHA: MTANDAO**

INAENDELEA UK. 18

UKURASA 13

Nipashe
Jumanne Oktoba 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581109
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mshtakiwa aeleza sababu kumuua mke

**NI** yule aliyemchoma kwa magunia mawili ya mkaa, aachiwa kisha akamatwa tena... *Endelea ukurasa 2*





Mtuhumiwa wa kesi ya mauaji, Khamis Luwonga (kulia), akiwa chini ya ulinzi wa Askari Magereza akitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam jana kusikiliza kesi inayomkabili ya kumuua mke wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UKURASA WA 4

### KINANA: MAALIM SEIF ALIKUWA MWENYE USHAWISHI MKUBWA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amemwelezea Hayati Maalim Seif Sharif Hamad kuwa kiongozi ...

UKURASA WA 4

### UPELELEZI KESI YA SABAYA WAIVA

KESI ya uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na rushwa, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, imeiva baada ya upande wa mashtaka kuomba kuwasilisha...

UKURASA WA 5

### MADAKTARI BINGWA IRELAND WAPIGA KAMBI MOI

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) imepokea jopo la madaktari bingwa wa mifupa wa watoto kutoka Taasisi ya Children Health Ireland Africa (CHIA) ambao wataendesha...

## Watoto wateketea kwa moto mama akilewa chakari kilabuni

UKURASA 2

## Tanzania, DRC zatiliana saini ushirikiano sekta ya mawasiliano

UKURASA 3

**MICHEZO** MICHO AFUNGUKA YANGA, AMTAJA MGUNDA, MATOLA UK. 32

**KATUNI** UK. 6



Wakazi wa Mtaa wa Mfifi, Kata ya Kihesa mkoani Iringa wakiwa nje ya nyumba iliyoteketea kwa moto na kuua watoto wawili. **PICHA: MARTHA SAMBO**

# Mshtakiwa aeleza sababu kuua mke

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38), anayedaiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani, kwa kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, ameeleza sababu za kutekeleza kitendo hicho.

Luwonga alitaja sababu za kuachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kueleza kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka dhidi yake. Hata hivyo, baadaye alikamatwa tena na kusomewa upya mashtaka.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa mke wake kila siku alikuwa anamwomba Mungu afe kuliko kuendelea kuishi katika ndoa yao na alikuwa anang'ang'ania kifo chake kwa nguvu. Kutokana na kifo hicho, kwa sasa mtoto wao anaishi bila wazazi.

Pia alidai kifo cha mke wake hakikusababishwa na yeye peke yake bali wengine waliohusika ni familia za pande zote za mbili, maofisa wa polisi na watumishi wa ngazi za chini za serikali.

Luwonga alizungumza hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Ruboroga, baada ya hakimu huyo kumaliza kutoa uamuzi wa kumwachia huru mshtakiwa kama upande wa Jamhuri ulivyoomba chini ya kifungu cha 91 (1) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Mshtakiwa alianza kwa kuomba radhi kwa hakimu kwa kutaka kujua jina lake ili ajue anazungumza na nani kwa sababu amesahau jina lake, lakini Ruboroga alimweleza kwamba yeye aendelee kusema anachokitaka.

Luwonga alishusha pumzi kwanza, akaweka dumu lake la maji na gazeti lake la Nipashe juu ya meza huku akiwa amefunika pua yake kwa kitambaa alidai kuwa siku zote watu wanapenda kuangalia uharibifu unapotokea, lakini hawaangalii chanzo cha tukio.

"Kama tukio nililoshtakiwa nalo, Watanzania wanaangalia uharibifu uliotokea hawaangalii chanzo nini. Nina maumivu makubwa sana ya kifo cha mke wangu kipenzi Naomi kwa sababu ya baadhi ya watu wanaodharau matukio.

"Walipaswa kuzuia mambo ya hatari kutokea na si kusubiri uharibifu kutokea. Hata vitabu vya dini vinaeleza hayo. Kwenye Quran na kwenye Biblia ukisoma utaona ninachokizungumza kwamba ukimuona mtu anataka kukengeuka unamweka sawa," alidai Luwonga.

Alidai si yeye peke yake anayehusika na kifo cha mke wake kipenzi. Alidai wengine waliohusika ni familia yake, familia ya mke, baadhi ya maofisa wa polisi, watumishi wa chini wa serikali pamoja na jamii kwa ujumla, kwa kushindwa kufanya uamuzi.

Huku akiwa anahema sana Luwonga kwa uchungu alidai kuwa waliohusika na kifo cha mke wake, wameanzisha jambo lingine la kuwakatalia ndugu zake kumwona mtoto wao kwa kumweka kifungo cha kutia huruma.

"Sidhani kama mwanangu anakuwa wa kwanza kulipiwa ada kama watoto wengine wanaosoma kwa sababu amewekwa katika kifungo na hawa hawa wanaosema mimi peke yangu ndiye nimeua wakati kisaikolojia anahitaji faraja na upendo.

"Mwanangu hayuko sawa kabisa. Kifungo anachopitia kwa sasa ni kibaya sana bora cha gerezani. Ndugu zangu wamezuiwa kumwona mtoto wangu. Mtoto ana kosa gani? Tunapaswa kutatua na kuzuia matatizo ya hatari kabla ya tatizo," alidai Luwonga.

Akiendelea kuzungumza kwa uchungu na kwa sauti huku akihema sana, Hakimu Ruboroga alimwambia kwamba alichokizungumza tayari ameshamwelewa kuwa suala analolilalamikia la msingi yeye ni suala la mtoto.

Hakimu Ruboroga alimshauri mshtakiwa kuwa suala hilo limekaa kifamilia zaidi kwa hiyo wakae kama familia kumsaidia mtoto.

Hata hivyo, hadi saa 8:00 mchana, mshtakiwa alikuwa bado yuko mahabusu kwa sababu kifungu cha sheria aliyoachiwa nacho anaweza kukamatwa na kushtakiwa tena, kwa hiyo haijajulikana kama atashtakiwa au la.

Pia mshtakiwa kwa siku ya jana alikuwa amebadilika kwa kuwa na tabia ya upole tofauti na awali alivyokuwa mkali sana. Alikuwa anatoa maneno ya vitisho kwa waandishi wa habari.

Hali hiyo ya vitisho iliyokuwa ikitolewa na mshtakiwa ilisababisha mshtakiwa kupelekwa mahakamani akiwa na pingu mikononi na miguuni.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba nne ya mwaka 2019, Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimuua Naomi Marijani.

Luwonga anadaiwa kumuua mke wake kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa ambapo alichukua majivu ya marehemu na kwenda kuyafukia shambani kwake.

**AKAMATWA TENA**

Ilipofika saa 8:26 mchana, mshitakiwa alipandishwa tena kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Rhoda Ngimilanga wa mahakamani hiyo na kusomewa upya mashtaka ya mauaji.

Wakili Ally alidai upelelezi haujakamilika na kuomba wapangiwe tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa, Ngimilanga aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 7, 2022.

Mshtakiwa amerudishwa mahabusu hadi tarehe hiyo kwa sababu kisheria shtaka la mauaji halina dhamana na pia hakutakiwa kujibu kweli au si kweli kwa sababu Mahakama ya Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza shauri lake.

# Watoto wateketea kwa moto mama akilewa chakari kilabuni

**Na Martha Sambo,** IRINGA

Watoto wawili wamefariki dunia baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto katika Mtaa wa Mafifi, Kata ya Kihesa, Manispaa ya Iringa huku mama yao akiwa analewa kilabuni.

Kwa mujibu wa mashahidi wa tukio hilo, watoto hao, Rehema Masanga (7) na Amos Masanga (5) walishindwa kujiokoa baada ya mama yao, Skolastica Mgombewa kufunga mlango kwa nje akiwaacha peke yao na kwenda kilabuni kunywa pombe.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mafifi, Rabi Mgata, aliiambia Nipashe kuwa chanzo cha moto huo ni mshumaa ambao ulishika godoro kisha kuunguza nyumba yote.

"Mama yao aliwafungia watoto ndani akaenda kunywa pombe. Kwa hiyo moto ulivyokuwa unaendelea kuwaka walishindwa kujiokoa. Mama alirudi baadaye akiwa amelewa wakati tayari tumeshazima moto na kugundua watoto wamekufa," alisema.

Mgata alisema taarifa za nyumba hiyo alizipata jana saa 4:00 usiku na kwenda kwenye tukio ambako tayari watu walikuwa wameanza kuzima moto.

Alisema baada ya kuzima moto, walibomoa mlango na kukuta watoto wawili waliokufa huku wakiwa wamekumbatiana kwenye kona moja ya nyumba.

Baadhi ya majirani walisema awali walianza kuona moshi ukifuka lakini wengine walidhani ni wa matairi.

Kamanda wa Zimamoto Mkoa wa Iringa, Isabela Bwago, amekiri kuwa chanzo cha tukio hilo ni mshumaa ambao ulishika godoro kisha kuunguza nyumba yote bila kuokoa kitu chochote.

"Ni uzembe wa mzazi ambaye aliondoka akiwa amewafungia watoto wake kwa nje. Taarifa ya moto tulipewa kwa kuchelewa na hata ingekuja mapema gari lisingeweza kufika eneo la tukio kulingana na miundombinu mibovu," alisema Bwango.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Issa Juma, alisema wakati jamii inahangaika kuzima moto huo hawakujua kama ndani kuna watoto.

Juma aliitaka jamii kuwa makini na matumizi ya mishumaa, vibatari, taa na kuwa walinzi wa familia zao hasa watoto.

"Niwasihi wazazi na walezi kuwa makini na waweke uangalizi kwa watoto kwa kuchukua tahadhari ili kuepuka vifo vinavyoweza kuzuilika," alisema.

HABARI KITAIFA

# Tanzania, DRC zakubaliana ushirikiano sekta mawasiliano

**Na Beatrice Moses**

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Felix Tshisekedi, wameshuhudia utiaji saini wa hati ya makubaliano (MoU) baina ya nchi hizo mbili inayohusu ushirikiano kuendeleza sekta ya mawasiliano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, kwa vyombo vya habari sekta ya mawasiliano imetajwa kuwa ni pekee inayozalisha rasilimali pamoja na ajira kwa vijana kwa kiasi kubwa.

Utiaji saini wa hati hiyo inayohusu ushirikiano katika masuala ya teknolojia (ICT), Posta na Mawasiliano, umefanyika Ikulu jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya kiserikali ya Rais Tshesikedi nchini.

Mkataba huo unaohusu teknolojia umetiwa saini na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa DRC, Christopher Lutundula.

Taarifa hiyo imebainisha kuwa katika kukuza jitihada za biashara kati ya nchi hizo mbili, Rais Samia amesema Serikali ya Tanzania inaifanyia marekebisho meli ya MV Sangara ili ianze tena kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kati ya Tanzania na DRC.

Pia alisema Tanzania na DRC kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zina mpango wa kujenga ushoroba wa kati (central corridor) wa barabara itakayounganisha Tanzania na DRC.

Takwimu za biashara baina ya nchi hizo mbili zimepungua kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, nchi hizo zimefufua tume ya pamoja ya ushirikiano ili kukuza uhusiano na ushirikiano uliopo kwa manufaa ya nchi zote mbili.

Rais Tshisekedi aliondoka nchini jana baada ya kumaliza ziara yake.

Akiwa Visiwani Zanziabr, alifanya mazungumzo na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ikulu na kwamba walijadili umuhimu wa kuangalia maeneo zaidi ya ushirikiano kati ya nchi mbili hizo kupitia sekta za kiuchumi na biashara, wakati huu biashara ya usafirishaji wa dagaa kutoka Zanzibar kwenda nchini Kongo ikishamiri.

Aidha, Dk. Mwinyi alimuomba Rais Tshisekedi kuutangaza utalii wa Zanzibar kwa wadau wa sekta ya utalii nchini Kongo.

Rais Tshisekedi alimshukuru kiongozi huyo kwa mapokezi mazuri aliyopata yeye na ujumbe aliofuatana nao na akatumia fursa hiyo kuahidi kuongeza ushirikiano kati nchi hizo kwa maslahi ya mataifa hayo na wananchi wake.

# NMB yazindua kampeni maalumu kufanikisha msimu mpya korosho

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa mwaka huu wa korosho unaanza rasmi kesho ukilenga kuzalishaji tani 400,000 za zao hilo, lengo ambalo Benki ya NMB imesema iko tayari na ina uwezo kifedha kuhakikisha linafanikiwa.

Katika kutimiza azma hiyo, jana benki hiyo ilibainisha utayari wake wa kufanya hivyo na kubainisha mikakati iliyonayo kulisaidia taifa kupata matokeo chanya kwenye msimu huu wa 2022/23.

Mbali ya mikopo na huduma zake zingine, NMB inapanga kutumia kampeni maalumu ya kuhamasisha matumizi ya benki kuufanya msimu huu mpya kuwa wa mafanikio makubwa zaidi kiuzalishaji na kibiashara kulinganishwa na misimu iliyopita.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Biashara wa benki hiyo, Isaac Masusu, alisema kampeni hiyo imepewa jina la "Bonge la Mpango - Mchongo wa Kusini" na mchakato mzima unawalenga wakulima wa korosho na vyama vyao vya ushirika (AMCOS).

"Ili kuendelea kuhamasisha matumizi ya huduma za Benki ya NMB kwa wakulima na vyama vya ushirika, leo hii tunawaletea kampeni maalum tunayoiita 'Bonge la Mpango' na kwa mwaka huu tumekuja na kaulimbiu ya 'Mchongo wa Kusini'.

"Tumeona ni vyema tukailenga zaidi kanda hii ya kusini kwani tunataka kuendelea kuvihamasisha vyama vya wakulima (AMCOS) pamoja na wakulima hususani katika kipindi hiki cha msimu wa korosho kuendelea kufanya malipo na kuhifadhi fedha zao katika Benki ya NMB kwa usalama zaidi huku wakiendelea kunufaika na huduma zetu zilizo bora na zilizoenea katika maeneo mbalimbali," kiongozi huyo alibainisha. Benki hiyo ilizindua kampeni hiyo jana kwenye Kongamano na Viongozi wa Vyama vya Ushirika mkoani Mtwara lililoandaliwa kwa ajili ya kubadilishana mawazo jinsi ya kuufanikisha msimu huu na wadau wa zao hilo.

Alisema kongamano hilo pia limefanyika kwa kutambua namna kilimo cha korosho kimekuwa nguzo muhimu kwa ustawi wa Kanda ya Kusini hususani mikoa ya Lindi na Mtwara, pia kwa taifa na hata Benki ya NMB.

"Benki ya NMB inatambua kuwa uchumi wa kanda hii hususani katika mikoa ya Lindi na Mtwara umeegemea zaidi kilimo cha korosho na ndio maana tumekuja katika kipindi hiki ili mbali na kunufaika na kilimo cha korosho, wakulima kupitia AMCOS zao wataweza pia kunufaika zaidi na zawadi wakitumia Benki ya NMB kuhifadhi fedha zao na kuitumia katika kufanya malipo mbalimbali," alibainisha.

Aidha, alisema kuwa wakulima watakaoitumia NMB wataziwezesha AMCOS zao kushinda zawadi zilizotengwa kwa ajili ya kampeni hiyo ambayo zawadi zake ni pikipiki tano watakazozipata washindi kwenye droo zitakazofanyika kila baada ya wiki mbili.

Droo yake ya kwanza itafanyika Oktoba 28, mwaka huu. Mbali na kuwahamasisha wakulima kuitumia zaidi Benki ya NMB kufanya miamala, sababu nyingine ya kampeni hiyo ni kuhamasisha amana na kuwasaidia watu kuweka akiba.

Masusu alisema NMB ina uwezo kifedha na iko vizuri kiutendaji pamoja na kujipanga vizuri sokoni kuhakikisha hayo yanafanyika na kampeni ya "Bonge la Mpango - Mchongo wa Kusini" inafanikiwa.

Hiyo inatokana na kuwa na matawi 228 yaliyotapakaa nchi nzima yakisaidiwa kuhudumia taifa na ATMs zaidi ya 800 huku ukwasi wake wa zaidi ya Sh. trilioni 8 ukiwa ndiyo mkubwa sana kwenye tasnia.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, alisema kampeni hiyo itasaidia kubadilisha maisha ya watu wengi na kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa korosho wa Mkoa wa Mtwara.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**

**Simu No: +255 (26) 2966008**
**Fax No: +255 (26) 2966008**
**Email: ded@uyuidc.go.tz**

**S.L.P. 610,**
**TABORA.**

**Kumb. Na.HWU/T.10/77** **25/10/2022**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Halmashauri ya Wilaya ya Uyui inawatangazia wananchi wote, wafanyabiashara, makampuni na Taasisi mbalimbali mnada wa hadhara. Kwa idhini tuliyopewa na Katibu Mkuu Hazina, tunauza kwa **MNADA WA HADHARA MAGARI 2 NA PIKIPIKI** 14 siku ya tarehe 8/11/2022 kuanzia saa 4.00 asubuhi. Kwenye jengo la ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Uyui.
Tarehe ya kuja kukagua Magari ni 7/11/2022.

**ORODHA YA MAGARI YATAKAYOUZWA NI KAMA IFUATAVYO;-**

| S/N | LOT NO | REGISTRATION NUMBER | MAKE /MODEL | CHASIS NUMBER | LOCATION |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 01/MV/UYUI/TBR/2019 | SM 4146 | ISUZU NQR | JAANR65R37100005 | UYUI DC |
| 2 | 03/MV/UYUI/TBR/2019 | STK848 | MITSUBISH L200P/UP | MMBJNK74040033126 | UYUI DC |
| **ORODHA YA PIKIPIKI ZINAZOTAKIWA KUUZWA NI KAMA ZIFUATAZO; -** | | | | | |
| 1 | 07/MC/UYUI/TBR/2019 | SM 4714 | YAMAHA AG | 3HA177883 | UYUI DC |
| 2 | 08/MC/UYUI/TBR/2019 | STJ 3229 | HONEDA XL | LI2555759945 | UYUI DC |
| 3 | 11/MC/UYUI/TBR/2019 | SM 3684 | YAMAHA DT | JYA3TS00000080163 | UYUI DC |
| 4 | 12/MC/UYUI/TBR/2019 | STK 5314 | YAMAHA DT | 3GX101204 | UYUI DC |
| 5 | 13/MC/UYUI/TBR/2019 | STK 7135 | HONDA XL | LI2555751585 | UYUI DC |
| 6 | 14/MC/UYUI/TBR/2019 | STJ 1409 | HONDA 110 | JD015301255 | UYUI DC |
| 7 | 15/MC/UYUI/TBR/2019 | STJ 1423 | HONDA 110 | JD015301204 | UYUI DC |
| 8 | 16/MC/UYUI/TBR/2019 | STJ 1501 | HONDA 110 | JD015304983 | UYUI DC |
| 9 | 18/MC/UYUI/TBR/2019 | SM 1712 | YAMAHA | 3HA132373 | UYUI DC |
| 10 | 19/MC/UYUI/TBR/2019 | STK 5360 | YAMAHA AG 200 | 3GX100136 | UYUI DC |
| 11 | 20/MC/UYUI/TBR/2019 | SM 8791 | YAMAHA AG | 3HA174343 | UYUI DC |
| 12 | 21/MC/UYUI/TBR/2019 | SM 4719 | YAMAHA AG | 3HA133765 | UYUI DC |
| 13 | 23/MC/UYUI/TBR/2019 | STK 2846 | YAMAHA AG | 3HA124559 | UYUI DC |
| 14 | 24/MC/UYUI/TBR/2019 | STK 5308 | YAMAHA AG 100 | 3GX100200 | UYUI DC |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi anatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi kilichobaki cha 75% kinatakiwa kilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) Mnunuzi akishindwa kulipia gharama ya 75% ya gharama iliyobaki atakuwa amejitoa kwenye mchakato mzima na fedha aliyotoa ya 25% haitarudishwa na mnada utarudiwa tena
2. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utafanyika mara moja kabla ya siku ya mnada kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 3.30 mchana siku ya kazi
3. Gharama ya kubadilisha umiliki (Transfer of ownership), kodi na gharama zingine zote zitakazojitokeza zitakuwa ni gharama za mnunuzi
4. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo
5. Mnunuzi atawajibika kuondosha/kuchukua mali aliyonunua ndani ya siku saba kuanzia siku ya kukamilisha malipo. Asipochukuwa baada ya muda huo atawajibika kulipia gharama za utunzaji wa chombo husika.

**Imetolea na**
**Hemed S. Magaro**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**

# Kinana: Maalim Seif Hamad alikuwa mwenye ushawishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR



MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amemwelezea Hayati Maalim Seif Sharif Hamad kuwa kiongozi mwenye maono, msimamo na ushawishi mkubwa kwa watu wengi ikiwamo wafuasi wake.

Aliyasema hayo jana mjini hapo wakati akifunga mkutano wa pili wa kumuenzi Hayati Maalim Seif ulioandaliwa na Taasisi ya Maalim Seif.

Kwa mujibu wa Kinana, kiongozi huyo alipenda kuona vijana wanapata elimu bora inayolingana na mahitaji ya wakati na yenye kuwajenga vijana kudadisi, kujituma, kujitegemea na wazalendo kwa wanadamu na ndiyo maana elimu yake alipata kwa kujituma bila kukata tamaa.

"Bila shaka viongozi wa wakati huo waliona na kuthamini kiu aliyo nayo Maalim Seif na hivyo kumpa nafasi ya kuongoza Wizara ya Elimu akiwa na umri mdogo, jukumu hilo lilikuwa zito kwa kuwa fursa za elimu zilikuwa ndogo na hafifu," alisema.

Kinana alisema kwa ujasiri mkubwa na kwa hatua za kuthubutu alijitwisha dhamana ya kufanya kazi aliyopewa kwa ustadi, hamasa na ari kubwa. Alisema kutokana na juhudi hizo vijana wengi wa Zanzibar walipata nafasi za elimu ndani na nje ya nchi.

Alisema Maalim Seif aliamini katika elimu, nafasi ya elimu na fursa zinazoletwa na elimu katika maisha ya binadamu na katika uhai wa taifa.

Aidha, alisema nchi ipo katika mchakato wa kutazama upya sera na mfumo wa elimu kwa lengo la kuboresha elimu, ili elimu wanayopata watoto ilenge kuwajenga, kujitegemea na kuendana na mabadiliko na mahitaji ya ulimwengu wa sasa.

Alisema anafurahishwa namna vijana wengi wanavyojituma, kujielimisha kwa kutumia akili na nguvu zao pamoja na ubunifu katika kujitafutia fursa za kujitengenezea ajira, kujiongezea kipato na kuwa wabunifu.

"Haya tumeyaona katika nyanja za teknolojia, sanaa, biashara na uzalishaji wa mazao na bidhaa vijana wetu wanajituma na wanahangaika wanatafuta njia kadhaa za kujiajiri na kujiongezea kipato," alisema Kinana.

Hata hivyo, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuleta maridhiano na mageuzi kwenye siasa na uendeshaji wa taifa.

Alisema kiongozi huyo ana lengo la kusimamia haki, kukuza, kuimarisha uhuru, kupanua wigo wa kuendesha shughuli za kisiasa na kuleta mageuzi katika uendeshaji wa serikali kwa madhumuni ya kuharakisha maendeleo ya nchi na watu wake.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Nassor Ahmed Mazrui, alizipongeza taasisi, mashirika ya kimataifa na mabalozi kwa mchango uliofanikisha mkutano huo.

"Nawapongeza taasisi mbalimbali ikiwamo mashirika ya kimataifa na mabalozi kwa mchango wao ambao umefanikisha mkutano huo na kwamba wataendelezwa watu wengi kielimu.

"Tutamuenzi Maalim Seif kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya katika kipindi chake chote ikiwamo kwenye mikakati ya kukuza sekta ya elimu, tunakusudia kuanzisha Kigoda Maalumu cha Elimu, kitakachozungumzia demokrasia," alisema Mazrui.

Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Mariyamu Ismali Jaffar, alisema mfumo wa elimu Zanzibar unahitaji kufanyiwa marekebisho, utakaowezesha wahitimu wake kuingia kwenye soko la ajira kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizoko.

Dk. Ismali ambaye ni mjumbe wa kamati ya kikosi kazi kinachopitia muundo wa elimu wa Zanzibar, alisema wameanza kukusanya maoni na kuonana na makundi mbalimbali kujua mahitaji ya sekta ya elimu kwa sasa.

"Mimi ni mjumbe wa kikosi kazi kilichoundwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuangalia nini kifanyike kuboresha muundo wa elimu Zanzibar, tunaendelea vizuri katika kazi ya kukusanya maoni," alibainisha.

Mkurugenzi mstaafu wa Wizara ya Elimu miaka ya 1990, Hussein Ali Suleiman, alikiri kuyumba kwa sekta ya elimu ikiwamo ufaulu wake na kukitaka kikosi kazi kilichoteuliwa kufanya utafiti na kuja na mikakati itakayohakikisha elimu ya Zanzibar inapiga hatua kubwa na kuwawezesha wahitimu kujiajiri.

"Mfumo wa elimu wa Zanzibar unatakiwa uvunjwe moja kwa moja na tuje na mikakati ambayo itatuwezesha kuja na muundo wa elimu ambayo utatuwezesha vijana wetu kuingia katika soko la ajira," alisema.

Aidha, Mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Chriss Maina Peter, alimwelezea Maalim Seif kuwa alikuwa mstari wa mbele kuona vijana wanajiunga na masomo ya sheria kwa ajili ya kujenga uwezo na kuingia soko la ajira.

"Maalim Seif Sharif Hamad alikuwa mstari wa mbele kuona vijana wanapata elimu ngazi mbalimbali, ikiwamo elimu ya sheria hatua iliyotuwezesha kuzalisha wanasheria wengi vyuoni," alisema.

# Kaganda ateuliwa Kamishna wa Polisi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amempandisha cheo Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Suzan Kaganda kuwa Kamishna wa Polisi.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Ikulu jana, ilisema vile vile, Rais Samia amemteua Kamishna Kaganda kuwa Kamishna wa Utawala na Rasilimali Watu wa Jeshi la Polisi.

Kamishna Kaganda anachukua nafasi ya Kamishna wa Polisi (CP) Benedict Wakulyamba ambaye atapangiwa kazi nyingine.

Kaganda anakuwa mwanamke wa pili nchini kushika wadhifa wa Kamishna. Wa kwanza alikuwa Elice Mapunda, ambaye kwa sasa ni mstaafu.

Mapunda, wakati anastaafu mwaka 2018, alikuwa Kamishna wa Uchunguzi wa Kisayansi wa Makosa ya Jinai.

Taarifa hiyo ilisema uteuzi huo unaanza mara moja.



# Upelelezi kesi ya Sabaya waiva

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KESI ya uhujumu uchumi, utakatishaji fedha na rushwa, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, imeiva baada ya upande wa mashtaka kuomba kuwasilisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kibali cha kuanza usikilizwaji wa shauri hilo.

Jana, Wakili wa Serikali, Susan Kimaro, akisaidiwa na mawakili Kassim Nasri na Sabitina Mcharo, aliwasilisha ombi hilo kwa Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Salome Mshasha, anayesikiliza kesi hiyo.

Wakili Kimaro alidai kuwa upande wa mashtaka unaomba kuwasilisha nyaraka na kibali ili shauri hilo lianze kusikilizwa na mahakama hiyo.

"Mheshimiwa, upelelezi wa shauri hili umekamilika. Tunaomba ikikupendeza upange tarehe nyingine ya shauri hili kwa ajili ya kuwasilisha vibali na nyaraka sahihi ili kesi ianze kusikilizwa," alidai.

Baada ya ombi hilo, Hakimu Mshasha aliwahoji mawakili wa utetezi kama wana pingamizi juu ya taarifa ya upande wa mashtaka na Wakili wa Utetezi, Helena Makuna, aliyekuwa akisaidiwa na Emmanuel Antony, alidai kuwa hawana pingamizi kuhusu nia ya upande wa mashtaka kuwasilisha kibali na kwamba wameridhika na taarifa hiyo.

Kutokana na majibu hayo, Hakimu Mshasha alisema kwa kuwa upande wa mashtaka unaoijenga kesi hiyo umewasilisha ombi la kuwasilisha kibali na nyaraka muhimu za kesi hiyo, anaahirisha shauri hilo hadi Novemba 7, mwaka huu, itakapotajwa mahakamani hapo.

Sabaya alipanda kizimbani kwa mara ya tatu jana akiwa peke yake, baada ya waliokuwa washtakiwa wenzake wanne kukiri kosa na kutiwa hatiani Septemba 6, mwaka huu. Kabla ya kuachiwa washirika wenzake, walimwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) ya kuomba kufanya makubaliano naye Agosti 3, mwaka huu.

Makosa anayokabiliwa nayo Sabaya ni kuongoza genge la uhalifu katika Wilaya ya Hai, Februari 2, mwaka jana, na kuomba rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Godbless Swai katika eneo la Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, Februari 22, mwaka jana.

Aidha, Sabaya anadaiwa kujipatia rushwa ya Sh. milioni 30 kutoka kwa Elibariki Swai kwa nia ya kuzuia taarifa za uchunguzi zilizohusiana na ukwepaji wa kodi.

Pia anakabiliwa na kosa la ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma katika Wilaya ya Hai na shtaka la utakatishaji wa fedha.

HABARI KITAIFA

# Madaktari bingwa Ireland wapiga kambi MOI

Na Mwandishi Wetu

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) imepokea jopo la madaktari bingwa wa mifupa wa watoto kutoka Taasisi ya Children Health Ireland Africa (CHIA) ambao wataendesha kambi maalum ya upasuaji kwa kushirikiana na madaktari bingwa wa MOI kwa siku nne. Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema jana kuwa ujio wa madaktari bingwa kutoka Ireland ni sehemu ya mkakati wa taasisi kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa ili kuboresha huduma kwa wananchi.

"Leo (jana) tumepokea wageni kutoka Ireland ambao watakuwa nasi hapa kwa siku nne. Watatoa huduma kwa wagonjwa ikiwamo upasuaji kwa watoto 10 wenye viungo vilivyopinda," alisema.

Dk. Boniface alisema ushirikiano kati ya MOI na CHIA utajikita katika maeneo ya Mafunzo, kubadilishana na watumishi, utafiti, tiba mtandao pamoja na vifaa tiba.

Ofisa Uendeshaji Mkuu wa CHIA, Joe Gannon, alisema ni heshima kubwa kupata fursa ya kushirikiana na MOI ili kuangalia namna bora ya kuboresha huduma kwa watoto.

Naye Mkurugenzi wa Tiba wa CHIA, Dk. Paula Llelly, alisema ushirikiano kati ya taasisi yake na MOI utakuwa na manufaa makubwa kwa pande zote mbili kwa kuwa wanaufaika wakubwa watakuwa wagonjwa.

Katika kutekeleza kwa vitendo agizo la serikali uboreshaji huduma kwa wananchi, MOI imekuwa ikianzisha ushirikiano na taasisi mbalimbali za kimataifa ili kuboresha huduma zake kwa Watanzania na kumaliza rufani za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.





## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | 1.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 ,2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NAMBA 172590 KIWANJA NAMBA 399 KITALU 'L' | 1. DAVID ABEL MLAU 2.SADIKI THAHONDI MAPORO | 1.CHARAMBE -MBAGALA , 2. MKURANGA | 09/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | NEEMA ERNEST KASILILIKA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | DASTAN SEVERIN CHANDE | MANZESE | 09/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TANDALE | YUDATHADE DONASIANI ASSENGA | NYUMBA | YUDATHADE DONASIANI ASSENGA | TEGETA 'A' | 10/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TANDALE | ZAITUNI OMARY JUMA | NYUMBA | ZAITUNI OMARY JUMA | KIVULE MATEMBELE YA PILI | 11/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TANDALE | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | NYUMBA | HAMAD ABDALLA MNEMBWE | TANDALE | 09/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0762260787/0785242219/0784252048**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



## Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

**IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-22 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,126 | 1,963 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 16,828 | 13,693 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 45,272 | 49,219 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,285 | 1,849 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 10,684 | 10,669 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 84,579 | 84,392 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,542 | 2,665 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,735 | 2,916 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **167,051** | **167,366** |
| B. | B. DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 54,628 | 55,567 |
| 18 | Amana za Wateja | 69,613 | 69,331 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 32 | 80 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 25 | 25 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,619 | 2,260 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,969 | 1,990 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **128,886** | **129,253** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **38,165** | **38,113** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,500 | 21,500 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,798 | 2,130 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 14,070 | 13,739 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 797 | 744 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **38,165** | **38,113** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 12,216 | 6,708 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,414 | 6,449 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,550 | 1,219 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22.85% | 22.77% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7.45% | 7.53% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 69.32% | 68.54% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 50.63% | 50.42% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85.05% | 86.93% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.53% | -7.33% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -0.19% | -4.55% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 3,168 | 3,815 | 9,635 | 9,417 |
| 2 Gharama za Riba | 1,391 | 1,160 | 3,822 | 3,540 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,777** | **2,655** | **5,813** | **5,877** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (31) | 3 | (36) | 3 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 351 | 300 | 932 | 691 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **221** | **242** | **592** | **501** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | 51 | 31 | 139 | 116 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 170 | 211 | 453 | 385 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **1,438** | **1,363** | **4,153** | **3,861** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 691 | 579 | 1,925 | 1,570 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 747 | 784 | 2,228 | 2,291 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **240** | **1,231** | **1,356** | **1,823** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 187 | 219 | 560 | 657 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **53** | **1,012** | **796** | **1,166** |
| **11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa robo ya** | **53** | **1,012** | **796** | **1,166** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 34 | 30 | 34 | 30 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 10 | 188 | 74 | 108 |
| 15 Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.58% | 2.99% | 1.60% | 1.48% |
| (ii) Wanahisa | 0.56% | 11.02% | 4.20% | 4.22% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 42.43% | 33.60% | 40.61% | 38.93% |
| (iv) Zinazozalisha | 5.11% | 7.45% | 8.01% | 5.60% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya bei ya Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo mwaka ya sasa 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.07.2022** | **21,500** | **-** | **14,483** | **2,130** | **-** | **-** | **38,113** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 53 | - | - | - | 53 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 332 | (332) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | | | - | | | | - |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.09.2022** | **21,500** | **-** | **14,867** | **1,798** | **-** | **-** | **38,165** |
| **Robo Mwaka iliyopita 2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka 01.04.2022** | **21,500** | **-** | **14,675** | **1,631** | **-** | **-** | **37,806** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 537 | - | - | - | 537 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (499) | 499 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mikopo iliyofutwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (230) | - | - | - | (230) |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka 30.06.2022** | **21,500** | **-** | **14,483** | **2,130** | **-** | **-** | **38,113** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-22 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 240 | 724 | 1,356 | 1,823 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 531 | 394 | 1,644 | 620 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (518) | (9,925) | (14,294) | (1,154) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (657) | (9,885) | (4,310) | 4,999 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (3,962) | 8,517 | (196) | (4,343) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 292 | 1,028 | 432 | (379) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (882) | 2,713 | 80 | 3,879 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (187) | (187) | (560) | (657) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za*** | ***(5,142)*** | ***(6,621)*** | ***(15,848)*** | ***4,788*** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2) | (0) | (284) | (210) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | ***(2)*** | ***(0)*** | ***(284)*** | ***(210)*** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | - | - | - | - |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | **Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **(5,144)** | **(6,621)** | **(16,132)** | **4,578** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 34,106 | 40,727 | 45,094 | 32,540 |
| | **Robo Mwaka** | **28,962** | **34,106** | **28,962** | **37,118** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **Mr. Antaryami Sarangi Mkurugenzi Mkuu** | | **21.10.2022** |
| **Mr. Mahadhil M.Karwani Mkuu wa Fedha** | | **21.10.2022** |
| **Mr. Allen Richard Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | **21.10.2022** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| **1. Mr. Suitbert Kageuka - Mkurugenzi** | | **21.10.2022** |
| **2. Dr. Paul Kato - Mkurugenzi** | | **21.10.2022** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania tudumishe utamaduni kusaidiana

**KATIKA** gazeti la Nipashe toleo la jana, kulikuwa na habari ya mjane Amina Ali (75) ambaye anashindwa kuingia nyumbani kwake kutokana na majirani zake kujenga uzio, hivyo kulazimika kuruka ukuta ili kutimiza azma yake. Bibi huyo analazimika kufanya hivyo kutokana na majirani hao kushindwa kumpatia hata nafasi ya kupita kwa miguu.

Akisimulia mkasa huo, Amina wakati watu hawajawa wengi huko Mwapemba, Kata ya Toangoma wilayani Kigamboni, Dar es Salaam, alinunua nyumba eneo hilo miaka mingi lakini baadaye walipoingia aliwaita matajiri na kununua maeneo ya makazi, alijikuta nyumba yake ikizungukwa na kukosa nafasi ya kupita kutokana na kuingia kwake.

Licha ya kuwa katika mazingira hayo, mjane huyo alisema wakati watu hao wanaomzunguka wakijenga, alikuwa akiwafuata na kuwaeleza kuwa sehemu hiyo ni njia ya kuingilia na kutokea kwake walikuwa hawampi ushirikiano zaidi ya kumweleza kuwa hawana habari na kwamba hawakuelezwa kama anavyodai.

Kisa cha kutokuwa na njia ya kupita, kwa mujibu wa bibi huyo, ni jirani yake ambaye alidai kuwa amejenga geti katika sehemu ya kuingilia.

Kutokana na kadhia hiyo, Amina alichukua hatua kwenye mamlaka za serikali zikiwamo serikali ya mtaa, diwani wa kata na baraza la ardhi la kata ambako kote huko walijaribu kulipatia ufumbuzi suala lake lakini likagongwa mwamba.

Hatua hiyo pia imesababisha ahame nyumba hiyo ili kuepuka bughudha za kuruka ukuta ikizingatiwa kuwa ni mtu wa umri mkubwa.

Gazeti hili lilipomuuliza mmoja wa majirani anayelalalmikiwa kuziba njia hiyo, alitoa majibu ambayo hayaleti dalili za kupatikana kwa suluhu huku akiweka mkazo kuwa hilo ni eneo lake halali na mlalamikaji aulizwe awali alikuwa anapita njia gani. Katika kuonyesha kuwa hana hata chembe ya ubinadamu, jirani huyo alisisitiza kuwa yuko tayari kwenda kokote lakini si kuruhusu njia kumwezesha bibi huyo na jirani yake kupita.

Matatizo kama hayo yako sehemu mbalimbali na pia yamesababisha watu kutoana uhai na wakati mwingine baadhi ya waathirika kuelezwa kuwa kama wanaona kuna shida waende kwenye vyombo vya sheria au kulazimishwa kuhama maeneo yao kwa kuwauzia wale walio na migogoro nao.

Kwa undani, jambo kama hilo, linaonekana kabisa kukosekana kwa ubinadamu miongoni mwa majirani, hasa huyo ambaye anajibu kwa jeuri kwamba hayuko tayari kumwachia mjane huyo sehemu ya kupita kuingia na kutokea nyumbani kwake. Jambo la kujiuliza mtu kama huyo anapata wapi jeuri hiyo kwani ameitwa kwenye baraza la kata na kugoma kuitika wito.

Watanzania wengi kwa utamaduni wetu, tumekuwa na hulka ya kupendana na kushirikiana katika shida na raha pamoja na kuwahurumia watu wenye mahitaji wakiwamo wajane.

Ni vyema suala hilo likamalizwa kwa kukutanishwa majirani na hatimaye kila mmoja kuishi kwa amani badala ya uhasama na kutunishiana misuli.

Iwapo litashindikana, ni vyema mamlaka husika kama vile serikali na vyombo vya sheria pamoja na asasi za kutetea haki za binadamu zikaingilia kati na kutafuta suluhu ya jambo hilo.

Kubwa zaidi, ni vyema Watanzania tukarejea kwenye mila na desturi za kupendana na kuheshimiana badala ya kuwa na kiburi cha fedha na madaraka kwa wale waliobarikiwa kuwa navyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Mamlaka zichunguze maji ya chumvi mitaani

**KUWAPO** kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka pamoja na Usafi wa Mazingira mijini ni ufunguo wa upatikanaji maji kwenye maeneo mengi ambayo hayana majisafi wala salama.

Hadi sasa wapo wananchi wanaotumia huduma hiyo pamoja na wanyama pori na wafugwao vijijini na hata mijini.

Ni vyema taasisi hizo za serikali kusaidia kudhibiti bei za maji hasa yanayochimbwa mitaani ambayo 'cubic liter moja ni tangi la lita 1,000' wateja huuziwa kwa Shilingi 4,000.

Kinachosikitisha ni kwamba maji hayo yana chumvi, hayajapimwa kufahamu usafi na usalama wake kwa kuchunguzwa kimaabara lakini yamekuwa yakisambazwa kila mahali kutokana na ukweli kuwa kuna fursa ya kuuza maji ya kuchimba kutokana na ukosefu wa maji ya umma na kwa Dar es Salaam na Pwani ya DAWASA.

Ulishaji watu maji ya kuchimba kutoka visima vya ardhini pengine unahitaji ujazo na kupimwa, kazi inayoweza kufanywa na RUWASA au Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira.

Wakazi wa maeneo ya Msumi jijini Dar es Salaam ni miongoni mwa waathirika wa tatizo la maji kwa vile sehemu hiyo haina maji ya DAWASA, hivyo wakazi wake kutegemea maji ya mabondeni ambayo ni machafu lakini hayo ya kununua kutoka kwa wawekezaji wanaochimba maji ya chumvi.

Wengi wanaeleza katika mazungumzo na gazeti hili kuwa wanalazimika kununua mita, mabomba na vifaa vyote vya kuunganisha na kusambaza maji na kuvikabidhi kwa wawekezaji au wenye maji ili wawafikishie maji nyumbani kwao.

Wanasema maji hayo ni ghali na wengi huuza kipimo cha pipa la lita 1,000 kwa Shilingi 3,000 hadi 4,000 kila mwezi na wakati mwingine wanaouza huwauzia wateja Shilingi 150 kwa ndoo au dumu la lita 20.

Ukweli ni kwamba kama walivyosema watabiri kuwa vita vya tatu duniani vitakuwa ni vya maji, changamoto ya upatikanaji wa huduma hiyo hasa eneo la Msumi ni kubwa licha ya kwamba serikali inaendelea na juhudi za kufikisha maji maeneo hayo.

Kinachowaumiza wananchi hao ni ughali wa maji hayo ya chumvi ambayo huuzwa ghali kupindukia kwa kuwa si wote wenye uwezo wa kuyanunua na kulipa zaidi ya Shilingi 3,000 kwa pipa lenye ujazo wa lita 1,000.

Pamoja na kwamba DAWASA imeruhusu watu kuchimba visima na hata wenye magari kuuzia wateja na kuyasambaza hasa sehemu ambazo hazina maji ni vyema pia ikatazama upya eneo hilo.

Ni vyema DAWASA na hata RUWASA kushirikiana na wananchi hasa kwenye eneo la bei elekezi ya maji, kama wananchi wanavyojiuliza hivi ni sahihi kuuza maji ya chumvi kwa Shilingi 4,000 kwa pipa la lita 1,000?

Wana mawazo kuwa pengine ni wakati wa kuja na bei elekezi ya maji yanayouzwa mitaani kutokana na ughali wake pamoja na kuuchunguza ubora wa maji hayo kwanza.

Ni bora DAWASA ikazingatia kuwa wananchi wa kaya maskini hawana uwezo wa kununua maji hayo hasa kwa sababu walikuwa wanategemea maji mabondeni ambayo nayo yamekauka kutokana na upepo mkali na ukame unaotikisa karibu kila mkoa.

Pamoja na jitihada za kusambaza maji na kupanua vyanzo ili kuongeza kiwango cha maji yanayozalishwa na serikali, suala la kukagua visima vinavyochimbwa mitaani linahitaji jicho la serikali.

Pamoja na kuchunguza usalama wa maeneo na vyanzo yanapotoka maji hayo ili kazi zisifanyike kienyeji serikali itoe bei elekezi maana wakati mwingine wananchi wanalipia hata kuliko huduma wanayopata.

Wakati mwingine wananchi wanahisi kuwa iwapo DAWASA au RUWASA zitawaachia wafanyabiashara hao wenyewe bila udhibiti watazidi kuwaumiza wananchi hasa wakati huu wa janga la ukame linalotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

## TANGAZO

MCB BANK BETTER TOGETHER
Mwalimu Commercial Bank Plc

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-2021 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-2021 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 735 | 1,127 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 5,033 | 5,728 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 30 | 42 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 8 | 41 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 1,402 | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 9,795 | 14,083 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 57,485 | 49,235 |
| 12. Mali Nyingine | 4,299 | 4,349 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 893 | 965 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **79,680** | **75,570** |
| **B. DHIMA:** | - | - |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 60,057 | 55,510 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,606 | 1,629 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 260 | 1,218 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 92 | 77 |
| 27. Dhima Nyingine | 1,702 | 1,193 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **63,717** | **59,627** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,963** | **15,943** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | - | - |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (19,975) | (19,975) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 26 | 6 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,963** | **15,943** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | - | - |
| 39. Mikopo Chechefu | 581 | 604 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (382) | (382) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 20.0% | 21.1% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.0% | 1.2% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 95.1% | 88.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 71.7% | 64.6% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84.4% | 83.8% |
| - Ongezeko la Amana | 8.2% | 14.5% |
| - Ongezeko la Mali | 5.4% | 11.4% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-2022 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-2022 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 2,280 | 1,638 | 6,103 | 3,893 |
| 2. Gharama za Riba | 847 | 501 | 2,313 | 1,207 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,433** | **1,137** | **3,790** | **2,686** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | (21) |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 492 | 487 | 1,516 | 766 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | - | - | 4 | 1 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 464 | 470 | 1,404 | 748 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 28 | 17 | 108 | 17 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,899 | 1,589 | 5,273 | 4,789 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 788 | 702 | 2,355 | 2,131 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 1,111 | 887 | 2,918 | 2,658 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **26** | **35** | **32** | **(1,316)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 6 | - | 6 | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **20** | **35** | **26** | **(1,316)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **20** | **35** | **26** | **(1,316)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 61 | 55 | 61 | 55 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 0 | 1 | 1 | -21 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *0.0%* | *0.1%* | *0.0%* | *-2.8%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *0.1%* | *0.2%* | *0.2%* | *-8.1%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *98.6%* | *97.8%* | *99.4%* | *138.0%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *2.1%* | *2.5%* | *5.6%* | *5.8%* |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mtaji tangulizi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | 16,017 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 26 | - | 26 |
| Mengineyo | - | (80) | - | (80) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(19,949)** | **5,000** | **15,963** |
| **Mwaka Uliopita** | - | - | - | - |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (18,508) | 5,000 | 17,404 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (1,387) | - | (1,387) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(19,895)** | **5,000** | **16,017** |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-2022 | Robo Mwaka iliyopita 30-Juni-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Sep-2021 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | 26 | 101 | 32 | (1,316) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 313 | 367 | 932 | 1,015 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (15,394) | 5,224 | (21,602) | (18,531) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 14,289 | (2,694) | 21,337 | 20,640 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,793) | 528 | (1,196) | (161) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,176) | 363 | (1,033) | 191 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | (156) | 15 | (86) | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(3,890)** | **3,904** | **(1,616)** | **1,838** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (15) | (34) | (223) | (150) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(15)** | **(34)** | **(223)** | **(150)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | (3,905) | 3,870 | (1,839) | 1,688 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 8,039 | 4,169 | 6,051 | 4,485 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,134 | 8,039 | 4,212 | 6,173 |

### BAADHI YA MAELEZO
### KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2022

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ......................... (Imesainiwa) | 21 Septemba 2022 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ......................... (Imesainiwa) | 21 Septemba 2022 |
| Patrick Mashalla (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ......................... (Imesainiwa) | 21 Septemba 2022 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ......................... (Imesainiwa) | 21 Septemba 2022 |
| 2/ Enna V. Mwakipesile (Mkurugenzi) | ......................... (Imesainiwa) | 21 Septemba 2022 |




**Contact Info**
Mlimani Tower – Mezzanine Floor,
Sam Nujoma Road,
P.O. BOX 61002, Dar Es Salaam.
E – mail: info@mcb.co.tz
Call: 0800 750 033

Visit: www.mwalimubank.co.tz



Baadhi ya wakufunzi ambao ni wataalamu wa afya, wakipata mafunzo ya kujikinga na ugonjwa wa ebola yaliyoandaliwa na Wizara ya Afya na Shirika la Afya Duniani (WHO), mjini Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watu 500 wasaidia kudhibiti moto Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VIKOSI vya uokozi kutoka vitengo mbalimbali vinavyoendelea na juhudi za kuuzima moto unaoendelea kwa siku ya tano sasa, kuiteketeza Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA), vimefanikiwa kuudhibiti moto huo baada ya serikali kuongeza nguvu zaidi, kwa kupeleka zaidi ya watu 500 Mlima Kilimanjaro.

Jana, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, wakati anatoa taarifa kuhusu juhudi hizo, alisema hadi kufikia Oktoba 23 jioni, moto huo ulikuwa umedhibitiwa katika maeneo mengi ya mlima huo, ikiwamo Kituo cha Millenium kuelekea Marangu Hut na Mweka Hut.

Moto huo uliozuka Ijumaa ya Oktoba 21 mwaka huu, majira ya usiku, umeunguza na kuteketeza eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 2.5, sawa na asilimia 0.4 ya hifadhi hiyo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,712.

"Juhudi zaidi zimelekezwa kwenye eneo lenye korongo kubwa la Karanga, ambako vikosi vinavyoendelea na kazi ya kuzima moto, viko katika eneo hilo kuhakikisha moto unadhibitiwa. Nichukue nafasi hii kuwashukuru wadau wote ambao wamejitokeza kuudhibiti moto huo.

"Vilevile, niushukuru sana uongozi wa mkoa, ambao tumekuwa nao bega kwa bega pamoja na mawaziri mbalimbali, wadau wa utalii na uhifadhi kutoka kampuni mbalimbali za utalii nchini, wanahabari, mashirika na wananchi, kutokana na juhudi walizoonyesha kuhakikisha mlima wetu unakuwa salama."

Aidha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ambaye alikwenda kuzuru eneo linaloteketea kwa moto, amewaagiza wataalamu wa wizara yake kufanya tathmini na utafiti ili kubaini chanzo cha moto katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, kujirudia mara kwa mara.

"Nimefika eneo la tukio, nimeona kazi ya kuudhibiti moto inakwenda vizuri na mafanikio ni makubwa. Ila tumewaelekeza wataalamu, baada ya kuudhibiti moto huu, sasa ifanyike tathmini na utafiti kubaini nini kilitokea.

"Hatuwezi kujua nini kilisababisha moto huu, hivyo ifanyike tathmini na utafiti kubaini chanzo cha moto ili kudhibiti hali hii kujirudia mara kwa mara na kuepusha athari zinazoweza kutokea za kimazingira, maliasili na utalii. Niwatoe hofu Watanzania, hali ni nzuri na nimefika eneo la tukio, watalii wanaendelea na shughuli za utalii bila shida yoyote na zaidi ya timu ya watu 459 wapo wakiendelea kuudhibiti moto huo."

Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), William Mwakilema alisema; "Tumefuatilia kwa picha za setilite jana usiku moto ulikuwa kwenye eneo moja na leo asubuhi moto ulikuwa umepungua sana na saa 11 jioni ya leo tumefuatilia picha inaonyesha moto umedhibitiwa kwa kiasi kikubwa na kwa sasa nguvu itaendelea kuwapo na vikosi vilivyopo vitapitia maeneo yote kuhakikisha moto umeisha."

Moto huo ulioanza kuwaka mwishoni mwa wiki iliyopita, uligunduliwa katika eneo la kupumzikia wageni maarufu 'Karanga Camp' kuelekea Baranco, ukiwa unatembea kwa kasi zaidi ukiteketeza sehemu kubwa ya miti ya asili ya hifadhi hiyo.

Mara ya mwisho moto kama huo ulizuka na kuteketeza sehemu ya hifadhi hiyo, Oktoba 11, 2020 katika eneo la Whona, ambacho ni kituo cha kupumzikia wageni wanaotumia njia ya Mandara na Horombo.

Kanzidata ya Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, inaonyesha kuwa mwaka 2015/16 eneo lililoteketea kwa moto ni hekta 49.13, mwaka 2016/17 hekta 17, mwaka 2017/18 hekta 82, mwaka 2018/19 hekta 72.3, mwaka 2020 hekta 22.05.

Kwa kipindi kisichozidi miaka mitano mpaka kufikia mwaka 2020, jumla ya hekta ambazo ziliteketea kwa moto katika hifadhi hiyo zinatajwa kufikia 242.48, huku sababu kubwa ya kuzuka kwa moto katika eneo hilo ikielezwa uvunaji mbaya wa asali, ujangili na njia mbaya za kilimo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi ya mwaka 2020/21 iliyotolewa Machi 30, mwaka huu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, alisema amefanya uchunguzi kuhusu ripoti ya tukio la moto la KINAPA la Desemba 2020 na kutoa mapendekezo manne kwa mamlaka husika.

CAG Kichere, alisema moto huo ulisababisha hasara ya jumla ya Sh. bilioni 1.214 na kubainisha kuwa mamlaka za hifadhi za taifa hazina uwezo wa vifaa na maandalizi ya kupambana na majanga ya asili.

# IGP aunda timu kuchunguza mauaji Kilombero

**Owen Bariki, TUDARCo na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi nchini, limefafanua kuhusu mauaji ya watu wawili na wengine kujeruhiwa wakati jeshi hilo likiwa kwenye harakati za kuzuia uvunjifu wa amani katika kijiji cha Ikwambi, Kata ya Mofu Tarafa ya Mngeta wilayani Kilombero, mkoani Morogoro.

Aidha, limeunda timu maalum chini ya uongozi wa Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) na taasisi nyingine za serikali kuchunguza tukio hilo.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolea jana na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, polisi walilazimika kutumia nguvu, kuwaokoa viongozi wa kijiji waliofungiwa ofisini na wananchi hao wakitaka kuwachoma moto.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi baada ya wakulima waliokuwa na malalamiko dhidi ya wafugaji waliolisha mifugo mashamba yao na wenzao wawili walojeruhiwa na kundi hilo.

IGP Wambura alisema kutokana na malalamiko hayo wananchi wa jamii ya wakulima walichukua sheria mkononi kwa kuwakamata viongozi wa kijiji cha Ikwambi pamoja na mkaguzi wa kata hiyo na kuwafungia ofisi ya kijiji.

"Juzi majira ya mchana askari polisi walipofika eneo la tukio kwa lengo la kuwaokoa viongozi hao, kulitokea tafrani zilizosababisha matumizi ya risasi za moto pamoja na mabomu ya machozi na kusababisha mauaji ya watu wawili," alibainisha.

Alisema timu hiyo itabainisha pia uwiano wa matumizi ya nguvu iliyotumiwa na Jeshi la Polisi katika kudhibiti vurugu hizo kama ilikwenda sambamba na vurugu zenyewe.

"Kwanza niwatake wananchi wa Kijiji cha Ikwambi wawe wavumilivu na kutoa ushirikiano wakati timu hii inakwenda kufanya kazi ya uchunguzi," alisema.

Aidha, aliagiza polisi waliohusika na tukio hilo wakae kando kupisha uchunguzi huru ili Watanzania wafahamu ukweli wote.

Pia, alimtaka Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kilombero, kutoa ushirikiano kwa timu hiyo inayokwenda kuchunguza na ukibainika uzembe hatua za kisheria zitachukuliwa.

Awali, ilidaiwa watu hao walifariki dunia na wengine wawili akiwamo diwani wa kata ya Mofu kujeruhiwa na Polisi baada ya vurugu kuibuka katika ofisi ya Serikali ya Kijiji baada ya baadhi ya viongozi kufungiwa ndani ya ofisi hiyo na kutaka kuchomwa moto.

Ilidaiwa polisi walilazimika kutumia risasi za moto kuzuia wananchi waliowafungia ofisini baadhi ya viongozi na kuchoma moto ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa kilichodaiwa kutoridhishwa na maamuzi yanayotolewa inapotokea migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mwenyekiti mstaafu wa Kijiji cha Ikwambi, Victor Timbulu, alisema miongoni mwa waliojeruhiwa ni Diwani wa Kata ya Mofu Greyson Mgonera maarufu kama Obama.

Timbulu alidai, Oktoba 24 majira ya mchana viongozi wa kijiji na kata wakiwa kwenye kikao, walivamiwa na wananchi walioandamana kwenda ofisi hizo na kuamua kuchoma moto ofisi huku wakiwalalamikia viongozi kuwapendelea wafugaji.

Alidai wananchi hao wanapopeleka malalamiko kuhusu wafugaji, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa dhidi ya watuhumiwa.

Alitoa mfano juzi, wakulima takribani kumi walidaiwa kupigwa na wafugaji na kuripoti tukio hilo katika kituo kidogo cha polisi lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

"Majira ya saa mbili asubuhi jana baada ya tukio hilo wananchi wakavamia ofisi na kuwafunga kamba wenyeviti wawili wa vitongoji vya Igia na Milamila baadaye wakamfuata Mwenyekiti wa Kijiji kanisani na kumfunga kamba na kumfuata Mkuu wa Polisi kata naye wakamkamata," alidai mwenyekiti huyo mstaafu.

Diwani wa Mofu alisema alipata matibabu katika Hospitali ya St Francis Ifakara na kuruhusiwa kurudi nyumbani.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi, alikiri kuwapo kwa tukio hilo ambalo alipata taarifa zake wakati akiwa mjini Morogoro.

Kamishna Jenerali wa Polisi, Camillius Wambura, akizungumza na vyombo vya habari, alikiri askari Polisi kuhusika na mauaji hayo kwa kutumia silaha za moto wakati wakizuia uvunjifu wa amani.

"Chanzo cha tukio hili la mauaji ni wakulima kuwa na malalamiko ya wananchi wengine jamii ya wafugaji kulisha mifugo kwenye mazao yao, na wenzao wawili kushambuliwa na wafugaji tarehe 22 mwezi wa kumi mwaka huu, na wananchi hao wakaamua kuwakamata baadhi ya viongozi wa kijiji, watendaji na kuwafungia ndani ya ofisi," alisema CGP Wambura.

Alisema miongoni mwa waliokamatwa ni viongozi wa kijiji, watendaji, kata na Mkaguzi wa Polisi kata.

HABARI KITAIFA

## TGNP yawakutanisha wanaharakati 25 duniani kujadili vuguvugu la haki

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umewakutanisha pamoja wanaharakati 25 kutoka nchi sita duniani, kushirikishana mbinu mpya za kukabili ukatili wa kijinsia na haki mbalimbali ikiwamo ujenzi imara wa vuguvugu la mapambano ya usawa.

Akifungua mafunzo hayo jana, Mjumbe wa Bodi wa TGNP, Dk. Ng'wanza Kamata alisema mafunzo hayo ni ya siku sita kwa washiriki kutoka India, Bangladesh, Zambia, Ethiopia, Zimbabwe, Kenya na Tanzania kwa kuimarisha nguvu ya mashirika yanayotetea haki za wanawake, ili kuimarisha uwezo wa kuendelea kudai usawa na haki. "Yatajikita katika kuwawezesha wanawake na washirika wao kupanga mipango ya uragibishi na utekelezaji wake, ili kuimarisha uwezo wao wa kupigania usawa wa kijinsia," alisema na kuongeza:

"Ujenzi wa vuguvugu la ukombozi wa wanawake (TAPO) ndiyo nguvu kubwa ya pekee inayoweza kuimarisha na kuharakisha matokeo ya mapambano ya wanawake katika kutafuta haki na usawa zaidi, watafundishwa mbinu za ujenzi na uimarishaji."

Alisema uwapo wa vuguvugu hilo unajumuisha watu wengi zaidi na kuwa na umoja wenye nguvu zaidi katika kupigania na kudai haki za wanawake na watoto.

Naye Mkuu wa Programu wa TGNP, Clara Kalanga, alisema mafunzo hayo yameandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha namna ya kufanya uchechemuzi kwenye masuala ya jinsia na kwamba watamaliza wakiwa na mbinu mpya na uwezo wa kutekeleza miradi kwenye maeneo yao.

"Pia watatembelea kituo cha taarifa na maarifa cha Saranga kwenda kuangalia namna wanafanya uchechemuzi ngazi ya jamii...mafunzo haya yamekuja sasa kwasababu tumeona dunia inavyokwenda lazima kujenga vuguvugu lenye nguvu ya pamoja kwa mashirika ya wanawake, ili kuwa na sauti imara," alisema Kalanga aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi.

Naye Mwakilishi wa wanawake Mkoa wa Mbeya ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisema changamoto za wanawake ni nyingi ikiwamo kujua misingi ya kusimamia kufanya mambo yao kwa kuwa wengi wanafanyabiashara wanakopa kwasababu hawana uelewa.

Alisema licha ya kuwa mbunge, lakini anaendesha shirika lisilo la kiserikali lililomwezesha kupata tuzo mbili na kwamba mafunzo kwa wanawake ni muhimu ili wanapokopa wajue fedha watazitumia kwa shughuli gani.

"Watunga sera tunapaswa kusimamia kilichotupeleka bungeni lazima tuseme, tunahitaji wanawake wafanyiwe mafunzo ya mara kwa mara, wasipewe mikopo bila kuelimishwa vizuri juu ya kile wanachokifanya hasa kwenye mikopo na ujasiriamali," alisema.

Naye Mwakilishi wa Shirika la COADY nchini Canada, Sarika Sinha, alisema wameamua kushirikiana na TGNP kujenga vuguvugu imara kwa kuwa ndilo litakaloweta pamoja wanawake na kupaza sauti imara katika kupinga ukatili wa kijinsia.

# Vijana 40 waungana kutafuta ufumbuzi wa foleni Dar

**Na Romana Mallya**

VIJANA 40 wameamua kutafutia ufumbuzi changamoto ya foleni inayowakabili watumiaji wa barabara za mkoani Dar es Salaam, baada ya Shirika lisilo la Kiserikali la Ujuzi Forum kuwapa mafunzo ya kutumia teknolojia kufanya mabadiliko.

Mafunzo hayo yaliyoendeshwa kwa siku tatu na shirika linalohusisha vijana wa kike na wa kiume kutoka shule za msingi hadi vyuo vikuu wenye umri wa miaka 12 hadi 25.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la UJUZI, Kai Maembe, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwasaidia vijana wanapomaliza shule waweze kujiajiri au kuajiriwa wakiwa na ujuzi.

"Ujuzi tunaowapa ni ule unaohitajika katika soko la ajira, kama unavyofahamu kuna kelele nyingi wahitimu waliowengi hawana ajira, tumeamua kuwapa ujuzi unaohitajika katika soko, tunawafundisha namna ya kutumia teknolojia kufanya mabadiliko katika jamii.

"Mfano, barabara nyingi za Dar es Salaam hasa wakati wa asubuhi na jioni zimekuwa na tatizo la foleni ambazo zinasababisha watu kuchelewa kwenye shughuli za uzalishaji ambazo ndizo zinazochangia kukua kwa kiuchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja."

Alisema kwa kutambua changamoto hiyo, wameamua kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapa mafunzo, ili waje na ufumbuzi wake kwa kutumia teknolojia kuunda programu (APP) ambayo watu wataitumia kuondokana na foleni.

Pia alisema lengo la mafunzo hayo ni vijana wanapomaliza masomo, wawe na ujuzi wa kubuni vitu vitakavyosaidia changamoto mbalimbali ndani ya jamii.

Alisema wamewachukua watoto wa umri kuanzia miaka 12 hadi 17 ili wakiwa shule kile watakachofundishwa waweze kuoanisha na elimu ya ujuzi waliyopatiwa na kwa vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 25 wanaamini suala la kuanzisha kampuni zao wenyewe ni kitu wanachokitegemea kutokana na ukosefu wa ajira.

Maembe alisema pamoja na kushirikiana na serikali, wanaomba itambue mchango unaotolewa kwa vijana ili uwe na matokeo chanya ndani ya jamii na kwa taifa.

Alisema mafunzo hayo ni endelevu na wamepanga kuwafikia vijana katika mikoa mingine ikiwamo Arusha, Dodoma, Iringa na Visiwani Zanzibar.

Mjumbe wa Bodi ya T-Marc Tanzania, Awaichi Mawalla, alisema wameamua kushirikiana na UJUZI kutoa fursa hiyo kwa vijana ambao wataleta mabadiliko kwenye jamii na kwa taifa.

Zuhura Mattaka (11) mwanafunzi wa Shule ya Msingi Fedha, alisema amejifunza pia kuwa mtoto wa kike anapoona kitu hatakiwi kunyamaza anapaswa kufunguka ili kama ni kibaya asaidiwe haraka kabla ya tatizo kuwa kubwa. Mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Elizabeth Senkoro, alisema mafunzo ya kumwongezea ujuzi kijana ni ya muhimu kwa sasa kutokana na ukuaji wa sayansi na teknolojia na hali ya soko la ajira.

Mwanafunzi wa Kidato cha Tano, Victor Mungereza katika Shule ya Sekondari Loyolla, alitaka serikali irekebishe mfumo wa elimu, ili vijana wenye bunifu shuleni ziweze kuendelezwa tangu wakiwa wadogo badala ya kusubiri akihitimu.



Khatibu Ally, akimtwisha ndoo ya maji mkazi wa Kitongoji cha Ilala wilayani Mkalama, Aisha Ramadhani, baada kuzindua kisima alichokichimba kusaidia wananchi wa kitongoji hicho. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

## Familia yachimba visima vya maji kusaidia wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIKA kuunga juhudi za serikali za kupunguza tatizo la maji kwa wananchi, visima sita vilivyogharimu mamilioni ya fedha vimechimbwa na familia ya Said Ally Magid, katika wilaya tatu za mkoa huo.

Mdau wa maendeleo wa familia hiyo, Khatibu Said alisema hayo jana wakati akikabidhi kisima kilichochimbwa katika Kitongoji cha Ilala, Kijiji cha Ntondo, wilayani Mkalama jana na visima vyote vilivyochimbwa wananchi wanapata huduma ya maji bure.

"Familia ya Mzee Said Ally Magid imeamua kuchimba visima hivyo kama msaada kwa wananchi wote bila kujali dini wala kabila na kuunga mkono juhudi za serikali za kumtua ndoa kichwani mwanamke," alisema.

Ally alitaja maeneo ambako visima hivyo vimechimbwa kuwa ni Nyuki Mizani, Sido na Mandewa, vyote katika Manispaa ya Singida.

Alitaja maeneo mengine kuwa ni katika Kijiji cha Kyengege na Mgundu vilivyoko wilayani Iramba na Kijiji cha Ntondo wilayani Mkalama.

Ally aliwaomba wananchi waliobahatika kuchimbiwa visima hivyo kuvitunza ili vidumu kwa muda mrefu na kuahidi kuendelea kuchimba vingine zaidi maeneo mengine yenye tatizo la maji mkoani humo.

Kwa upande wao, wananchi wa Kitongoji cha Ilala wakizungumza baada ya kukabidhiwa kisima, walimshukuru mdau huyo kwa msaada huo na kumwahidi kukitunza.

Zurika Magula, mkazi wa kitongoji hicho alisema kwa muda mrefu walikuwa wakipata tabu ya maji na kusababisha ugomvi kwenye ndoa zao wanapochukua muda mrefu kwenda kutafuta maji.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Ntondo, Zuberi Mwilu, alisema kuchimbwa kwa kisima hicho kutasaidia huduma ya maji kaya 480 ambazo kwa muda mrefu walikuwa wakipata tabu ya maji.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ilala, Joseph Shilla, alisema wananchi walikuwa wakitembea umbali mrefu zaidi ya kilomita moja kwenda kutafuta maji, kisima hicho kitakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi.

# Chumvi nyingi chanzo magonjwa ya moyo

**Na Shaban Njia,** BUKOMBE

MATUMIZI ya chumvi nyingi katika chakula yametajwa kuwa miongoni mwa visababishi vya magonjwa ya moyo kwa watu wengi katika jamii na kuhatarisha maisha yao.

Hayo yamebainishwa na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo wa Hospitali ya Rufani Kanda Bugando, Prof. William Mahalu, wakati akitoa huduma ya matibabu ya moyo bila malipo katika Kliniki ya Baraka Charles Kulwa Memorial Hospitali wilayani Bukombe mkoani Geita.

Alisema kuna aina mbili za magonjwa ya moyo, wa kuzaliwa nao na mtu anaopata katika matumizi ya vyakula mbalimbali, ikiwa ni pamoja na chumvi nyingi.

Alieleza pamoja na sababu hiyo mtu anaweza kupata ugonjwa wa moyo kutokana na matumizi ya sigara, kutokujishughulisha na kazi mbalimbali pamoja na vyakula vyenye mafuta mengi.

Prof. Mahalu alisema Siku ya Moyo Duniani, wanaifanya kwa kuwafikia wananchi na kuwapatia elimu ya ugonjwa huo na dalili zake ili kufahamu chanzo chake na jinsi ya kujikinga.

"Magonjwa mengi yanayowakabili binadamu ni endelevu na ndio maana tunashauri watu wanapobaini kupata dalili ndani ya mwili ambazo sio nzuri kufika katika vituo vya afya kupata matibabu," alisema Prof. Mahalu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Hospitali ya Charles Kulwa Memorial Baraka, Charles Kulwa, alisema wamekuwa wakishirikiana na madaktari bingwa kutoa huduma mara kwa mara kwa wananchi, kwa wiki wanatoa mara moja bila malipo.

Mmoja wa wakazi wa Bukombe, Swaum Ibrahimu, alisema awali alikuwa hafahamu kama chumvi inaweza kuwa chanzo kikubwa cha kupata ugonjwa wa moyo na atahakikisha anaitumia kwa makini ili kumletea shida na kushindwa kutimiza ndoto zake za kimaisha.

Naye Nicodemas Lucas aliomba elimu hiyo itolewe katika vituo vya afya hususan kliniki ili wajawazito wanaopofika kujua maendeleo ya mtoto tumboni wafahamu kuwa chumvi ni chanzo cha kupata ugonjwa huo.



Aliyekuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Boniphace Luhende (kulia) ambaye sasa ni Wakili Mkuu wa Serikali, akimkabidhi vitendea kazi Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Sara Mwaipopo, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yamwachia huru Ofisa Maliasili

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya Geita imemwachia huru Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghwale, Asaph Manya (48), baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha makosa aliyokuwa akikabiliwa.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samwel Maweda, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha makosa yote matatu pasipokuacha shaka.

Hakimu Maweda alisema mshtakiwa huyo alikuwa anakabiliwa na makosa matatu ya kushawishi rushwa ya Sh. milioni 15 na kupokea Sh. milioni 4.1 kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 kama ilivyofanyiwa mapitio ya mwaka 2019.

Maweda alisema upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri ambaye alipeleka mahakamani mashahidi 18 na vielelezo vitatu.

Pia alisema upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na wakili wa kujitegemea Beatus Masaka, ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa.

Hakimu Maweda alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha makosa yote matatu na mshtakiwa anaachiwa huru.

Aidha, alisema upande wa mashtaka ulipeleka mahakamani mashahidi 18 ambao walidai kuwa walimwona mshtakiwa akiwa na mfuko, lakini katika mashahidi wote hao hakuna aliyemuona mshtakiwa akipokea Sh. milioni 4.1.

"Kwani ukimuona mtu anatembea na mfuko tu unadai kwenye mfuko kuna fedha za rushwa, kama kwenye mfuko kuna nyama, kwa kuwa hakuna shahidi aliyemuona mshtakiwa akipokea fedha, mahakama hii inamuachia huru mshtakiwa, lakini upande wa mashtaka unajukumu la kuthibitisha kosa pasipokuacha shaka yoyote, kutokana na upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha makosa yote matatu yaliyokuwa yakimkabili mshtakiwa namuachia huru," alifafanua Hakimu Maweda.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa TAKUKURU Mkoa wa Geita, Murusuri alidai kuwa kati ya Januari na Aprili 2021, mshtakiwa akiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghwale, Mkoa wa Geita aliomba rushwa ya Sh. milioni 15 kutoka kwa wananchi wa Kitongoji cha Ndati Kijiji cha Shabaka kupitia kwa mtu mmoja, Kazimili Busweke kama kishawishi cha kuwasaidia kuendelea kuishi katika Hifadhi ya Misitu ya Mienze wakati wa operesheni ya mipaka.

Murusuri aliendelea kudai kuwa kosa la pili mshtakiwa huyo ni kupokea rushwa ya Sh. milioni 4.1 kutoka kwa wananchi wawili, Kazimili Busweke na Wiliam Rushika kama wawakilishi wa wananchi wa kitongoji cha Ndati.

Mwendesha Mashtaka huyo alidai, kosa la tatu ni kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kinyume na kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa mapitio mwaka 2019.

# BoT yawataka wafanyakazi taasisi za fedha uadilifu

**Na Beatrice Moses**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imebainisha baadhi ya wafanyakazi wa taasisi za fedha (benki) wasio waaminifu na wasiozingatia uadilifu kwenye kazi zao kusababisha hasara kwa benki zao na kuzua hofu kwa wateja kutumia huduma zao na kuchelewesha kukua kwa uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Msimamizi wa Sekta ya Fedha, Sadati Mussa, alisema hayo alipomwakilisha Gavana wa BoT ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Benki (TIOB), kwenye mahafali ya 21 ya taasisi hiyo yaliyofanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Aliwataka wafanyakazi wa taasisi hizo kuzingatia maadili ya huduma za benki kuwa waaminifu na kudumisha uadilifu.

"Tumeona mifano mingi baadhi ya wafanyakazi kutokuwa waaminifu hivyo kusababisha hofu kwa wananchi kusita kutumia huduma za benki mwananchi anapopata hasara kwenye miamala yake au mikopo inamfanya asiwe karibu na benki," alisema.

Alisema, anaamini kuwa wahitimu hao watazingatia maadili kwa kuwa ni sehemu ya mafunzo ya msingi waliyoyapata kupitia kozi maalum ambayo inasisitizwa uaminifu ni jambo la kwanza kwa mfanyakazi wa benki wakati anapotekeleza majukumu yake.

Kwa upande wake, Dk. Charles Kimei, alizitaka taasisi za kifedha zijitahidi kupunguza tozo kwa wateja wao ili kuwavutia kutumia huduma hizo.

Alisema uelewa wa bidhaa za huduma za kibenki kwa namna ya kisasa umebadilika, wahitimu wamejifunza mambo ambayo yanaendeana na huduma za kisasa za benki.

"Mafunzo haya yanaendana na karne hii ikiwamo kumudu kuunda programu maalum za kutoa huduma kwa wateja wao," alisema Dk. Kimei.

Alifurahishwa na mwitikio mkubwa wa wanawake katika huduma za fedha benki, aliwataka watumie vyema taaluma yao badala ya kubweteka wahakikishe wanajituma kwenye jamii ikiwamo kutoa elimu ya ujasiriamali.

Pia taasisi za kifedha zijikite kuhabarisha wateja wake kuhusu kuwapo kwa uhalifu wa kimtandao ili wateja waweze kuwa salama na fedha zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya TIOB, Patrick Mususa, aliwapongeza wahitimu wote akiamini wataongeza chachu katika huduma za kifedha.

Katika mahafali hayo tuzo kwa wanachama wa daraja la juu kwenye sekta fedha ilitolewa kwa wataalamu wa masuala ya kibenki kutokana na michango yao ya hali na mali, waliopewa tuzo hiyo ni pamoja na Hayati Profesa Benno Ndulu, tuzo yake ilikabidhiwa kwa binti yake, wengine ni Dk. Charles Kimei, Abdulmajid Nsekela, Cosmas Kimario na Ruth Mkurugenizi wa Benki ya NMB.



# NGO zatakiwa kuweka mifumo itakayowaongezea kipato wananchi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS wa Foundation For Civil Society (FCS), Dk. Stigmata Tenga, ameagiza taasisi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali kuweka mifumo yenye dira thabiti na sera wezeshi zitakazowasaidia kuongeza kipato badala ya kuwategemea wahisani.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha wakati wa mkutano wa AZAKI ambao umewakutanisha washiriki zaidi ya 500 kutoka mashirika na taasisi mbalimbali.

Alisema endapo wakibadilisha mifumo hiyo itasaidia kuleta maendeleo kwa kuwa itawaunganisha wananchi na mhimili mingine ya kutoa uamuzi kuhusu suala husika.

Hata hivyo alisema wakiwa kwenye mkutano huo wataangalia namna ya kuimarisha ushirikiano kati yao na serikali, Bunge na wananchi.

"Kutajaribu kufanya uchanguzi wa kina kwa kuangalia matatizo yanayowakabili wananchi kwa kuwa sisi ni sauti ya wananchi wasiokuwa na sauti,"alisema.

Kadhalika alisema watajadiliana njia ya kuendelea kuimarisha tunu za nchi za Afrika ili kuepukana na mianya ya kuonyooshewa vidole au kubanwa na serikali kwa aina yoyote.

"Asasi za kiraia zinanguvu kubwa ya kuleta mabadiliko kwa kuwa ziko karibu na wananchi, pia zimejikita kutatua matatizo yanayowakabili, hivyo tuendelee kuzikumbuka tunu zetu, ikiwamo kuwa wawajibikaji, uwazi, upendo, amani na ushirikiano,"alisema.

Akizungumza kwa niaba ya sekta binafsi, Kai Mollel kutoka Benki ya Stanbic, alisema benki hiyo inashiriki katika mijadala na shughuli mbalimbali za kimaendeleo kwa jamii kupata fursa ambazo zinatokana na uwekezaji.

Alisema watahakikisha kwa watu ambao ni wabunifu wanapata solo la uhakika na huduma za kifedha.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Trademake East Afrika, Dk. Anthony Mveyange, alisema nchi za kiafrika zinakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwamo ya umaskini, ajira, kukosa huduma ya maji na elimu.

Alisema: "Wananchi wa Afrika wanashida nyingi, ukiangalia asilimia 37 hawana ajira, asilimia 20 ni maskini, asilimia 23 hawajasona na asilimia 23 hawana huduma ya majisafi na salama, hivyo kwa wiki nzima tunatakiwa kujikita kuangalia namna ya kusaidia watu wetu."

# Serikali yafufua vyuo saba vya watu wenye ulemavu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali inajivunia kuvifufua vyuo saba vilivyokuwa vimeanzishwa kwa ajili ya kutoa taaluma mbalimbali kwa jamii ya watu wenye ulemavu nchini.

Vyuo vilivyorejeshwa tena ili kuanza kutoa huduma kwa jamii hiyo ni Rwenzali (Tabora), Sabasaba (Singida), Yombo (Dar es Salaam), Mutapika (Masasi) na Masiwani (Tanga).

Katambi alisema uamuzi wa kuvifufua vyuo hivyo ulitokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kutenga Sh. bilioni tatu za kuvihuisha vyuo hivyo. "Hivi vyuo saba ambavyo ni maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu vilivyofufuliwa na serikali, vilikuwa havifanyi kazi lakini sasa vimeanza kufanya kazi tangu Rais Samia, alipoingia madarakani. Sasa ili kuimarisha miundombinu ya vyuo hivyo, ndiyo maana serikali ikatoa fedha hizo ili kuboresha mazingira ya vyuo vya wenye ulemavu waweze kupata elimu.

"Ninyi ni mashahidi kwamba watu wenye ulemavu wakipewa kazi ni waaminifu na wanafanya kazi vizuri kuliko watu ambao wasio walemavu. Kwa sababu ya unyeti wa hilo, serikali inaenda kujipanga kuhakikisha inatungwa sheria ambayo itasimamia alama za barabarani ili zifuatwe na watumiaji wa barabara bila kuathiri jamii ya watu wenye ulemavu."

Juzi serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu mgawanyo wa ajira za umma kwa makundi maalum, ikisema jamii ya watu wenye ulemavu imenufaika na ajira mpya 261, kati ya ajira 9,800 zilizotolewa hivi karibuni na sekta mbalimbali karibuni.

Alizikumbusha taasisi za serikali zinapotangaza ajira, zihakikishe wana waajiri watu wenye ulemavu, kwa kuwa ni takwa la kisheria ambalo lipo kwenye Sheria ya Walemavu, Namba 9 ya Mwaka 2010, ambayo inawataka kila watu wanaowaajiri waajiri asilimia tatu ya watu wenye ulemavu.



Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Manyara (MNRPC), Mary Margwe, akizungumza katika mkutano mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) CCM Wilaya ya Simanjiro, kuhusu waandishi wa habari kushirikiana na viongozi ili kutatua changamoto zao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TAKUKURU yashauriwa kubuni mbinu kudhibiti rushwa ya ngono

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

KAMISHNA wa Tume ya Utumishi wa Umma nchini, Balozi Adadi Rajabu, ameishauri Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), kuhakikisha wana buni mbinu zinazoweza kudhibiti vitendo vya rushwa ya ngono nchini.

Balozi Adadi alitoa ushauri huo wakati wa mahafali ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari Muheza Muslim.

"Vitendo vya rushwa ya ngono vipo tu tangu TAKUKURU walipopewa jukumu la kudhibiti vitendo hivyo. Naona ni wakati sahihi kuhakikisha wanakuja na mwarobaini wake. Wao wanapaswa kuona namna nzuri ya kubuni mbinu ambazo zinaweza kupelekea kudhibiti badala ya kusubiri matukio yanatokea ndio waweze kuanza kupambana nayo.

"Haya mambo yapo kwa sababu kwenye vyuo hivyo ni jinsi ya vyombo vilivyo kabidhiwa kufanya kazi hiyo wanafanya nini ili kuweza kuondokana na tatizo hilo. Tunataka wanaofanya vitendo hivyo wakamatwe ili iweze kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia za namna hiyo kuweza kubadilika hivyo suala hili lina umuhimu wake hasa chombo ambacho kimepewa mamlaka ya kusimamia.


Aidha, Balozi Adadi aliwahimiza wanafunzi katika shule hiyo kuhakikisha wanasoma kwa bidii ili wataalamu mbalimbali waweze kupatikana.

Alisema ni lazima wanapokuwa shuleni waweze kujiandaa na kuzingatia nidhamu, malengo na kusoma vizuri ili baadaye waje kufanikiwa kupitia elimu.

Balozi Adadi aliwaambia kwamba mitihani inahitaji maandalizi mazuri ili waweze kufanya vema, hivyo hawana budi kuhakikisha wanajiandaa.

Katika mahafali hayo, Balozi Adadi, aliendesha harambee kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya maabara katika shule hiyo, huku akiahidi kuendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha wanapata mafanikio.

Pia aliuomba uongozi wa shule kwamba ujenzi wa maabara utakapokamilika ipewe jina la Bahoza Laboratory ili kuwaenzi kwa juhudi kubwa ambazo wamezifanya kufanikisha maabara hiyo.





# Serikali yaunda kamati kuchunguza chanzo cha ghala kuungua moto

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SIKU mbili baada ya ghala la Mamlaka ya Mapato (TRA) Mkoa wa Tanga ambalo lilikuwa limehifadhi shehena ya bidhaa za magendo kuteketea kwa moto, serikali imeunda kamati maalum ya watu 11 kuchunguza kama tukio hilo ni hujuma au hitilafu ya miundombinu ya umeme ya ghala hilo.

Aidha, imetaka kuchunguzwa mjumbe mmoja wa Kamati ya Kuzuia Magendo ya Mkoa, aliyetajwa kwa jina moja la Kisaka, ambaye anatuhumiwa moto ulivyotokea, alipigiwa simu ili aweze kutoa taarifa lakini mpaka asubuhi simu iliita haikupokelewa.

Akitangaza uamuzi wa kuundwa kwa kamati hiyo jana, Mkuu wa Mkoa huo, Omari Mgumba, alisema kamati hiyo ya wataalamu wa kada mbalimbali itafanya kazi ya uchunguzi ndani ya siku saba na baadaye itawasilisha ripoti yake kwake.

Ghala hilo kabla ya kuteketekea, lililkuwa limehifadhi bidhaa mbalimbali zikiwamo mabalo ya vitenge 370, sukari, mchele, mafuta ya kupikia na pikipiki zilizoshindwa kulipiwa ushuru na wafanyabiashara walioingiza mali hizo kwa njia ya magendo.

"Wanakwenda kufanya uchunguzi na wataleta kwangu walichokiona kuhusiana na tukio la kuungua kwa moto ghala la kuhifadhi bidhaa za magendo lililoko Bandari ya Tanga. Kimsingi, kamati hiyo inahusisha wataalamu kutoka Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), TAKUKURU, Jeshi la Polisi na Wakala wa Majengo nchini (TBA).

"Wengine ambao nimewajumuisha katika kamati hiyo ni mtaalamu kutoka Mamlaka ya Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wa uhandisi maalumu kwa ajili ya kuzuia milipuko. Tayari kamati hiyo imepewa hadidu za rejea na watakwenda kutafsiri kama tukio hilo ni hujuma ama ajali au uhalifu. Tunataka watuambie chanzo ni hitilafu ya umeme au ni hujuma."

Moja ya hadidu za rejea ni kupitia nyaraka zote za TRA za kuingiza na kupokea mzigo, kuhoji muda wa mzigo ulipokaa tokea mwaka jana na uliingia mwezi upi. Pia, kuhakiki mali zilizokuwapo kwa mujibu wa nyaraka na kufanya uchunguzi taarifa hizo.

"Kwa mfano mtumishi mmoja ambaye anaitwa Kisaka, yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Kuzuia Magendo ya Mkoa, moto ulivyotokea, alipigiwa simu ili aweze kutoa taarifa lakini mpaka asubuhi simu iliiita haijapokelewa na ndiyo huyo yupo kwenye hilo. Hao watu wachunguze kwa nini hakupokea simu usiku mzima," alisema Mgumba.

Kutokana na sakata hilo, Mkuu huyo wa Mkoa, aliagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuimarisha ulinzi na doria za kawaida kwenye mkoa mzima.

"Lakini imarisheni doria kwenye taasisi za fedha, benki, kwenye viwanda vinavyohusika na watu wengi kama TPA, GBP na Tanga Cement za mara kwa mara mchana na usiku huku wamiliki wa mahoteli na wawekezaji sekta binafsi na za umma, mahoteli kuimarisha ulinzi,"alisema.

Oktoba 2, mwaka huu, shehena ya magendo ya sukari na mafuta ya chakula iliyokuwa imeingizwa nchini kupitia Bandari Bubu ya Kasera iliyoko nje kidogo ya Jiji la Tanga, iliripotiwa kutoroshwa na watu wasiojulikana katika mazingira ya kutatanisha.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, bidhaa hizo zilitoroshwa muda mfupi baada ya kufika bandarini hapo, huku majahazi yaliyoubeba mzigo huo yakitelekezwa.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (wa pili kushoto), akitembelea kiwanda cha vinywaji vikali cha Kampuni ya bia ya Serengeti (SBL), katika ziara yake ya ukaguzi wa upanuzi wa kiwanda hicho, mjini Moshi juzi. Wengine ni wafanyakazi wa SBL. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPC yawapa majani wafugaji kuinusuru mifugo na ukame

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

TISHIO la ukame ambalo limeathiri kwa asilimia 90 nyanda za malisho ya mifugo katika Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, limeigusa Menejimenti ya Kiwanda cha Sukari cha TPC, baada ya kuamua kuwafuta machozi wafugaji wanaopakana na mashamba yake, kwa kuwapa majani yaliyosokotwa kisasa ili kuinusuru mifugo yao kufa kwa njaa.

Jana Ofisa Mtendaji Mkuu/Utawala wa TPC, Jaffary Ally, alisema wafugaji watakaonufaika na mpango huo wa kuinusuru mifugo yao na njaa ni wa Kata ya Kahe ambao wanayazunguka mashamba ya miwa.

"Tumeandaa mpango wa muda mfupi na mrefu wa namna ya kuinusuru mifugo ya wafugaji wa kata hiyo, ambapo katika Kijiji cha Mawala peke yake, wafugaji wamepoteza mifugo 570 baada ya kudhoofu na kufa kwa njaa. Kwetu sisi tunaona hili ni jambo kubwa kumsaidia jirani yako anayekuzunguka," alisema.

Kata ya Kahe inayokaliwa na idadi kubwa ya wakulima na jamii za kifugaji, ilipoteza mifugo hiyo kutokana na ukame mkali, uliotokea kati ya Julai hadi Septemba mwaka huu.

"Wafugaji wanaotoka ukanda wa tambarare hasa Kahe, waliomba kuingiza mifugo yao kwenye eneo la mashamba ya kiwanda chetu ambayo sasa hayatumiki, lakini tukaona siyo vyema kuruhusu hilo. Ni bora tukafanya jambo ambalo litasaidia pande zote mbili. Menejimenti ikaamua kununua mashine ya kuvuna nyasi katika eneo hilo na kuzifunga katika marobota na kisha kuzikabidhi kwa serikali ya kijiji," alieleza.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, Menejimenti ya TPC ilipokaa kujadili ombi hilo, iliona kwamba kama wakiruhusiwa kuingiza mifugo yao shambani, kuna uwezekano mkubwa wa kuharibu miundombinu ya umwagiliaji wa mashamba ya miwa ya kampuni.

Kabla ya wafugaji hao kuwasilisha ombi la kutaka kuingiza mifugo kwenye mashamba hayo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, aliwasiliana pia na menejimenti ya kiwanda hicho, kuwajulisha juu ya barua ya wafugaji hao wa Kata ya Kahe.

Kata ya Kahe peke yake iliyopo eneo la ukanda wa Lower Moshi, inakadiriwa kuwa na wastani wa mifugo 10,000 wakiwamo ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Januari mwaka huu, Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro, ilikiri kuwa janga la ukame lilisababisha vifo vya mifugo zaidi 1,200 katika mkoa huo.

Kati ya hiyo ng'ombe walikuwa 841, kondoo 406 na punda 10.

## Shekhe awapa angalizo wakazi K'njaro kuhusu vikundi uhalifu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHEKHE wa Mkoa wa Kilimanjaro, Shaaban Mlewa, amewasihi wakazi wa mkoa huo kuhakikisha hakuna kikundi chochote cha uhalifu kinachowahusu watoto kinazaliwa na kuwa tishio mitaani au kuathiri shughuli za kiuchumi.

Alitoa ushauri huo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa dini na serikali wakati wa uzinduzi wa Chuo cha Dini cha Izzudin Rau kilichoko Ushirika katika Manispaa ya Moshi.

"Hivi sasa kumezuka watoto wanaoitwa Panya Road kwa Dar es Salaam, kule Mkoa wa Tanga wanajiita Watoto wa Ibilisi, huku Arusha wanajiita Tatu Mzuka. Yaani kila mahali ni tatizo na ukikutana nao hao watoto wahalifu mwombe Mungu, maana hawakuachi ni lazima wakujeruhi na kukupora au wakuuwe ama wakutie ulemavu wa kudumu.

"Ndugu zangu wa Mkoa wa Kilimanjaro, tusikubali kufika huko. Sisi hapa kwetu makundi hayo bado hayajazaliwa. Wazazi na walezi wajengeni na kuwalea watoto wetu katika misingi ya dini ili waje kuwa wenye tabia njema kwenye jamii na siyo kuwaacha wajitafutie mahitaji kama chakula na mavazi, watajikuta wameingia katika makundi ya kihalifu," alisema.

Aidha, alizitaja sababu za watoto hao kukata tamaa na kuingia katika uhalifu ni kukosa malezi bora, ambayo yangewafanya watoto hao kuwa na ubinadamu na kujitambua.

"Tafiti mbalimbali za saikolojia ya makuzi ya mtoto zinamtaka mzazi awe kiongozi wa familia. Hii inasaidia mtoto katika kipindi cha ukuaji wake na maisha ya kila siku, matendo na misemo huunda taswira vichwani mwa watoto juu ya maisha, lugha na mahusiano.

Zaidi aliongeza: "Ndiyo maana tunaambiwa mabadiliko katika mfumo wa utandawazi na ongezeko la zana za dijiti, yameleta athari kubwa katika malezi ya watoto. Wazazi wanatumia muda mwingi katika mitandao ya kijamii na kusahau kutoa malezi shirikishi kwa watoto wao. Hali hii imeleta ongezeko kubwa la mmomonyoko wa maadili katika jamii."

Akitoa taarifa ya maendeleo ya chuo hicho, Salimu Muhidin, alisema walivutiwa kuanzisha na kufungua chuo hicho, baada ya kuona ongezeko la waumini katika Ushirika ambalo lina idadai kubwa ya wanafunzi wa vyuo vikuu, sekondari na taasisi za umma na wananchi wa kawaida.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 25, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

## Asasi ya kuokoa wasichana dhidi ya mila potofu yajikita Pwani, shule 22 zaneemeka



Ukurasa 16



Ukurasa 15

## Haya yanawachochea watoto kuhama familia, kuishi mitaani

SAYANSI

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

### KIRUSI HATARI CHA MAABARA

# Chuo Kikuu kilivyozua taharuki chazalisha toleo hatari la UVIKO-19


- Kinaua asilimia 80, ni mahiri kukwepa na kuharibu kinga za mwili kuliko vingine

MWEZI Oktoba, umekuwa wa kishindo kipya cha hofu ya kuibuka upya UVIKO-19 kufuatia taarifa kuwa Chuo Kikuu cha Boston cha Marekani kimetengeneza kirusi kingine cha COVID-19 hatari zaidi, kuliko kile cha Omicron.

Aidha, taarifa zinasema kuwa aina hiyo mpya ya UVIKO au COVID-19 ni mseto unaochanganywa na wanasayansi katika Chuo Kikuu cha Boston na kwamba kirusi kina nguvu nyingi na kinaua kwa asilimia 80 na kina mizungu au uganga zaidi wa kuzikwepa kinga za mwili.

Maelezo hayo yakiongeza kuwa miongoni mwa majaribio yake yalifanywa kwenye panya na kubaini kuwa ni hatari na tofauti na aina ya zamani ya Omicron kwa vile kwenye omicron, panya hao walipata athari kidogo tu walipoambukizwa virusi.

Wanasayansi na wataalamu wa matibabu wakiwa na nadharia tofauti wengi wakipinga kuwa utafiti kama huo kwenye popo ulifanywa katika maabara za jimbo la Wuhan nchini China ukawa chimbuko la corona duniani na kuanzisha janga la virusi waliokatishia uhai wa mamilioni bila sababu hasa watumishi wa afya.



Wanasayansi wa Chuo Kikuu cha Boston wakiwa maabara kuzalisha kirusi kipya. **PICHA: MTANDAO**

Hatua ya Boston, ikikosolewa na wataalamu wanaosema: "Utafiti juu ya vimelea vya magonjwa vinavyoweza kutokea unahitaji kuongezwa na kulindwa ili kuepusha matatizo hatari yanayoweza kuibuka mbeleni." Dk. Richard Ebright wa Chuo Kikuu cha Rutgers na mtaalamu mkuu wa kemia anasema.

Anaongeza kuwa anaamini kwamba utafiti ukifanywa, husaidia kuelewa kinachoharibika na hapo ndipo wanaweza kuepuka janga linalofuata la maabara kuzalisha maradhi hatari.

Huko Boston, wanasayansi wanaotafiti aina mpya ya COVID-19 walitoa protini kutoka kwa aina ya Omicron. Protini hiyo ndiyo hung'ang'ania seli za binadamu na kisha kuzishambulia, watafiti waligundua kuwa panya walikipokea kirusi kwa njia tofauti na kuliko ile mpya, ambayo ilikuwa nyepesi kwa wanyama mamalia akiwamo binadamu.

Lakini aina mpya, Omicron S, ilishambulia panya wote na kuua asilimia 80 yao, waliandika katika ripoti zao watafiti hao wa Boston.

**JUHUDI ZA KUKANUSHA**

Baada ya taarifa kusambaa kuwa wameandaa kirusi hatari kwenye maabara zao, Chuo Kikuu cha Boston kikaingia kiwewe na kuanza kufafanua utafiti wake wa COVID-19,

wanajitetea kuwa aina mpya kitaalamu ikiitwa 'new variant' haikuwa mbaya sana.

"Gazeti la udaku la Daily Mail la Uingereza lilizua utata na taharuki kwa kusema Chuo Kikuu cha Boston kimeunda kirusi kingine hatari cha COVID chenye "kiwango cha kusababisha vifo kwa asilimia 80," gazeti la Boston Globe linabainisha.

Likazidi kukanusha kuwa chuo kikuu kimejibu kwa ukali na kikabaini kuwa majaribio yake yalifanya virusi kuwa hatari zaidi.

Boston University -BU inaripoti kwamba iliunda aina hatari zaidi ya COVID 'ya uwongo na isiyo sahihi' na kuongeza kuwa jarida la udaku la Uingereza lilipotosha matokeo ya utafiti wa virusi uliofanywa katika maabara ya BU ya South End.

**INAENDELEA UK. 18**

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Kisomo watu wazima chaingia kwa gia kubwa Dar, Pwani

• Asiyejua KKK aeleza alivyokosa uongozi

ELIMU ya watu wazima imekuwa na mchango mkubwa wa kumwezesha mtu kufuta ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) na kumpa ujuzi wa kazi mbalimbali licha ya kujiona kuwa ana umri mkubwa.

Kimsingi, elimu hiyo iliyokuwa ikiitwa ngumbaru inakuondoa pengo la elimu miongoni mwa Watanzania na ina mchango mkubwa kwa wale wanaojitokeza kuipata, kwani inawawezesha kutoka kwenye hali duni ya maisha na kujifunza jinsi ya kuinua hali ya maisha na kuongeza uwezo wa kuzalisha mali.

Kwa kutambua umuhimu huo wa elimu baadhi ya wafugaji wenye asili ya Kimasai ambao hawakubahatika kupata elimu kupitia mfumo rasmi, wameamua kujiunga na elimu ya watu wazima ili kufuta ujinga.

Wafugaji hao 245 wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani sasa wanahudhuria madarasa ya elimu ya watu wazima kila siku katika vituo vinavyosimamiwa na Kanisa la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani.

Mwalimu wa wanafunzi hao, Christina Moleto anasema hayo katika kilele cha maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima, hivi karibuni katika viwanja vya Chuo cha Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE).

"Dar es Salaam kuna vituo vitatu vikiwa na wanafunzi 149, Pwani pia vipo vitatu vikiwa na wanaafunzi 96 na tupo walimu 12, kila eneo lina walimu sita ambao tunawafundisha," anasema Christina, akieleza kuwa mwamko ni mzuri na kwamba tangu madarasa hayo yaanze miezi sita iliyopita, tayari wanazijua KKK, hali inayoonyesha kuwa wana nia ya kweli ya kutaka kufuta ujinga.

Katika maelezo yake anafafanua kuwa vituo vya Dar es Salaam vipo Mwenge, Msasani na Tegeta, wakati vikundi vya Pwani vipo Nabanya, Mindutulieni Shuleni na Nduli katika Kata ya Lugoba, Halmashauri ya Chalinze.

Anaongeza kuwa kwa Dar es Salaam wanasoma kuanzia Jumatatu hadi Jumatano muda wa saa nne asubuhi hadi saa sita mchana na Pwani wanasoma kuanzia Jumanne hadi Alhamisi muda wa saa nane hadi kumi jioni.

"Lakini pamoja na maendeleo hayo, ninadhani ni vyema serikali ikatusaidia wataalamu wa kuwafundisha ujuzi wa fani mbalimbali ili waweze hata kuboresha biashara zao na mambo mengine ukiwamo ujasiriamali,"anatoa ombi akisema elimu si KKK pekee, kuna mambo mengi zikiwamo mbinu za utafutaji na kubuni miradi.




Naibu Waziri wa Elimu (wa nne kutoka kulia waliokaa) Omary Kipanga, akiwa na viongozi wengine na wadau wa elimu ya watu wazima kutoka mikoa mbalimbali. **PICHA ZOTE: SABATO**

### ALIVYOKOSA UONGOZI

Mmoja wa wanafunzi hao Moses Charles, anatoa ushuhuda mbele ya hadhara kuwa alikosa uongozi katika kitongoji cha nyumbani kwao Kibirashi Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, kutokana na kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu wananchi wakimshangaa atafanyaje kazi zama hizi za elimu kuwa ufunguo wa maisha.

"Wananchi walikuwa wanataka niwe kiongozi wao, nikakubali, zililetwa fomu za kuwania uongozi nikatakiwa kujaza, lakini nikashindwa kwa sababu nilikuwa sijui kusoma, hivyo nikakosa uongozi," anasema Charles.

Hata hivyo, anabainisha kuwa baada ya kuhudhuria madarasa ya elimu ya watu wazima, sasa anajua kusoma, kuandika na kuhesabu, huku akiweka wazi kuwa akirudi kwao atakwenda kuhamasisha jamii yake kusoma na kufuta ujinga kwa vile hakuna linaloweza kufanyika bila kujua KKK.

"Nimeshatambua kuwa elimu ndio kila kitu katika maisha, nami ninaungana na mwalimu wetu kwamba sasa serikali itufundishe jinsi ya kuwa na ujuzi wa fani mbalimbali, ili kufanya kazi zetu kwa ufanisi, lakini pia kuwa na ujuzi wa masuala mbalimbali ya kimaisha ambayo yanamfanya mtu kumudu na kuboresha Maisha," anasema.

### HALMASHAURI ZAAGIZWA

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, anawaagiza wakurugenzi wa halmashauri kutenga bajeti, kwa ajili ya shughuli za elimu ya watu wazima, kuwezesha maofisa wanaoisimamia kuwafikia walengwa.

"Viongozi wote katika maeneo yenu hakikisheni mnaendelea kuipa uhai elimu ya watu wazima kwa kuyafanya maadhimisho kuwa endelevu yakihusisha makundi mengi zaidi katika kila mkoa nchini," anasema Kipanga.

Anataka ushirikiano kati ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na viongozi wengine wa serikali na kutaka uendelee huku wakihamasisha, kuanzisha na kusimamia madarasa ya MEMKWA na kuhakikisha yanakuwa na vitendea kazi vinavyokidhi mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji.

"Ni muhimu kila Mtanzania kuthamini mchango wa elimu ya Watu wa Wazima, kwani katika miaka ya 70, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliitumia kama chombo cha kulikomboa kundi kubwa la Watanzania waliokuwa wanakabiliwa na changamoto ya ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu," anasema.

Anasema kupitia elimu hiyo watu waliweza kukabiliana na maradhi na umaskini na kwamba katika kipindi hicho, programu kama Kisomo Chenye Manufaa, ilitumika kuwafundisha watu wazima waliokuwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK).

"Kulikuwa pia na programu ya kujiendeleza kwa wale waliokuwa wakijua kusoma, kuandika na kuhesabu, lakini wakakosa stadi mbalimbali, hivyo hatua hiyo iliwaongezea maarifa na iliendana na matamko mbalimbali likiwamo la elimu haina mwisho," anasema.

### HALI HALISI

Inaelezwa kuwa, idadi ya Watanzania wasiojua kusoma na kuandika kwa sasa ni asilimia 22, na kwamba ili kukabilia na tatizo hilo, wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma, uliozinduliwa mwaka 2020, unaolenga kuboresha programu za kisomo kwa njia mbadala.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, anataja mojawapo ya programu hizo kuwa ni elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi.

Kamishna huyo anafafanua kuwa wizara inatekeleza programu hiyo kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, na kwamba katika mwaka wa masomo wa 2022, jumla ya wanafunzi 17,529 wamedahiliwa.

"Elimu hii inatolewa katika vituo vya shule huria 743, kati ya hivyo, 151 vinaendeshwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na vilivyobaki viko chini ya wadau wa elimu," anasema Dk. Mtahabwa.

Anafafanua kuwa miradi hiyo inatekelezwa katika mikoa nane ya Kigoma, Dodoma, Iringa, Tabora, Mbeya, Njombe, Songwe na Dar es Salaam na kwamba katika awamu ya pili, itatekelezwa katika mikoa sita mengine ya Simiyu, Shinyanga, Manyara, Pwani, Singida na Pwani.

"Mipango na mfumo wa elimu ya watu wazima kwa sasa imebadilika, inajikita zaidi katika kutatua changamoto za wakati huu kama vile kukosa fursa ya elimu ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Fursa za kupata ajira, elimu ya ujasiriamali, utunzaji wa mazingira, haki za kijinsia watoto na wanawake," anasema.



Baadhi ya wafugaji ambao sasa ni wanafunzi wa elimu ya watu wazima (mbele), wakifuatilia maadhimisho hayo.

ELIMU

NA VITUS AUDAX, MWANZA

# Haya yanawachochea watoto kuhama familia, kuishi mitaani

- Ni matokeo ya chuki, kutesa, njaa, vipigo vya kikatili, kujeruhi



Watoto wanalazimika kuishi majalalani kutokana na mateso na manyanyaso nyumbani kwa walezi au wazazi. **PICHA: MTANDAO**

MIJI mikubwa na majiji yanashuhudia wimbi kubwa la watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu na kwa mujibu wa takwimu za sensa ya mwaka 2012, watoto wawili kati ya 838 huishi na kulala mitaani.

Aidha, zinaeleza kuwa watoto 5,600 wamekimbilia mtaani jijini Dar-Es- Salaam na takribani 1,568 sawa na asilimia 28 ya idadi hiyo wamezagaa mkoani humo ikifuatiwa na Dodoma asilimia nane na Mwanza ikiwa na asilimia saba ya watoto hao walioko mitaani.

Kadhalika takwimu zinaeleza kuwa asilimia 57 ya watoto hao ni kutoka mikoa ya Tanga, Arusha, Iringa, Morogoro na Pwani. Na katika hali ya kawaida ongezeko la watoto hawa linaweza kuwa juu zaidi baada ya matokeo ya sensa ya mwaka huu.

Ongezeko la watoto hawa linaweza kutatuliwa endapo utajulikana mzizi mkuu wa kuuona mtaa sehemu salama kwa maisha yao zaidi ya kubaki katika familia zao na kuendelea na elimu hususani kwa kipindi hiki serikali ikigharamia elimu kuanzia msingi mpaka kidato cha sita.

Ikumbukwe kuwa si kila mtoto aonekanaye mtaani huipenda hali hiyo, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika katika jiji la Mwanza, watoto saba kati ya 10 wameingia mtaani kutokana na migogoro ya familia.

Mbali na migogoro hiyo ukali wa wazazi na walezi pia unachangia ongezeko hilo, huku watoto kati ya 10 huagizwa na wazazi wao kwenda mtaani kuomba fedha kwa ajili ya kujipatia mkate wa kila siku.

Hata hivyo, mtoto mmoja kati ya hao 10 hukimbia nyumbani bila sababu za msingi kutokana na shinikizo la watoto waliopo mtaani, utafiti unabainishwa na ushuhuda wa miaka 12 jina tunalo, anayesema kuwa kwamba Agosti, 2019, alipanda lori kusafirisha mkaa kutoka Karagwe mkoani Kagera na kuingia Mwanza kutokana na wazazi wake kuhitilafiana hatua iliyofuatiwa na baba yake kuoa mke mwingine ambaye hakumpenda.

"Baada ya kuoa mke mwingine nilianza kupigwa na kufanyishwa kazi ngumu, napigwa mno na kufukuzwa ili nilale nje, pia mara nyingi nilikuwa nikizuiliwa kula chakula au anachukua sahani yangu na kukimwaga nikilala njaa. Nikachoka mateso nikaamua kutafuta ninapoweza kuishi bila usumbufu."

Mwingine mwenye miaka 11 wa kiume, kutoka Ukerewe alikimbia yumbani mwaka 2017 akiwa na miaka sita. Anautaja ulevi na usumbufu wa mjomba wake aliyekuwa mlezi baada ya wazazi wake kufariki kuwa chanzo cha kuacha maisha ya familia yake.

"Mjomba alikuwa mlevi kila akirudi nyumbani ni kutukana na kutuzuia kula chakula wakati mwingine alikuwa akimwaga chakula chote kilichoandaliwa. Hapo sikuwa na jambo la kunifanya niendelee kunyanyasika nyumbani kwake ikanibidi nitafute pa kukimbilia ndipo nikaja hapa Mwanza."

Kadhalika kuna taarifa ya mtoto wa kiume mwenye miaka 13 miongoni mwa watoto wanaopatikana Barabara ya Nyerere, jijini Mwanza ikiwa alitokea mkoani Mara, aliingia mtaani baada ya wazazi kugombana na kuachana akibaki na mama yake aliyeanza kufanya mambo ambayo hayakumpendeza tena hakuwa na muda wa kumhudumia. Aidha, yupo binti wa miaka saba anayepatikana maeneo ya jengo la NSSF, Mwanza anayedai anatumwa na mama yake mzazi ili kuomba fedha. Kwa mujibu wa maelezo yake mzazi anabaki nyumbani wakati mwingine humleta na kumuacha eneo hilo na kumrudia jioni.

"Sisomi na kila asubuhi huamka na kuambatana na mama mjini wakati mwingine huniacha nyumbani akinielekeza eneo la kukaa ili nikaombe hela na kila nikipata ni lazima nimpelekee. Nisipopata mara nyingi tunashinda au kulala njaa kitu kinachopelekea kuomba kila mtu anayepita eneo nililoko."Anasema.

Nje na kukimbia matatizo ya nyumbani kwao watoto hao hali ya kimaisha kwao bado ni kizungumkuti wawapo mtaani, ikiwa usalama wao wa maisha ni mdogo kutokana na vijana wa mitaani wakubwa zaidi yao kuwapiga, kuwanyang'anya wakitafutacho vilevile kuwatumia watoto hao katika shughuli za wizi kwa kuwapitisha madirishani.

Aghalabu, watoto hao wamekubaliana ya hali hapo mtaani kimazingira, ikiwa ni pamoja na kulala pembezoni mwa barabara, kuomba, mitaani, kuvaa mavazi duni pamoja na huduma nyingine za kijamii. Huku ombi lao likiwa nikusaidiwa kupelekwa shule ikiwa ni salama zaidi nje ya familia zao ili waweze kusoma na kuishi ndoto zao kama watoto wengine.

**ATHARI ZA ONGEZEKO**

Yusufu Mtobela ni Mkurugezi wa Upendo Daima, kituo cha kulea watoto kutoka mitaani na kuwarudisha nyumbani kwao wanaporidhia na kutoa elimu kwa jamii hiyo. Anaeleza ushirikishwaji wa jamii pamoja na elimu kwa wanafamilia kuwa suluhisho la tatizo hilo.

Anasema madhara ya kuongezeka kwa watoto mitaani katika jamii ni pamoja na ongezeko la magenge ya vijana wafanya uhalifu mtaani mfano 'panyarodi', wizi wa bidhaa madukani, vitendo vya ulawiti pamoja na ubakaji.

"Hili ni tatizo kubwa katika jamii ya sasa kubwa zaidi tunatakiwa kujua kuwa hakuna mtaa unaozaa mtoto bali kila mtoto ana wazazi na haki yake kubwa ni kukaa na familia yake. Jamii inatakiwa kupewa elimu ya familia, watoto wanaoachwa na wazazi wanaofariki nao waweze kutunzwa na ndugu wa familia hizo."Anasema Mtobela. "Tunajitahidi kuwatafuta watoto kutoka mitaani wanaoridhia kurudi nyumbani tunatoa semina kwa familia zao juu ya kuwa na upendo kwao. Vilevile wale wasioridhia kurudi kwao kutokana na matatizo yaliyowatoa, tunawatunza na kuwapeleka shule ambapo wanasoma na kuendelea vizuri kama ilivyo kwa watoto wengine wenye ndoto za maisha." Anaongeza.

Wajumbe wa Mkakati wa Kupambana na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) mkoani Mwanza, Aprili, mwaka huu walianza mkakati wa kuwaondoa watoto wa mitaani na kuwarejesha nyumbani kwao, ikiwa ni lengo la kutokomeza utoro katika shule za msingi na sekondari pamoja na kutembelea familia mbalimbali na kuelimisha, wazazi na walezi ili kudhibiti wimbi hilo la watoto mitaani.

Anahimiza jamii kushirikiana na serikali na wadau kutekeleza mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kukabiliana na changamoto za ulinzi wa kundi hilo kwa kushiriki mafunzo yanayoandaliwa, kutoa elimu na hamasa kwa jamii ili ibadilike na ijali watoto.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA

# Asasi ya kuokoa wasichana dhidi ya mila potofu yajikita Pwani, shule 22 zaneemeka

MILA zilizopitwa na wakati kama kuoza watoto, kukeketa na kuthamini watoto wa kiume kuliko wa kike zimekuwa zikiendelea zaidi vijijini lakini zama hizi si jambo geni kujua kuwa zimeingia na kuenea mijini.

Ni kwa sababu waliopo vijijini wanapohamia mijini wanakwenda nazo iwe ni Dar es Salaam, Mwanza au Mbeya jambo linalokwamisha kampeni za kuzitokomeza kusuasua.

Baadhi ya mashirika yanalazimika kusimama na mtoto wa kike kumpambania ili kupata haki zake za msingi kama ilivyo kwa wavulana, yakijitahidi wasome na kujishughulisha na vitu vingine vya kumuinua kiuchumi na kuondokana na kuwa mtu wa kulea familia.

Ni mila za kizamani kwa kuwa zimepitwa na wakati na nyingi ni za kumkandamiza binti endapo makabila yanayoziendekeza yakibadilika kauli itakuwa moja ya kuinua mtoto wa kike na kupata haki zake za msingi.

Ndiyo maana baadhi ya wadau wanasema wakati umefika mashirika yanayopambania haki ya mtoto wa kike kwenda vijijini na kufanya programu za kuwashirikisha watoto wa kike kuwapa kipaumbele kwa kila sehemu ili jamii iamini kwamba wanaweza kufanya yale yanayofanywa na watoto wa kiume na kubadili mitazamo yao hasi.

Halmashauri ya Chalinze ni kati ya tisa za mkoa wa Pwani ambazo ni miongoni mwa shule zinazonufaika na miradi ya Shirika la Room to Read ikitoa elimu na stadi za maisha zinazolenga kumsaidia msichana dhidi ya mila potofu.

Halmashauri hiyo ina shule 23 kati ya 22 zinatekeleza miradi ya Room to Read ambayo ni elimu ya fedha pamoja na nguvu ya msichana (stadi za maisha) miradi yote miwili inatekelezeka kwa wanafunzi wa kike 2,423 wa kidato cha kwanza na cha pili.

Kwa upande wa programu ya elimu ya fedha kuna shule 10 ambazo Room to Read wanatoa msaada moja kwa moja kwa wanafunzi 1,408 zikiwamo Changalikwa, Mandera, Kikaro, Msata, Kiwangwa, Vigwaza, Pera, Chahua, Ubena pamoja na Mdaula.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Chalinze, Salama Ndyetabura, anasema utekelezaji wa mradi wa elimu kwa msichana na usawa wa kijinsia pamoja na elimu ya fedha ulianza mwaka 2014 hadi 2018 kwa awamu ya kwanza katika shule mbili za Lugoba na Chalinze.

**Anasema Room to Read waliwezesha na kutoa**

Mafunzo kwa mabinti wa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Anaongeza kuwa mwaka 2021 halmashauri iliona kuna umuhimu wa kuendeleza na kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu hiyo katika shule zote kutokana na mwitikio chanya wa wanafunzi wa kike na mafanikio yaliyojitokeza kutokana na miradi ya Room to Read, ikiwamo mabadiliko chanya ya makuzi na kimazingira kwa wanafunzi wa kike.

"Utekelezaji wa Miradi ya Room to Read kwa awamu ya pili katika Halmashauri ya Chalinze ulianza Juni, 2021 baada ya kuomba asasi hiyo kuendelea tena kuwezesha mafunzo kwa shule zote 22 za sekondari," anasema Salama.

Aidha, anafahamisha kuwa katika awamu hiyo ya pili ndipo walipoanza kutekeleza mradi wa Nuru ya Msichana na Februari mwaka huu, wanaendelea na mradi wa elimu ya fedha kwa shule zote 22 kati ya hizo shule 10 ziko chini ya usaidizi wa moja kwa moja wa taasisi.

Kupitia mradi huo wanafunzi wa kike wameonyesha mabadiliko kiufahamu lakini wameanza kupendwa hata na vidato vingine pamoja na baadhi ya wanafunzi wa kiume na wamekuwa wakishiriki katika mafunzo ipasavyo.



Wasichana wanalazimika kuishi na mila kandamizi bila kujali ni mijini au vijijini kutokana na jamii kuendelea kuzidumisha. **PICHA:MTANDAO**

> "Anazitaja sekondari za Mboga, Ubena, Pera, Msata na Mandera kuwa ni baadhi ya zile ambazo wanafunzi wametengeneza bidhaa hizo na kuziuza kwa walimu wao na jamii inayowazunguka."

Inaelezwa kuwa hadi sasa wanafunzi wa kike 3,831 wananufaika na miradi ya Room to Read na kumekuwa na mabadiliko ya tabia kwa kupaza sauti kuhusu vitendo vyote vinavyokiuka haki na utu wao.

Ofisa ya elimu inabainisha kuwa kutokana na miradi hiyo wanafunzi wamekuwa wakitoa taarifa na kuomba ushauri kwa walimu kuhusu vitendo vya ukandamizaji mila kwenye jamii zao ikiwamo za kuchezwa ngoma wakati wakiwa masomoni.

"Hilo pia limebadilisha baadhi ya wazazi na walezi ambao wamepata uelewa na kukubali kusubiri watoto wao wamalize masomo ndipo waendeleze utamaduni wao, hapa kumekuwa na msemo unaotumika Ubena Sekondari 'niache nisome, kuchezwa baadaye,' hali ambayo tunaweza kuilezea katika matokeo chanya kwenye halmashauri yetu."

" Wanaeleza pia mazingira na hali halisi ya maisha yao nyumbani na kuomba msaada kwa walimu, hapa tumeweza kubaini watoto wanaotoka katika mazingira magumu na ambao ni waathirikia wa VVU na UKIMWI kuweza kuchukua hatua za kuwapa matumaini na kuwa karibu nao ili waweze kutimiza ndoto zao," anaeleza Salama.

Halikadhalika, upande wa mradi wa elimu ya fedha anasema wanafunzi wa kike wamepata maarifa na ujuzi wa ujasiriamali na kuanza kushiriki katika kutengeneza bidhaa mbalimbali wakati wa muda wa ziada na hususan kipindi cha likizo.

"Kwa kweli mabadiliko yapo ni jambo la kujivunia wanafunzi walionufaika na mradi sasa wanatengeneza sabuni za maji, keki, bidhaa za asili zinazotengenezwa kwa mikono kama mikeka, vyungu pamoja na miiko ya kwa ajili ya ugali na wali na matumizi mengine ya jikoni," anasema.

Anazitaja sekondari za Mboga, Ubena, Pera, Msata na Mandera kuwa ni baadhi ya zile ambazo wanafunzi wametengeneza bidhaa hizo na kuziuza kwa walimu wao na jamii inayowazunguka."

Room to Read imeongeza fursa kwa mabinti na kuwawezesha kumudu masomo hasa wale ambao ni wakuu wa kaya, hivyo ujasiriamali ndiyo msingi wa kutimiza ndoto zao ikiwamo elimu," anaeleza ofisa elimu huyo.

Akizungumzia upande wa walimu anasema kupitia mafunzo ya mradi wa elimu ya fedha wameanzisha umoja wa ujasiriamali ujulikanao kama 'Three Mummy' unaojihusisha na kutengeneza mikoba na pochi na baadhi ya walimu wameboresha biashara za awali zikiwamo za kutengeneza keki.

Anatumia nafasi hiyo kuomba shirika hilo kuangalia namna ya kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu hiyo kuanzia shule za msingi hasa katika madarasa ya sita na saba, pamoja na kuwafikia vijana wa kiume kwani ni kundi ambalo pia lipo hatarini.

Mkurugenzi wa Room To Read, Juvenalius Kuruletera, anasema tangu walipoanza kutekeleza miradi ya elimu hapa nchini ukiwemo mkoa wa Pwani wamewafikia watoto 6,000.

Anasema kupitia miradi hiyo matokeo chanya yameonekana kwa upande wa ongezeko la ufaulu kwa watoto wa kike na kupungua utoro shuleni.

Mmoja wa wanafunzi ambao wamenufaika na miradi ya Room to Read kutoka Sekondari ya Bundikani, Shadya Mohamed, anasema kwasasa wameondokana na hofu liyokuwa inawasumbua kwamba yanayofanywa na wavulana, wasichana hawawezi.

Shadya anasema hofu hiyo ilikuwa imejengeka awali kwamba wasichana hawawezi kusoma masomo ya sayansi jambo ambalo kwasasa limeondoka na wote wanachuana madarasani.

ELIMU

NA JULIETH MKIRERI

# Ndoa za utotoni zinavyowageuza mabinti wajakazi wa mama wakwe

•Mwenye miaka 13 asimulia alivyochomoka kukataa utumwa



Binti mbali na kuozwa katika umri mdogo anatumikishwa kwa mama mkwe ili aamue hatima yake. Anafanyishwa kazi za nyumbani na za shambani. **PICHA: MTANDAO**

"ALIPOELEZWA suala la kuolewa, akatoroka nyumbani kuanzia saa 9:00 mchana alisakwa na alipopatikana saa 12 jioni, hapo hapo akakabidhiwa kwa mume wake waondoke kwenda kuanza maisha mapya," anaeleza Maria Leuda.

Maria ni kati ya wakazi wa Kitongoji cha Switi Kona, kilichoko Kijiji cha Vigwaza Halmashauri ya Chalinze mkoa wa Pwani, ambao wanasimulia mkasa wa ndoa ya binti wa miaka 13 aliyeolewa na baadaye kurejea nyumbani baada ya kubwaga manyanga kutokana na kunyanyaswa na mama mkwe.

Anaeleza kuwa binti huyo ambaye jina linahifadhiwa anao ndugu watatu wote wakilelewa na mama yao ambaye ameachwa na mume wake miaka ya hivi karibuni.

Historia ya mama huyo inayotolewa na Maria ambaye ni jirani inadaiwa kuwa ni kati ya watu ambao hawajahamasika kielimu, hivyo watoto wake wote hawajui kusoma wala kuandika.

Inaelezwa kuwa hata pale baadhi ya ndugu walipojitolea kuwanunulia vifaa vya shule watoto waanze masomo mama huyo aliviuza na kuendelea kuishi kwenye dimbwi la kutokujua kusoma, kuhesabu na kuandika.

Kuhusiana na binti yake huyo inadaiwa kuwa mara nyingi amekuwa akimwomba mama yake kumpeleka shule lakini hakuafiki wala kumuunga mkono na alichokuwa anasubiri ni mtoto akue ili amwozeshe.

Miaka 13 ilipotimia alilazimishwa kuolewa katika kijiji jirani cha Kidogozero kwa mwanaume ambaye tayari alikuwa na familia ya mke mwenye watoto wanne.

Maria anaeleza kuwa kila binti huyu alipotamkiwa suala la kuolewa hakuliafiki na wimbo wake mdomoni ilikuwa ni hataki kuolewa na anachohitaji ni kwenda kusoma.

Hata hivyo Maria anasema binti huyo pamoja na kutoroka na kurejea nyumbani mama yake alishikilia msimamo wake na kumwozesha kwa mahari ya ng'ombe wanne.

Inaelezwa kuwa mwezi mmoja baadaye zilikuja taarifa za binti huyo kutoweka nyumbani kwa mume wake alikokuwa akiishi na mama mkwe ikidaiwa kuwa alikimbia kusikojulikana.

Ndugu upande wa mume na kwa binti walimtafuta msichana huyo kwa mawasiliano ya simu usiku kucha bila mafanikio hadi kesho yake alipopatikana saa 11 na kuwaeleza kuwa hayuko tayari tena kuendelea kuishi kwenye ndoa, kwa mujibu wa Maria.

Akizungumza na Nipashe anaeleza kuwa haikuwa kazi rahisi kuishi ukweni kwa muda huo wa mwezi mmoja akisema kuwa baada ya kuolewa mumewe alimuacha kwa mama mkwe na kuondoka kuendelea na shughuli zake zikifanyika maeneo ya mbali na kijiji cha Kidogozero.

"Kwa kipindi cha mwezi mmoja nilikuwa nikimfanyia kazi mama mkwe kuosha vyombo, kumpikia na wakati mwingine kwenda kutafuta kuni, lakini nikirejea alikuwa ananifokea na kunituhumu kuwa nilikwenda kwa wanaume na sikuwa natafuta kuni."

Anaendelea kudai kuwa hata alipoachwa nyumbani peke yake mama mkwe akirejea alikuwa akimtuhumu kuwa si mwaminifu kwa maelezo kuwa alikuwa akileta wanaume nyumbani hapo.

Binti huyo anaendelea kueleza kuwa kutokana na manyanyaso aliyoyapata alilazimika kutoroka nyumbani mchana na kutembea kwa saa saba ili kurejea kwa mama yake anayeishi Switi Kona Vigwaza.

"Nilitembea kuanzia saa saba mchana, usiku ulinikuta nikiwa porini nikalala na ilipofika alfajiri niliendelea na safari ya kurudi nyumbani nilifika saa 11 jioni na kukuta kila mtu akiwa anataka kujua nilikuwa wapi," anaeleza binti huyo.

Hata hivyo baada ya kurejea na kuwakuta ndugu wa mume wakimsubiri alitakiwa kurudi kwake jambo analolipinga akikataa katakata akitaka kubaki nyumbani na sio ndoa ya kulazimishwa.

Anasema baada ya kugoma kurudi kwa mume wake wakwe zake walichukua ng'ombe zao walizotoa mahari na kurejea nazo kwao Kidogozero.

Kwa mujibu wa binti huyo mama yake pamoja na kutokubaliana na alichotaka mtoto wake awali lakini alimruhusu kukaa nyumbani kwake.

Inaelezwa kuwa kwa sasa mama huyo amekubali mtoto wake akipata msaada aende kusoma na kwamba hawezi kulazimisha tena kuolewa kutokana na manyanyaso anayodai kupitia binti huyo.

Wakielezea kuhusiana na binti huyo majirani na baadhi ya ndugu na familia yake yenye asili ya Kimaasai wanasema kuozeshwa binti huyo ni suala la kimila na kwamba wapo wanaoozwa wakiwa na miaka 12 na baada ya ndoa wanapelekwa kuishi na wakwe zao kuwasaidia kazi mbalimbali hadi pale watakapoonekana wanamudu kuishi na waume.

"Kuolewa katika umri mdogo kunafanyika ilimradi wazazi na walezi wakikubali hata kama ni mdogo unakwenda kuishi na mama mkwe unamfanyia kazi mbalimbali hadi pale atakapoamua kukuruhusu ukaishi kwa mume wako," anasema msichana huyo.

Wana jamii ya Switi Kona wanaeleza kuwa kwa sasa hali inaanza kubadilika kwa baadhi ya wazazi na walezi kwani wamekuwa wakisisitiza watoto kusoma ili kujiendeleza kielimu na baadhi yao wameanza kuipa kisogo mila ya kuozesha watoto wadogo.

**ANGALIZO OFISA MAENDELEO**

Rukia Hoja ni Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Vigwaza anayesema jamii ya Wamaasai wanaoishi katika kata hiyo haijamka kikamilifu kuacha ndoa za utotoni na hata ukatili wa wanawake unaofanywa na waume bado wanaukumbatia badala ya kuwaripoti.

Anasema kutokana na hali hiyo wanalazimika kuanza mikakati ya kumlinda binti kwa kutoa elimu kuhusiana na athari za ndoa za utotoni kwa kuwaelimisha watoto wa kike, walezi na wazazi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Vigwaza, Ally Hamis, anataja baadhi ya mbinu zinazotumiwa kuwa ni pamoja na mikutano ya wananchi kusisitiza suala la elimu na kupinga mila kandamizi kwenye jamii zao.

"Tukiwapa elimu hata watoto wa kike wanaokumbana na adha ya kuolewa udogoni wataelewa ni wapi wafikishe matatizo yao na sisi tunaendelea kusisitiza elimu kila tunapofanya mikutano," anaeleza Ally.

Diwani wa Vigwaza, Mussa Gama, anaomba serikali kuwaunga mkono kutoa elimu kwa jamii hiyo ya kupinga vitendo vya ukandamizaji watoto wa kike.

Anasema kesi za mabinti kuozeshwa wakiwa na umri mdogo hazifiki serikalini kwa muda muafaka, ambapo pia zinahitajika jitihada za kukutana na viongozi wakuu wa Kimasai kuwaelimisha haki za mtoto wa kike na athari za kuozwa udogoni.

Viongozi hao pia wanakumbusha umuhimu Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ikafanyiwa marekebisho ili ipatikane kinga kwa mabinti hao wanapofikisha kesi kwenye vyombo vya sheria.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto Halmashauri ya Chalinze, Beata Mchopa, anasema madhara ya mimba katika umri mdogo ni pamoja na kuathirika kisaikolojia, kuambukizwa maradhi kama VVU, homa ya ini, walengwa kutosoma na kuwa na idadi kumbwa ya mbumbumbu kwenye familia, uhusiano mbaya ndani ya ndoa na hata kuvunjika.

Kwa mujibu wa utafiti wa demografia ya afya nchini (TDHS) wa mwaka 2010 mikoa yenye viwango vikubwa vya ndoa za utotoni ni Shinyanga yenye asilimia 59, Tabora 58 wakati Mara ni ya tatu kwa asilimia 55 na Dodoma inafikia kiwango cha 51.

## KIRUSI HATARI CHA MAABARA

# Chuo Kikuu kilivyozua taharuki chazalisha toleo hatari la UVIKO-19

INATOKA UK. 13

Chuo Kikuu cha Boston wiki hii kilikanusha ripoti za habari kwamba kilitengeneza kirusi na kupinga kile kilichokiita jarida la udaku la Uingereza lilichoelezea bila hofu kuwa ni aina ya COVID “na kiwango cha maangamizi ni asilimia 80.

Kwa kuona kuwa taarifa hiyo imeustua ulimwengu wa utafiti wa sayansi za tiba, Boston inapinga na kueleza kuwa habari hiyo imeleta taharuki na kunukuliwa na vyombo vingine vya habari duniani.

“ Kichwa cha habari kilichochukuliwa na vyombo vingine vya habari kilizua hofu na taharuki duniani kwamba kirusi hicho kinasababishi magonjwa ya COVID na ni kipya tena hatari kinaweza kuachiliwa na kudhuru zaidi.

Taarifa hiyo ilianzia na Daily Mail ya Uingereza ikaendelea kukanushwa juhudi zaidi zikisema, ilikuwa “ya uwongo na si sahihi,” maofisa wa Chuo Kikuu Boston wakihaha kupinga kila kilichoripotiwa wakisema kuwa kwa sababu majaribio yaliyofanywa katika maabara yake ya South End kweli yalifanya virusi hivyo kuwa hatari.

Na hapa kuwa na ushahidi kwamba jaribio hilo, ambalo lilikuwa limeidhinishwa na kamati ya ndani ya ukaguzi wa usalama wa viumbe na Tume ya Afya ya Umma ya Boston, lilifanyika kwa njia isiyo salama au isiyofaa.

Boston inasema ripoti ya awali, ambayo baadaye ilichukuliwa na Fox News na vyombo vingine vya habari, ilichota mstari mmoja kutoka kwa taarifa ya awali iliyochapishwa na wanasayansi wa maabara nje ya utaratibu.

Kichwa cha habari cha gazeti hilo kilisema watafiti wa BU wameunda aina ya COVID na “kiwango cha kuua ni asilimia 80 ikionyesha majaribio hatari yanayohofiwa kuanzisha janga upya.”




Mabingwa wa kupambana na corona na virusi vya COVID-19 maradhi ambayo huangamiza watu lakini pia kutikisa sekta ya afya. **PICHA: MTANDAO**

Maofisa wa chuo kikuu wanasema toleo la mseto lililotengenezwa na maabara la virusi vya SARS-CoV-2 liliua asilimia 80 ya panya, lakini hiyo ilikuwa mbaya sana kuliko aina ya asili ya Wuhan, ambayo iliua asilimia 100 ya panya katika jaribio la kulinganisha.

Ripoti za habari pia hazikugundua kuwa viwango vya vifo kutoka kwa coronavirus kwenye panya ni tofauti sana na vile vya wanadamu.

Kwa kweli, Robert Davey, profesa wa biolojia katika maabara ambaye hakuhusika katika jaribio hilo, anasema panya sio wanyama wa kuaminika sana kutumia katika majaribio ya maabara ya vrusi vya corona.

**ONYO JIPYA**

XBB, BQ.1.1, BA.2.75.2 ni kundi tofauti la kirusi linaloweza kuchochea kuongezeka kwa msimu wa baridi Gazeti la Washington Post la Amerika la Oktoba 18, 2022, linasema likakoleza moto kwa maelezo kuwa kuna maongezeko hayo mwisho wa mwaka unapokaribia.

Kwa miaka miwili, aina mbalimbali za virusi vya corona ziliibuka, moja baada ya nyingine, zikienea duniani kote lakini msimu huu wa baridi au winta inahofiwa itakuwa tofauti, linaongeza.

Badala ya aina moja ya kutisha inayojificha kwenye upeo wa macho, wataalamu wanatazama kwa hofu kundi la virusi na awamu mpya ya mageuzi au mabadiliko ndani ya seli na jeni za kirusi katika janga hilo.

Kwa wakati huu, kuna uwezekano kwamba dunia itakabiliwa na mkusanyiko mpya wa virusi vyenye alfabeti za Kigiriki, badala yake toleo moja au zaidi kati ya mengi ya mbadala wa omicron yanayoendelea kujitokeza yanaweza kuendesha watu kikamilifu.

Ni ladha tofauti za omicron, lakini zinafanana - zimepambwa kwa mchanganyiko sawa wa mabadiliko.

Kila toleo jipya linatajwa kuwa linalishinda la mwisho katika uwezo wake wa kukwepa ulinzi wa kinga na kuzichanganya ili kuharibu mwili. “Ni mbio hizi za mageuzi za silaha tunazokuwa nazo na virusi hivi,” Jonathan Abraham, profesa msaidizi wa biolojia katika Shule ya Matibabu ya Harvard, anasema akiongeza kuwa miaka miwili, matoleo ya virusi vya corona yaliibuka, moja baada ya nyingine yakaenea duniani kote.

Lakini majira haya ya kiangazi na ya baridi yanatarajiwa kuwa tofauti badala ya toleo moja la kuogofya linalonyemelea upeo wa macho, wataalamu wana wasiwasi kuwa wakati huu, kuna uwezekano kwamba dunia itakabiliwa na mkusanyiko mpya wa alfabeti za Kigiriki pengine kuanzia alfa, beta, gama hadi zote.

Ni kwa sababu matoleo mengi ya mbadala wa omicron yanayoendelea kujitokeza yanaweza kuendesha wimbi linalofuata ni kama omicron, lakini yanapambwa kwa mchanganyiko sawa wa mabadiliko.

Kila kipya kinachoibuka kinaonekana kushinda kilichokitangulia katika uwezo wake wa kukwepa ulinzi wa kinga.

“Ni mbio hizi za mageuzi za silaha tunazokuwa nazo na virusi hivi,” Jonathan Abraham, profesa msaidizi wa biolojia katika Shule ya Matibabu ya Harvard.

Mwezi mmoja uliopita, wanasayansi walikuwa na wasiwasi kuhusu BA.2.75, toleo jipya la kirusi lililoanzia Asia Kusini na kuzaa wingu la hofuduniani.

Nchini Marekani, BA.4.6 na BF.7 zimekuwa zikivuta kasi na wiki chache zilizopita, BQ.1.1 ilianza kuonekana ikisambaa

Ulaya na Amerika Kaskazini lakini kirusi kingine kinachoitwa XBB kinakuja na kinatishia maisha japo ukweli ni kwamba masuala ya COVID-19 yanakotoka yana maswali mengi kuliko majibu. Yaelekea UVIKO-19 ni biashara inayochochea kuuza chanjo na dawa za kuudhibiti.

***MITANDAO.***

## WANENAVYO MALENGA

# LAKINI TUTAFIKA TU

PALE mimi nimepita, sitaki wewe upite,
Kisima nilichochota, sitaki wewe uchote,
Mali nilipookota, sifurahi uokote,
Ni mambo ya walimwengu, lakini tutafika tu.

Kisirisiri wateta, yenu yenu asipate,
Mnaujenga ukuta, kuupandia asote,
Mwaweka mwingi utata, ajaribu atepete,
Ni mambo ya walimwengu, lakini tutafika tu.

Mechanga vema karata, yeye ng'anda azipate,
We afande ye kuruta, vya chini aviokote,
Ujinga umeufuta, yeye umfuate,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Mpangaji kwenye data, nyumba wapi aipate,
Kila akifurukuta, ili keki aing'ate,
Ukingoni anagota, acha wembe umkate,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Ukuu aliupata, walifanya aupate,
Baraka alizochota, waliziacha zipite,
Yeye kazi kukong'ota, ili waipatepate,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Miaka ndiyo avuta, misuli ivutevute,
Kitu chini kuokota, shida yaja aipate,
Wadogo wa kuokota, lizuia wasipite,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Ombwe lile twalikuta, haohao tuwasute,
Kufanya watu kusota, mpini uwakong'ote,
Wakutwe waweze juta, njia ngumu waipite,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Korosho nimeokota, eti nikaange zote,
Nitengeneze mafuta, kutafuna zinipite,
Nakataa katakata, za kutafuna nipate,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Marais wanapita, tena twasema wapite,
Na majaji wanapita, wengine chansi wapate,
Na wazazi wanapita, wazee wapya tupate,
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

Hekima anapopata, kesho mema tuyapate,
Ni kwa vile ulipata, unao umatemate,
Leo huyu wamfuta, koroma uziokote!
Ni mambo ya malimwengu, lakini tutafika tu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

TEKNOLOJIA

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Unajua kunawa mikono kikamilifu au unalipua, fuata hatua hizi uwe salama



Wanafunzi wa Sekondari ya Ngokolo wakipewa elimu kwa vitendo namna ya kunawa mikono kwa ufasaha hasa wanapotoka kujisaidia kuepuka maradhi. **PICHA: MARCO MADUHU**

KUTOKUNAWA mikono ipasavyo hasa iliyochafuliwa na kinyesi cha binadamu ni moja ya chanzo kikuu cha kuenea magonjwa, zama hizi virusi vikihama kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa wengine kwa njia ya kugusa choo, maji maji za mwili wa aliyeathirika kama damu na haja ndogo.

Pamoja na maradhi yanayotokana na virusi, uchafu wa kinyesi huambukiza magonjwa ya ya kuhara na kutapika, kipindupindu na homa ya matumbo.

Katika maeneo ya shule suala la kuzingatia usafi ni jambo muhimu kutokana na wingi wa watu, ili kujilinda na maradhi mbalimbali yatokanayo na uchafu hasa wa kinyesi.

Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wa usafi wa mazingira (WASH SDG) kipingele cha unawaji mikono, linaunga mkono juhudi za kukabiliana na maradhi yanayosababishwa na kutokunawa mikono.

Upo msemo kuwa elimu haina mwisho, ukimaanisha kuwa kila leo watu hujifunza jambo jipya na hilo linadhihirishwa na wataalamu kutoka Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wa usafi wa mazingira (WASH SDG) kipingele cha kunawa mikono, wanapowafundisha usafi wa mikono wanafunzi wa Manispaa ya Shinyanga.

Wanaamua kutoa elimu ya kunawa mikono kwa ufasaha kwa wanafunzi shuleni katika shule za Msingi na Sekondari Manispaa ya Shinyanga.

Ofisa mradi msaidizi wa usafi na mazingira kutoka SNV, Issack Msumba, anasema ni muhimu wanafunzi kupewa elimu ya kunawa mikono kwa ufasaha sababu ya wingi wao, na lisipozingatiwa kunaweza kutokea milipuko ya magonjwa.

Anasema pamoja na kutoa elimu hiyo, pia wameunda klabu za afya na mazingira shuleni ili wanafunzi waendelee kufundishana na kuhimizana kunawa mikono mara kwa mara na kwa usahihi hasa wanapotoka chooni ili kujikinga na magonjwa.

> "Watoto wakipata elimu hii kwa ufasaha pia watakwenda kuisambaza majumbani mwao na kuisaidia jamii kukabiliana na magonjwa yanayochangiwa na uchafu wa mikono," anaongeza.

"Wanafunzi wakumbushwe hatari ya kupatwa na magonjwa ya mlipuko sababu ya kula uchafu wenye vimelea vya maradhi ndiyo maana tukaamua kutoa elimu hii ya kunawa mikono katika shule zote za Manispaa ya Shinyanga Msingi na Sekondari," anasema Msumba.

"Watoto wakipata elimu hii kwa ufasaha pia watakwenda kuisambaza majumbani mwao na kuisaidia jamii kukabiliana na magonjwa yanayochangiwa na uchafu wa mikono," anaongeza.

Ofisa Elimu masuala ya afya na mazingira kwa shule za msingi na sekondari Manispaa ya Shinyanga, Beatrice Mbonea, anasema elimu ya kunawa mikono shuleni ni jambo sahihi linalowaepusha watoto na walimu na maradhi mbalimbali.

Anasema wanachozingatia ni kusugua viganja vyao na mianya yote ya vidole kwa kutumia sabuni na maji tiririka. Kunawa mzunguko wa dole gumba hadi kwenye kiwiko na kujikausha kwa kutumia vitambaa au kutikisa mikono hewani ikiwa imeelekea juu ili kuwa salama.

Anawasihi wanafunzi kuzingatia elimu wanayopewa ya kunawa mikono yao ili isiwe chanzo cha walimu wao kula uchafu kikiwamo kinyesi wakati wa kuwahudumia ikiwamo kusahihisha kazi zao.

Anasema walimu wamekuwa wakila taka hizo wakisahihisha madaftari ya mwanafunzi, ambaye ametoka maliwatoni kujisaidia, lakini hakunawa mikono kikamilifu.

"Wanaweza kuathirika kutokana na ukweli kuwa ili ufunue ukurasa wa daftari kusahihisha lazima ujilambe kidole na endapo hawatanawa kikamilifu tayari atakuwa umememlisha mwalimu kinyesi na kuhatarisha afya yako," anasema Mbonea.

"Nawaombeni sana wanafunzi mzingatie kunawa mikono muda wote hasa mnapotoka kujisaidia, ili kulinda afya za walimu wenu na zenu pia," anaongeza Mbonea.

Mwalimu wa Mazingira wa Sekondari ya Ngokolo, Ernest Ngarama, anasisitiza ulazima wa kunawa mikono ili kulinda afya za walimu na wanafunzi, akiongeza kuwa kwa nafasi yake ya usimamizi wa mazingira amekuwa akitoa elimu ya kunawa mikono mara kwa mara kwa wanafunzi, ili kuhakikisha hawaweki rehani afya za walimu wao kupitia kusahihisha madaftari.

"Ni kweli afya zetu walimu zipo hatarini endapo wanafunzi wasipozingatia usafi kwa kunawa mikono kwa ufasaha hasa wanapotoka kujisaidia, ndiyo maana tunaendelea kutoa elimu ili wao na sisi tuwe salama," anasema Ngarama.

Mwenyekiti wa Klabu ya Afya na Mazingira ya Sekondari ya Ngokolo, Mariamu Enock, anasema kupitia klabu yao wametoa elimu ya usafi na mazingira kwa wanafunzi wenzao hasa kunawa mikono.

Anasema kwenye klabu yao wapo wanachama 52 na shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 1,281 ambapo wao awali walishapewa mafunzo namna ya kunawa kutoka SNV, elimu ambayo wamekuwa wakiitoa kwa wenzao.

"Kupitia klabu yetu ya afya na mazingira, tutaendelea kuwahamasisha wanafunzi wenzetu wazingatie suala la usafi la unawaji mikono hasa wanapokuwa wakitoka kujisaidia sababu maji yapo ya kutosha ili kuimarisha usafi na kujikinga na maradhi.

"Shuleni kwetu maji yapo ya kutosha, vyoo vipo vizuri na kwenye mabomba ya maji kunasabuni kwa ajili ya kunawa mikono, nawasihi wanafunzi wenzangu tuzingatie kusafisha mikono mara kwa mara na kiufasaha ili kujilinda na maradhi yatokanayo na kula uchafu," anasema Mariam.

## HABARI PICHANI



Mkuu wa Shule ya Sekondari Kerege, Bagamoyo mkoani Pwani, Kasika Mateko, akizungumza kwenye mahafali ya kidato cha nne ya shule hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (kushoto), akiendesha harambee ya kuchangia fedha za ujenzi wa msikiti katika sherehe za Maulid ya Mtume Muhamad S A W iliyofanyika kimkoa Kijiji cha Kimande, Kata ya Itunundu, wilayani humo juzi, ambapo Sh. 765,600 zilipatikana. P**ICHA: STEVEN WILLIAM**




Mafundi wakijenga kituo cha mabasi ya mwendokasi eneo la Mbagala Rangi Tatu juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

## CHEMSHABONGO NA -00 16 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
4. muwa
7. sampuli
8. kasirika ghafla
10.matokeo mabaya 14.nsi
16.mdudu anayekaa katika nywele
17.mtu mgomvi mwenye maneno ya ufidhuli 20.shikwa na hasira juu ya jambo 21.mji mkuu Eritrea
23.pengine 25.alika
26.hema takatifu kwa wayahudi


Chini:
1. mahali pa kulia chakula
2. nema
3. sehemu ya kuhifadhia fedha
5. fidia 6. kiongozi wa Jamhuri
9. kileo cha sukari na mchele
11.acha kinywa wazi 12.madini
13.kitu kisichotosheleza uhitaji
15.kitengo cha kurusha matangazo ya redio 17.vazi linalovaliwa sehemu ya juu ya mwili
18.kiongozi wa Wanyamwezi
19.miungu wa uwongo
22.Mja 24.iliyopita kiasi




## Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

ANGALIWA
BARAFU
ARALIA
UBAYA
MIMBA
GHALA
UASI
HAIBA
ASMARA
LIBYA
MAUAJI
BANDAMA
TIMUA
KABLA

RAI
MTI
DUA
GUMU
KADA
RUDI
AALI
MADA










## Viongozi wa dini waipa 5 serikali kuanzisha bima ya afya kwa wote

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa dini Mkoa wa Mbeya wameipongeza serikali kwa kuanzisha muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa maelezo kuwa itasaidia wananchi wengi kuwa na uhakika wa matibabu kabla ya kuugua.

Walitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo maalumu ya kuwaelimisha kuhusu utaratibu huo wa bima ya afya kwa wote yaliyoandaliwa na uongozi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) Mkoa wa Mbeya, Daudi Sichinga, alisema mpango huo una faida kubwa kwa wananchi na kwamba ni vema uanze mapema ili kuokoa maisha ya Watanzania maskini.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kuja na mpango huu mahususi kwa ajili ya kusaidia jamii hasa kwa upande wa afya kwani siyo wote walio na uchumi wa kuwawezesha kupata matibabu,"alisema Padri Sichinga.

Shekhe Ibrahim Omary Bombo, aliipongeza Wizara ya Afya kupitia uongozi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya kwa kuona umuhimu wa kuwajengea uelewa viongozi wa dini kwa maelezo kuwa nao ni wadau muhimu kwenye shughuli hiyo.

Alisema watatumia nafasi zao kuwahamasisha wananchi kuchangia bima hiyo kutokana na kwamba suala la afya linahitaji ushirikiano kwenye kulishughulikia.

Mchungaji kutoka Jumuiya ya Makanisa Kipentekoste Tanzania (CPCT), Erika Mwakyolile, alisema suala la Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote limechelewa kuanza kwa maelezo kuwa lilitakiwa lianze mapema kama ilivyo kwenye mataifa mengine.

Alisema watahakikisha wanashirikiana na serikali kuhamasisha jamii kwa kuwa afya ni muhimu, hivyo jamii kama inavyochangia sherehe nyingine, pia wachangie bima ya afya ili kulinda afya zao.

"Nitoe rai kwa watu wote hata kwa serikali kwamba ni kweli tulichelewa sana, tunashukuru kwa mwaliko huu, sisi kama watumishi wa Mungu tunaamka kwa nguvu zote kwenda kuelimisha watu wetu," alisema Mchungaji Erika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, aliwashukuru viongozi wa dini wa Mkoa wa Mbeya kwa umoja na ushirikiano walioonyesha katika kushirikiana na serikali.

Alisema Tanzania ipo nyuma kwenye suala la bima kwa maelezo kuwa mpaka sasa ni asilimia 15 pekee ya Watanzania ambao wamejiunga na bima ya afya tofauti na ilivyo kwenye mataifa mengine.

Alisema endapo muswada huo utapitishwa na Bunge na kuwa sheria kuna uwezekano taifa likapiga hatua na kuwa miongoni mwa mataifa yenye idadi kubwa ya watu waliojiunga na bima hiyo.

# Wazalishaji mbolea wataka sera kuhamasisha kilimo ikolojia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZALISHAJI wa mbolea za asili na wakulima katika mikoa ya Mbeya na Songwe, wameiomba serikali kutunga sera itakayohamasisha matumizi ya kilimo ikolojia ambayo itahamasisha matumizi ya mbolea hiyo katika uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini na kusaidia kutunza mazingira.

Rai hiyo ilitolewa juzi na wakulima pamoja na wadau wanaohusika na uzalishaji wa mazao mbalimbali wakijadiliana namna kilimo cha ikolojia kitakavyoweza kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija na kuongeza rutuba katika udongo.

Walisema utungaji wa sera unaweza kuwa msaada wa kuhamasisha kilimo hicho.

Miongoni mwa wakulima hao akiwamo Tujolege Mwakisunga kutoka Kijiji cha Ndobo wilayani Kyela alisema serikali inapaswa kutengeneza mifumo mizuri ya kuboresha kilimo cha ikolojia ambacho kina tija kwa mkulima.

Mwakisunga alisema mfumuko wa pembejeo za kilimo umewaibua wabunifu wa kuzalisha mbolea ya asili ya kutumia samadi na mabaki ya mpunga, hivyo ni wakati sasa serikali kuwaunga mkono jitihada hizo ili kuongeza tija ya uzalishaji na kuwapo masoko ya uhakika ya ndani na nje.

"Msimu huu wa kilimo tumepata shida sana bei ya pembejeo ilipanda bei kupita kiasi tunashukuru wataalamu wakiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA) walifanya utafiti wa udongo na kuhamasisha kilimo ikolojia kinachohamasisha matumizi ya mbolea ya asili ili kuongeza uzalishaji wa mazao," alisema Mwakisunga.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Mababu Wilaya ya Kyela, Benjamin Mwaijumba, alisema kuwa uwapo wa kilimo cha ikolojia kimekuwa na tija kwa wakulima kutokana na kuwapo kwa mfumuko wa gharama za pembejeo za kisasa.

"Tulifikiwa na kupatiwa elimu na watafiti wa taasisi mbalimbali za serikali na wakulima walipojaribu kilimo hicho wameona kina tija sana na pia kinachangia kufufua uhai wa ardhi ambayo imeharibiwa na matumizi ya mbolea zenye simu," alisema.

Mtaalamu wa mazao kutoka Jukwaa Huru la Wadau wa Kilimo (ANSAF), Owen Nelson, alisema kuwa utafiti walioufanya katika sekta ya kilimo wamebaini uwapo wa manufaa makubwa kwa wakulima kutumia kilimo cha ikolojia kwa kutumia mbolea ya asili tofauti na za kisasa.

"Suala hapo ni wakulima kuzingatia elimu ya kitaalamu katika uzalishaji pia serikali ione umuhimu wa kuweka sera ya kuboresha kilimo cha ikolojia ili kuweza kutambulika ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa masoko kwa wazalishaji wa ndani," alisema.

Mwakilishi wa Ofisa Kilimo Mkoa wa Mbeya, Adam Mhagama, alisema kuwa tatizo ni maofisa ugani ambao wamekuwa wakitoa elimu ya matumizi ya pembejeo za kilimo za kisasa badala ya za asili ambazo ni nafuu kwa mkulima kutokana na mfumuko wa bei ya pembejeo nchini.



Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe (wa pili kulia), akielezwa na mmoja wa wafanyakazi wa Kiwanda cha Brew Master cha jijini Mbeya namna kinavyozalisha vinywaji vikali aina ya Pan Master alipokwenda kukizindua mwishoni mwa wiki, (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wizara ya Viwanda yaagiza wajasiriamali kupewa ushirikiano

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZARA ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, imeziagiza taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kutoa ushirikiano kwa wajasiriamali na kuhakikisha sekta ya viwanda inakua na kuendelezwa kwa lengo la kukuza pato la taifa. Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Exaud Kigahe alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akizundua kiwanda cha kuzalisha vinywaji vikali cha Brew master kilichoko jijini Mbeya.

Aliwataka watendaji wa taasisi hizo kila mmoja kutimiza wajibu wake ili kuhakikisha sekta ya viwanda na biashara inakuwa miongoni mwa sekta zinazoliingizia taifa pato kubwa.

"Nawaagiza watendaji wa taasisi zote zilizo chini ya wizara yangu kushirikiana na wajasiriamali wanaoanzisha viwanda ili kuhakikisha sekta hii inakuwa kwa kasi na kuongeza ukusanyaji wa pato la taifa," alisema Kigahe.

Aidha, aliupongeza uongozi wa kiwanda hicho kwa kubuni biashara hiyo akieleza kuwa kiwanda hicho ni miongoni mwa shughuli ambazo zimesaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana nchini.

Aliwataka kuendelea kukipanua kiwanda hicho ili kuongeza uzalishaji na kuongeza ajira kwa wananchi hasa wa Jiji la Mbeya na kwamba serikali itaendelea kuwasaidia ili uwekezaji huo uwe na tija.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuandaa maeneo ya uwekezaji na kuunda sera na sheria ambazo zitakuwa rafiki kwao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alivitaka viwanda vinavyoanzishwa mkoani humo kuwajibika kulipa kodi ipasavyo ili kuongeza pato la mkoa na taifa kwa ujumla kukua.

Alisema Mkoa wa Mbeya kwa sasa ni miongoni mwa mikoa nchini ambayo pato lake ni kubwa hutokana na kuwa na shughuli nyingi za uzalishaji ikiwamo viwanda, kilimo na shughuli za uchimbaji wa madini.

Alisema serikali ya mkoa huo imetenga maeneo ya uwekezaji katika kila wilaya kwa ajili ya shughuli mbalimbali za uwekezaji ikiwamo viwanda na hivyo akawataka wawekezaji wa maeneo mengine kujitokeza kuwekeza.

"Sisi sasa hivi Mkoa wa Mbeya ni wa tatu kitaifa kuwa na uchumi mkubwa baada ya Dar es Salaam na Mwanza, kwa hiyo naamini kwamba tukishirikiana vizuri baina ya wawekezaji na serikali uchumi wetu utazidi kuwa imara," alisema Homera.

Hata hivyo alizitaka taasisi za kifedha katika mkoa huo kuendelea kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wawekezaji ili uwekezaji wao uwe na tija zaidi.

Mkurugenzi wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO), Prof. Sylivester Mpanduji, alizitaka taasisi za kifedha nchini kuongeza viwango vya mikopo ili kuwezesha Watanzania wengi zaidi kuanzisha viwanda.

Alisema taasisi za kifedha zikitoa mikopo ya kutosha zitawasaidia wawekezaji kuwa na uwezo wa kununua mitambo pamoja na malighafi kwa ajili ya uendeshaji wa viwanda hivyo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kiwanda cha Brew Master, Musa Leonard, alisema kiwanda hicho kwa sasa kimeajiri zaidi ya Watanzania 300 ambao wanafanya kazi mbalimbali ikiwamo uzalishaji.



# Mpanju aanika siri ya ukuzaji uchumi nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalaum, Amoni Mpanju, amesema Watanzania ili waweze kukuza uchumi lazima vyuo vya maendeleo ya jamii nchini viwekeze kwa watu kwa kuwapatia maarifa yanayoendana na wakati uliopo.

Alisema kupitia Ibara ya 229 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 hadi 2025 imeelekeza kuwapatia vijana elimu na ujuzi ili waweze kujikwamua na kujiinua kiuchumi.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akifunga mkutano wa mwaka wa tathmini wa viongozi wa vyuo na taasisi zilizoko chini ya wizara hiyo uliofanyika jijini Dodoma kuanzia Oktoba 17 hadi 22.

Akifunga mkutano huo Mpanju alivitaka vyuo na taasisi hizo kuweka kipaumbele katika dhana tatu za uwanagenzi, maarifa na ushirikishwaji wa jamii sambamba na kufanya tafiti, huku akiwasisitiza kuzingatia sheria, taratibu na miongozo kwa miradi inayotekelezwa.

"Mhakikishe hizi dhana tatu za uanagenzi ambazo ni ushirikishaji wa jamii, ubunifu na maarifa mnaweka mikakati madhubuti ili kuendeleza na kusimamia maeneo hayo," alisema Mpanju.

Aidha, alivitaka vyuo na taasisi hizo kuongeza nguvu katika maeneo yenye matatizo ambayo ni eneo la utafiti na huduma shirikishi.

"Kama tatizo ni bajeti itengewe kwa mwaka wa fedha ujao wa fedha na pia ninyi muwe na ushirikiano na vyuo vya ndani na nje ya nchi," alisema.

Aliwaagiza wakuu hao wa vyuo, waratibu na wakufunzi wa vyuo kuhakikisha wanapinga na kukemea ukatili unaojitokeza na unaoendelea kushamili katika jamii kwa kuanzisha madawati ya jinsia ili yaweze kusaidiana kupambana na vitendo hivyo.

"Tuna janga la ukatili wa wanawake na watoto, kitu ambacho kinaathiri nguvu kazi ya taifa na kuondoa amani kwa familia na jamii, hivyo mnatakiwa muanze kuandaa midahalo yenye lengo la kujadili matatizo ya jamii, muweke ushirikiano na serikali za mitaa ili kuleta mabadiliko," alisema Mpanju.

Mkurugenzi Msaidizi Usimamizi wa Vyuo kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Neema Ndoboka, alisema lengo la mkutano huo ni kufanya tathmini ya mwaka kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa mwaka wa masomo ili kuboresha utendaji kazi na kuleta matokeo chanya na tija iliyokusudiwa.




Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima nchini (TEWW), Dk. Michael Ng'umbi, akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa Maelezo jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/23. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Chuo cha Mipango chapanga kudahili wanafunzi 16,663

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Prof. Hozen Mayaya, amesema katika mwaka huu wa fedha wamepanga kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 14,417 hadi 16,663.

Aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti katika chuo hicho katika mwaka wa fedha 2022/23.

Prof. Mayaya alisema chuo hicho kinaendelea kupitia mitaala ya mafunzo ya muda mrefu na kuandaa mitaala ya kozi mpya na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga miundombinu ya kufundishia.

Alitaja vipaumbele vya mwaka huu wa fedha kuwa ni kuendelea kuajiri watumishi wapya, kulipa stahili mbalimbali, kupandisha vyeo watumishi waliokidhi vigezo pamoja na kuboresha huduma za ustawi na kuongeza uwezo wa kielimu na kiutendaji kwa watumishi 396.

Kuhusu utekelezaji wa majukumu ya chuo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22, Prof. Mayaya alieleza kuwa hadi kufikia Juni 2022, watumishi 351 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 50 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi.

Alisema Sh.bilioni tisa zimetumika kugharamia utekelezaji wa miradi ya uendelezaji na utunzaji wa miundombinu ya chuo, kwamba Sh. bilioni 5 zimetumika katika ujenzi wa kumbi tatu za mihadhara na mabweni mawili ya wanafunzi wa kike.

Alifafanua kuwa kati ya Sh.bilioni tisa, Sh. bilioni nne ambazo ni mapato ya ndani zimetumika kutekeleza miradi katika kituo cha mafunzo kilichoko Mwanza ikiwamo ujenzi wa mgahawa, jengo la utawala, maktaba na kununua ardhi kwa ajili ya upanuzi wa chuo.

Sambamba na hilo alisema kuwa katika mwaka wa masomo 2021/22, chuo kimeendesha programu za muda mrefu 31.

Alisema: "Mpaka kufikia Juni 2022, washiriki 31 wa nje wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Kwa mwaka 2021/22, chuo kimesajili jumla ya wanafunzi 14,461. Aidha, jumla ya wahitimu 8,200 wamehitimu Desemba, 2021."

Profesa Mayaya alisema: "Katika mwaka wa fedha 2021/22, chuo kiliwezesha wahadhiri wake kufanya tafiti saba zinazolenga kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi na kuchangia kuandaa sera na miongozo mbalimbali ya kitaifa."

# Samia kuzindua matokeo ya sensa wiki ijayo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuzindua matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi Oktoba 31, mwaka huu katika Uwanja wa Jamuhuri jijini Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Shenyamule, alibainisha hayo juzi jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu uzinduzi wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Alisema maandalizi ya uzinduzi huo yanaendelea vizuri na serikali imejiandaa kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata fursa kufahamu matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi.

"Kama mnavyofahamu serikali ilikamilisha rasmi mchakato wa kuhesabu watu, majengo na anwani za makazi kupitia mfumo wa utekelezaji wa Sensa ya Watu na Makazi. "Mchakato huo ambao ulishirikisha watu wote waliolala ndani ya mipaka ya nchi yetu usiku wa kuamkia siku ya sensa yaani Agosti 22 kuamkia Agosti 23, 2022, lilifanyika kwa mafanikio makubwa," alisema.

Kadhalika alisema kwa mujibu wa mpango wa utekelezaji na usimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi, baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuhesabu watu, kazi zinazotakiwa kufanyika ni kuchakata taarifa zilizokusanywa ili kupata matokeo yake na hatimaye kutangazwa rasmi kwa umma matokeo ya mwanzo.

Vile vile alisema baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuhesabu watu Septemba 5, mwaka huu, wataalamu walianza uchakataji wa taarifa hizo na hadi sasa matokeo ya mwanzo yapo tayari kwa uzinduzi.

"Katika mnasaba huo ninayo furaha kutangaza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, atazindua matokeo ya mwanzo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Oktoba 31, mwaka huu katika Uwanja wa Jamuhuri jijini Dodoma,"alisema.

Aidha, alisema utoaji wa matokeo ya sensa ya mwaka 2022, unafanyika mapema zaidi kuliko ilivyokuwa katika miaka iliyopita.

"Kwa mfano Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 na ile ya mwaka 2012 ambazo zilitumia teknolojia ya usomaji wa vivuli matokeo ya sensa hizi yalizinduliwa rasmi miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuhesabu watu," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa sensa ya mwaka huu matokeo yake yatatoka ndani ya kipindi cha mwezi mmoja baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuhesabu watu.

Alisema: "Haya ni mafanikio makubwa katika utekelezaji wa sensa nchini kwetu na yamewezekana kutokana na matumizi makubwa ya teknolojia za kisasa hasa matumizi ya vishikwambi katika awamu zote za utekelezaji wake na utashi wa siasa katika kusimamia zoezi hilo kuanzia maandalizi hadi leo."





## Waziri: SMZ inathamini mchango wa wahudumu wa afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inathamini na kutambua mchango mkubwa wa wahudumu wa afya wa kujitolea katika jamii.

Alisema mchango wao ni sehemu muhimu ya mfumo wa afya na serikali inaendelea kuwategemea kwa wingi wa shughuli katika ngazi ya jamii.

Aliyasema hayo jana katika maadhimisho ya miaka 77 ya Umoja wa Mataifa zilizofanyika katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar.

Waziri Mazrui alisema mkakati wa afya ya jamii 2019-2024 unatambua majukumu na kazi muhimu za wahudumu wa afya wa kujitolea katika jamii na unajumuisha mkakati wa jinsi ya kuwawezesha kwa utendaji bora.

Aidha, alisema serikali inatambua kuwa CHVs wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwapo kufanya kazi katika mazingira mangumu.

Alisema serikali itaendelea kuwapa ushirikiano wahudumu wa afya wa kujitolea ili huduma za afya ziwafikie watu wengi zaidi hususani wale waliopo pembezoni na mazingira hatarishi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe, alisema Umoja wa Mataifa (UN) upo mbele kufanya kazi kwa jamii kwa kuunga misingi ya maendeleo.

Alisema umoja huo kwa kushirikiana na serikali umeunga mkono harakati katika kuimarisha wanawake katika siasa, kufanya maamuzi na kukabiliana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Akisoma risala ya wahudumu wa afya wa kujitolea, Husna Yunus Alimia, alisema kuna matatizo katika vituo vya afya ikiwamo ukosefu wa vipimo muhimu, shinikizo la damu, uzito, dawa za damu na uhaba wa madaktari.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa, Shalini Buluguna, aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza mipango ya usawa wa kijinsia na kuiingiza katika utekelezaji wake wa taifa wenye lengo la kuleta mabadiliko makubwa kwa jamii ya wanawake na kuwakomboa kiuchumi.

"Shirika la Umoja wa Mataifa limefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza mipango yake ambayo imejikita katika kuona usawa wa kijinsia unafikiwa ambao utawawezesha wanawake kufikia malengo ya uongozi,"alisema.

Siku ya Umoja wa Mataifa huadhimishwa Oktoba 24 ya kila mwaka na kauli mbiu ya mwaka huu katika maadhimiisho hayo ni 'Jamii jumuishi hakuna anayeachwa nyuma'.

# W'biashara wanaopandisha bei ya bidhaa kufutiwa leseni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, imesema wafanyabiashara ambao watashindwa kufuata bei elekezi iliyowekwa na serikali kwa bidhaa za chakula watachukuliwa hatua kali ikiwamo kufutiwa leseni.


Onyo hilo lilitolewa na Waziri wa Wizara hiyo, Omar Said Shaaban, alipofanya ziara ya ukaguzi wa maduka yanayouza bidhaa ikiwamo za chakula katika maeneo ya Darajani na Mlandege.

Alisema serikali pamoja na wafanyabiashara wamekubaliana kwa pamoja bei ya bidhaa mbalimbali za chakula, kuweka bei elekezi ambayo tayari imefanyiwa tathmini zote ikiwamo faida kwa wafanyabiashara.

Alisema kitendo cha wafanyabiashara hao kuuza vyakula kwa bei wanayotaka wao na kukiuka makubaliano ni kosa kwa mujibu wa sheria za biashara na ushindani wa mlaji.

Alizitaja baadhi ya bidhaa ambazo serikali kwa kushirikiana na wafanyabiashara zimewekewa bei elekezi ikiwamo sukari, mchele pamoja na unga wa ngano, bidhaa ambazo ushuru wake tayari umepunguzwa na serikali.

Mkurugenzi wa Tume ya Ushindani Zanzibar, Mohamed Sijamin Mohamed, aliwataka wafanyabiashara kuhakikisha wanafuata bei elekezi ambayo ni makubaliano kati ya serikali na wafanyabiashara.




Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui (wa tatu kulia), akiangalia kitabu katika maonesho ya Siku ya Umoja wa Mataifa (UN) akiwa na viongozi mbalimbali, (kulia) ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Raziki Pembe na Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa, Shalini Balaguna, jana Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## 'Zanzibar imebarikiwa maeneo ya ufugaji mazao bahari'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Aboud Suleiman Jumbe, amesema kuwa Zanzibar imebarikiwa kuwa na maeneo bora ya ufugaji wa mazao bahari ikiwamo kaa, samaki na vitango bahari (jongoo la pwani).

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya utiaji saini ya kuingia ubia wa uendeshaji wa kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki kilichoko beit- raas baina ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini na Kampuni ya Afrivision.

Jumbe alisema matango bahari hutumika katika chakula, dawa na vipodozi na bidhaa hiyo ina soko kubwa katika nchi za Asia, China, Japan na Korea.

Alisema kabla ya ugonjwa wa Uviko-19 tani 4,600 ya vitango bahari ulimwenguni vilinunuliwa katika Bara la Asia sawa na thamani ya Dola za Marekani bilioni moja.

Alisema katika Afrika kuna nchi tano kuu zinazoongoza kwa biashara ya vitango bahari ikiwamo Zanzibar, Tanzania BAara, Madagascar, Msumbiji, Seychels na Mauritania.

Aidha, alisema, kwa pamoja nchi hizo zilipeleka China na Honkong tani 230 za matango bahari katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Zanzibar pekee ilisafirisha tani 30.

Alisema kwa mwaka 2021 Zanzibar imesafirisha kaa tope tani 177 nje ya nchi.

Jumbe alisema jitihada za Rais Dk. Mwinyi katika kuinua uchumi wa buluu kwa kuwawezesha wananchi kwa kuwajengea mashamba 100 ya matango bahari, mashamba 60 ya kaa tope na mabwawa 40 ya samaki wa kufuga.

"Serikali tayari imeshatenga fedha zitokanazo na kupunguza makali ya ahuweni ya Uviko-19 kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya uwezeshaji wa mazao ya baharini pekee," alisema Jumbe.

Waziri wa wizara hiyo, Masoud Suleiman Makame alisema soko la mazao ya bahari lipo la kutosha na mazao yote ya baharini yakiwamo kaa na vitango baharini yatanunuliwa kwa wakati.

Alisema serikali na sekta binafsi zimejipanga vizuri katika uhakika wa masoko ya ndani na nje ya nchi kwa mazao ya baharini.


"Leo ni siku ya furaha kwetu sote hasa wafugaji wa mazao ya baharini. Nawaomba wafugaji wa mazao ya baharini Unguja na Pemba kujipanga kutumia fursa zinazotolewa na serikali," alisema.

Aidha, alisema makubaliano hayo yaliyofikiwa ni kwamba, mgawanyo wa hisa ni asilimia 51 kwa Afrivisions na 49 kwa serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI).

Waziri huyo alisema serikali imeweka vipaumbele vya kuwaendeleza wananchi katika sekta ya uchumi wa buluu na uvuvi ikiwamo ufugaji wa mazao ya baharini, kama ufugaji wa kaa, samaki na vitango bahari. "Utiaji wa saini huu ni hatua kubwa sana, inayohitaji kuviendeleza vikundi vya wafugaji wa mazao ya baharini ambapo wengi wao ni wanawake," alisema.

Mwakilishi wa Afrivion, Fesali Juma Shabani, alisema, wanatarajia kuzalisha vifaranga vya vitango bahari na kwa mwaka wa kwanza kuwa na vifaranga milioni moja na asilimia 85 kuwanufaisha wakulima.

Alisema ubia huo utakua na manufaa makubwa kwa wananchi na taifa kwa sababu soko la vifaranga vya samaki, kaa na vitango bahari litakua endelevu.





# CWT yakemea walimu utovu nidhamu kazini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

CHAMA Cha Walimu Tanzania (CWT) Manispaa ya Shinyanga kimekemea utovu wa nidhamu unaofanywa na baadhi ya walimu na kuidhalilisha taaluma hiyo kwa vitendo vya ulevi, wizi wa mitihani pamoja na ulawiti kwa watoto.

Hayo yamebainisha mwishoni mwa wiki, kwenye mkutano mkuu wa nusu mhula wa chama hicho Manispaa ya Shinyanga, uliofanyika katika Shule ya Msingi Buhangija na Katibu wa chama hicho, Allen Shuli na kueleza kuwa vitendo hivyo vinashusha heshima ya walimu na chama.

Akisoma taarifa ya chama, Shuli alisema kinaendelea kusisitiza nidhamu kwa walimu pamoja na kuacha ulevi, wizi wa mitihani, pamoja na kudhalilisha wanafunzi wao.

Alisema walimu ni kioo cha jamii wanapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu na kuacha kufanya vitendo vibaya ambavyo vinaidhalilisha taaluma hiyo na kupoteza heshima yake ambayo ilikuwapo miaka ya nyuma.

“Chama cha Walimu Tanzania Manispaa ya Shinyanga, tunasisitiza nidhamu, uwajibikaji na utii kwa walimu wote na tunakemea matendo maovu ya ulevi wizi wa mitihani na kudhalilisha wanafunzi wetu,” alisema Shuli.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Manispaa ya Shinyanga, Meshack Mashigala, alisema chama hicho licha ya kutetea haki za walimu, wamekuwa wakionyana wakiona mienendo ya walimu sio mizuri na kuwasihi waiishi kwenye misingi ya taaluma yao na kutoichafua.

Aidha, aliiomba serikali kushughulikia matatizo yanayowakabili walimu likiwamo suala la mapunjo ya mshahara, posho za kujikimu walimu wapya, kupunguziwa nauli za likizo na wengine kulipwa nauli hizo hadi watoke likizo na wakati walipaswa kulipwa kabla.

Alitaja matatizo mengine ni kupunjwa madaraja yao toka mwaka 2013 hadi 2022, jambo ambalo limesababisha walimu walioanza kazi pamoja kutofautiana mishahara na waliotangulia kazini kuzidiwa mishahara na wanafunzi.

Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Shinyanga, Mathias Balele, aliwasilisha kilio kwa serikali akiomba kurudisha malipo ya ziada kwa walimu ili kuwaongezea kipato cha ziada na kuwapa hali ya kufanya kazi kwa ufanisi na kutojiingiza kwenye mikopo umiza.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga Jomaary Satura, aliwasisitiza walimu kuendelea kuwajibikaji kwa kuchapa kazi kwa bidii na kuahidi kuwa serikali itashughulikia matatizo yao moja baada ya jingine na kuhakikisha yanatatuliwa kwa wakati.




Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni Selous Jimbiza Camp, Arif Ahmed, (wa tatu kulia), alipotembelea banda hilo kwenye maonyesho ya 6 ya Swahili International Tourism Expo – 2022, yanayofanyika Mlimani City, jijini Dar es Salaam. Wa pili kulia ni Mtaalamu wa Magari wa Kampuni ya Selous Jimbiza Camp, Saheer Ahmed. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Walazimika kutumia maji yasiyo salama kushindwa gharama

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI katika Manispaa ya Kahama wanalazimika kutumia maji yasiyo salama ya mabwawa pamoja na mifugo yao kutokana na kushindwa kulipia gharama za majisafi yanayosambazwa katika maeneo yao.

Imedaiwa kuwa wananchi hao hutumia kipindi cha matamazamio kinachotoa nafasi kwao kuchota maji bila kulipia kwa kuchota maji hayo na baada ya kipindi hicho huacha na kurejea katika utaratibu wa kuchota maji ya kwenye mabwawa kwa kukwepa kulipia.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), Mhandisi Devotha Madata, juzi katika kikao cha majumuisho baada ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya afya, elimu na afya iliyotekelezwa na Shirika la World Vision Kata za Iyenze na Kilago kilichofanyika Manispaa ya Kahama. Madata alisema, kipindi cha matazamio ya mradi wananchi huchota maji bure kwa kipindi cha miezi kadhaa, lakini unapokabidhiwa serikalini na kuanza kuchangia gharama kwa kila ndoo ya maji, wananchi huacha kuyatumia na kurejea kutumia maji ya kwenye mabwawa na visima na wanyama wao.

Aidha, Madata alisema magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuhara damu na kuumwa matumbo hayataweza kuisha kwa wananchi wa vijiji kwa kuwa bado wanatumia maji ambayo sio safi na salama ya kwenye visima na wanyama na kushindwa kulipia gharama ya Sh. 30 hadi 50 kwa ndoo moja.

“Vituo vyetu na vya afya na zahanati zilizoko vijijini vimerekodi magonjwa mengi yanatokana na kutumia maji machafu ya mabwawa licha ya kuwapo kwa majisafi na ya uhakika, hivyo tukubali kuchangia gharama ili miradi yetu inapoharibika tupate fedha za marekebisho,” alisisitiza Madata.

Aliwataka wenyeviti wa vijiji kufanya mikutano ya hadhara mara kwa mara kuwaeleza wananchi wao umuhimu wa miradi ya maji na matumizi yake ili wayatumie ipasavyo kwa kuchangia gharama ndogo na kuondokana na magonjwa hayo ikiwa ni pamoja na kuitunza ili iwanufaishe wote.

Naye Mratibu wa miradi kata ya Iyenze na Kilago kutoka Shirika la World Vision Tanzania, Dominick Mbamba, alisema, wametekeleza miradi ya maji katika vijiji viwili vya Iyenze na Kilago kwa lengo la kuwaondolea adha wananchi kutumia maji ya visima na mabwawa ya wanyama wanao wafuga. Alisema, mradi wa kijiji cha Iyenze umekamilika na kukabidhiwa kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba na kusogeza maji katika kituo cha afya Iyenze na mradi wa Kilago bado uko katika matazamio na wananchi wanaendelea kutumia huduma hiyo bure.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo Robert Kwela, alisema vijiji vyote vilivyoko pembezoni vimepata maji kupitia wahisani World Vision Tanzania na jukumu lililobaki ni kuhakikisha maji yanafika katika shule za msingi na sekondari zisizo na huduma ikiwamo zahanati na vituo vya afya.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, aliwataka wananchi kuacha kutumia maji yasio safi na salama na badala yake watumie katika miradi iliyotekelezwa na RUWASA na ya World Vision Tanzania ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko.

## Wanaume washauriwa kupima saratani ya matiti

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATAALAMU wa magonjwa ya saratani mkoani Mwanza wamewashauri wanaume kuwa na utaratibu wa kupima ugonjwa wa saratani ya matiti wanapohisi kuwa na maumivu au uvimbe katika matiti yao.

Imeelezwa kuwa ugonjwa huo una uwezo wa kuwaambukiza watu wa jinsi zote huku wanaume wakitakiwa kwenda kupima.

Hayo yamebainishwa juzi na Dk. Ikupa Mwakapala wa kitengo cha saratani kutoka Hospitali ya Rufani Bugando akizungumza baada ya matembezi ya hisani katika maadhimisho ya mwezi wa kuhamasisha uelewa kuhusu saratani ya matiti duniani yaliyoandaliwa na Shirika la Tanzania Health and Education Supporter (THES), mkoani Mwanza.

Dk. Ikupa alisema, ugonjwa wa saratani ya matiti umeendelea kuenea kwa kasi na kuathiri idadi kubwa ya Watanzania, wanawake wakiwa na nafasi kubwa ya kuambukizwa.

“Ugonjwa huu ni hatari kwa sasa na unaambukizwa kwa watu wa jinsia zote wenye umri wa mtu mzima na unatibika endapo mtu atawahi kupima kabla ugonjwa huu haujafikia hatua ya nne ambayo hauwezi kutibika kabisa,” alisema.

Naye Dk. Henry Massawe, Katibu Mtendaji wa Shirika la THES aliwashauri watu wote kuwa na utaratibu wa kupima saratani ya matiti ili kutambua hali zao.

“Kutokana na takwimu za Shirika la Afya Duniani WHO mwaka 2020 zinaeleza kuwa ugonjwa wa saratani ya matiti unaongoza ikiwa wagonjwa milioni 2.3 wamegundulika kuwa na ugonjwa huo huku kwa Tanzania saratani hiyo inashika namba mbili kulinganisha na saratani zote, inahitajika hamasa kubwa kuhakikisha ugonjwa huu unatokomezwa,” alisema.

Akitoa taarifa ya ugonjwa wa saratani nchini, Mwenyekiti wa THES, Martine Massawe, alisema asilimia 75 ya wagonjwa wa saratani nchini hufika hospitalini wakiwa wamechelewa kutokana na kutokuwa na utaratibu wa kupima na kufahamu afya zao hatua inayosababisha ugonjwa huo kushindwa kupatiwa matibabu.

# ‘HAKUNA WA KUISHUSHA KONDE GANG’

**Na Mwandishi Wetu**


MENEJA wa msanii, Harmonize na Lebo ya muziki ya Konde Gang, Choppa, amesema kuwa hakuna wa kuishusha lebo hiyo.

Kupitia Instagram yake, meneja huyo amesema hakuna na hatatokeo wa kuishusha ama kuizuia Lebo ya Konde Gang zaidi ya Mungu na kifo.

“Hakuna kwa sasa anayeweza kuishusha au kuizua Lebo ya Konde Gang zaidi ya Mungu na kifo tu,” aliandika Meneja Choppa.

Kauli ya Choppa inakuja baada ya hivi karibuni lebo hiyo kufikishwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), na waliokuwa wasanii wao, Cheed na Killy.

Wasanii hao walitemwa rasmi kwenye lebo hiyo, Oktoba 10, mwaka huu na wao wakaamua kushitaki Basata.





# MASANJA AMNUNULIA GARI MKEWE

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI chache baada ya skendo ya mke wa mchekeshaji na mchungaji, Masanja Mkandamizaji, kudaiwa kutoka kimapenzi na katibu wa kanisa lao ambaye alijitoa uhai, mchungaji huyo sasa amemnunulia gari.

Mchungaji huyo baada ya kumalizika kwa ibada ya Jumapili katika kanisa lake la Feel Free, alimfanyia ‘sapraizi’ kwa kumzawadia gari dogo kama njia moja ya kumuonyesha upendo wake akishere-hekea kuongeza mwaka mmoja katika maisha yake.

“Heri njema ya siku ya kuzaliwa mke wangu mzuri Msukuma. Mungu akutunze, wewe ni mama bora kwa watoto wetu.

“Japo ni zawadi ndogo, lakini kwa sasa ipokee mke wangu,” aliandika Mchungaji huyo na kuweka picha akionekana kumkabidhi ufunguo wa gari hilo.

Itakumbukwa katibu wa kanisa la Masanja alijitoa uhai na kuacha barua ndefu iliyoeleza mapenzi yake kwa mke wa mchungaji huyo.

Baada ya tukio hilo Masanja alivunja ukimya kwa kusema kwamba liwake jua, inyeshe mvua, hakuwa tayari hata kidogo kumuacha mke wake kwa sababu tu ya skendo hiyo.

Kwa maneno yake, Masanja alimhakikishia mkewe upendo na kusimama na yeye muda wake wakati zogo hilo likiendelea kuteketeza wasifu wake kwenye mitandao ya kijamii.


# ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED
# MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| DESCRIPTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|
| **ACCESS RAHISI,NORMAL SAVINGS, RAHISI CAA, ELIMU, AND KIKUNDI ACCOUNT(RAHISI ACCOUNT)** | **TZS** | **USD** |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | - |
| Monthly service fees | 2,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | - |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | - |
| Bank statement 1free per month | FREE | - |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | - |
| New ATM card issuance | 10,000.00 | - |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | - |
| Replacement of the PIN | 10,000.00 | - |
| Standing order Internal | 2,000.00 | - |
| Standing order External | 12,980.00 | - |
| Dormant account fee | FREE | - |
| Interbank transfer | 10,000.00 | - |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Closure of account | 20,000.00 | - |
| **NUFAIKA TRANSACTIONAL ACCOUNT** | | |
| Required minimum opening balance | 50,000.00 | 25.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **NORMAL CURRENT ACCOUNT (NUFAIKA ACCOUNTS)** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 6,000.00 | 3.00 |
| Cash withdrawal over counter up to 10M | 3,000.00 | 0.18% |
| Cash withdrawal over counter >10M | 10,000 | 10 |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | FREE |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | 10,000.00 | 4.20 |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **SPECIAL ACCESS NUFAIKA ACCOUNT** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 100,000.00 | 50.00 |
| Monthly service fees | 60,000.00 | 50.00 |
| Minimum monthly turover | 20,000,000.00 | 10,000.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | 0.18% |
| Fees per ATM withdrawal | 2,000.00 | N/A |
| ATM mini statement | 1,000.00 | N/A |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 25 leaves | 20,000.00 | 10.00 |
| Cheque book 50 leaves | 35,000.00 | 15.00 |
| Dishonored cheque | 30,000.00 | 30.00 |
| Bankers Cheque | 50,000.00 | FREE |
| Stop payment | 30,000.00 | 30.00 |
| Standing order Internal | 2,000.00 | 1.00 |
| Standing order External | 12,980.00 | 12.98 |
| Balance enquiry | 1,000.00 | 1.00 |
| New ATM card issuance | 15,000.00 | N/A |
| ATM card renewal or replacement | 15,000.00 | N/A |
| Interbank transfer | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Dormant account fee | 5,000.00 | 5.00 |
| Reactivation of Dormant account | FREE | FREE |
| Letter of recommendation and certificate of balance | 50,000.00 | 23.00 |
| **MIKAKATI SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | 20,000.00 | 20.00 |
| monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | 1 FREE PER MONTH | 1 FREE PER MONTH |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 20,000.00 | 20.00 |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | 12,000.00 | 5.00 |
| **KIKUNDI SAVING ACCOUNT** | **TZS** | |
| Required minimum opening balance | 10,000.00 | |
| monthly service fees | 2,000.00 | |
| Bank statement 1free per month | FREE | |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | |
| Cash withdrawal over counter | 3,000.00 | |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | 3,000 | |
| Dormant account fee | FREE | |
| International transfer | $ 55 | |
| Account closure | FREE | |
| **MINOR SAVING ACCOUNTS** | **TZS** | **USD/EURO** |
| Required minimum opening balance | - | - |
| monthly service fees | FREE | FREE |
| Bank statement 1free per month | FREE | FREE |
| Bank statement subsequent months | 10,000.00 | 10.00 |
| Cash withdrawal over counter | FREE | FREE |
| Subsequent Cash withdrawal over counter | FREE | FREE |
| Dormant account fee | FREE | FREE |
| International transfer | $ 55 | 55.00 |
| Account closure | FREE | FREE |

| TERM DEPOSIT RATES 2022 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Amount** | | | **Interest Rates** | | |
| 5,000,000 - 500,000,000 | | | 3% - 12% p.a | | |
| > 500,000,000 | | | Negotiation | | |
| **AGENCY BANKING** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| **Withdrawal (TZS) (agents) Range** | | | **TZS** | | |
| 1 - 2,999 | 10 | 710 | 350 | 350 | 710 |
| 3,000 - 3,999 | 14 | 711 | 350 | 350 | 714 |
| 4,000 - 4,999 | 27 | 719 | 350 | 350 | 727 |
| 5,000 - 6,999 | 54 | 739 | 350 | 350 | 754 |
| 7,000 - 9,999 | 56 | 770 | 350 | 350 | 756 |
| 10,000 - 14,999 | 102 | 788 | 350 | 350 | 802 |
| 15,000 - 19,999 | 195 | 924 | 350 | 350 | 895 |
| 20,000 - 20,000 | 306 | 1,127 | 350 | 350 | 1,006 |
| 20,001 - 29,999 | 306 | 1,372 | 1,300 | 700 | 2,306 |
| 30,000 - 39,999 | 351 | 2,672 | 1,300 | 700 | 2,351 |
| 40,000 - 49,999 | 419 | 2,770 | 1,300 | 700 | 2,419 |
| 50,000 - 99,999 | 573 | 3,050 | 1,300 | 700 | 2,573 |
| 100,000 - 100,000 | 707 | 3,435 | 1,300 | 700 | 2,707 |
| 100,001 - 199,999 | 707 | 3,771 | 2,520 | 980 | 4,207 |
| 200,000 - 200,000 | 821 | 5,271 | 2,520 | 980 | 4,321 |
| 200,001 - 299,999 | 821 | 5,558 | 3,225 | 1,275 | 5,321 |
| 300,000 - 300,000 | 838 | 6,558 | 3,225 | 1,275 | 5,338 |
| 300,001 - 399,999 | 838 | 6,950 | 3,850 | 1,650 | 6,338 |
| 400,000 - 499,999 | 982 | 7,950 | 3,850 | 1,650 | 6,482 |
| 500,000 - 599,999 | 1,245 | 8,370 | 3,850 | 1,650 | 6,745 |
| 600,000 - 699,999 | 1,532 | 9,140 | 3,850 | 1,650 | 7,032 |
| 700,000 - 750,000 | 1,700 | 9,980 | 3,850 | 1,650 | 7,200 |
| 750,001 - 799,999 | 1,700 | 10,470 | 4,750 | 2,250 | 8,700 |
| 800,000 - 899,999 | 1,500 | 11,970 | 4,750 | 2,250 | 8,500 |
| 900,000 - 1,000,000 | 1,776 | 12,264 | 4,750 | 2,250 | 8,776 |
| 1,000,0001 - 3,000,000 | 1,875 | 13,230 | 4,750 | 2,250 | 8,875 |
| 3,000,0001 - 5,000,000 | 2,000 | 13,580 | 4,750 | 2,250 | 9,000 |
| **Deposit (TZS) (agents) Range** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | **To Agent** | **New Customer Fee** |
| 0 - 10,000 | - | - | - | 100 | - |
| 10,001 - 20,000 | - | - | - | 150 | - |
| 20,001 - 50,000 | - | - | - | 200 | - |
| 50,001 - 100,000 | - | - | - | 350 | - |
| 100,001 - 150,000 | - | - | - | 550 | - |
| 150,001 - 200,000 | - | - | - | 700 | - |
| 200,001 - 250,000 | - | - | - | 850 | - |
| 250,001 - 300,000 | - | - | - | 900 | - |
| 300,001 - 500,000 | - | - | - | 1,100 | - |
| 500,001 - 750,000 | - | - | - | 1,200 | - |
| 750,001 - 3,000,000 | - | - | - | 1,600 | - |
| **MOBILE BANKING** | | | | | |
| **Withdrawal - Bank to Wallet (TZS)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 100-2,999 | 10 | 500 | 500 | | 510 |
| 3,000-3,999 | 14 | 500 | 500 | | 514 |
| 4,000-4,999 | 27 | 500 | 500 | | 527 |
| 5,000-6,999 | 54 | 500 | 500 | | 554 |
| 7,000-9,999 | 56 | 500 | 500 | | 556 |
| 10,000-14,999 | 102 | 500 | 500 | | 602 |
| 15,000-19,999 | 195 | 500 | 500 | | 695 |
| 20,000-29,999 | 306 | 500 | 500 | | 806 |
| 30,000-39,999 | 351 | 500 | 500 | | 851 |
| 40,000-49,999 | 419 | 500 | 500 | | 919 |
| 50,000-50,000 | 573 | 500 | 500 | | 1,073 |
| 50,001-99,999 | 573 | 1,000 | 1,000 | | 1,573 |
| 100,000-100,000 | 707 | 1,000 | 1,000 | | 1,707 |
| 100,000-199,999 | 707 | 2,000 | 2,000 | | 2,707 |
| 200,000-250,000 | 821 | 2,000 | 2,000 | | 2,821 |
| 250,001-299,999 | 821 | 3,000 | 3,000 | | 3,821 |
| 300,000-399,999 | 838 | 3,000 | 3,000 | | 3,838 |
| 400,000-499,999 | 982 | 3,000 | 3,000 | | 3,982 |
| 500,000-599,999 | 1,245 | 3,000 | 3,000 | | 4,245 |
| 600,000-699,999 | 1,532 | 3,000 | 3,000 | | 4,532 |
| 700,000-750,000 | 1,700 | 3,000 | 3,000 | | 4,700 |
| 750,001-799,999 | 1,700 | 4,000 | 4,000 | | 5,700 |
| 800,000-899,999 | 1,500 | 4,000 | 4,000 | | 5,500 |
| 900,000-1,000,000 | 1,776 | 4,000 | 4,000 | | 5,776 |
| 1,000,001-3,000,000 | 1,875 | 4,000 | 4,000 | | 5,875 |
| 3,000,001-5,000,000 | 2,000 | 4,000 | 4,500 | | 6,500 |
| **Deposit (TZS) (Wallet to Bank)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 0 - 50,000 | - | FREE | - | | - |
| 50,001 - 100,000 | - | FREE | - | | - |
| 100,001 - 250,000 | - | FREE | - | | - |
| 250,001 - 750,000 | - | FREE | - | | - |
| 750,001 - 3,000,000 | - | FREE | - | | - |
| **Air-time top-up** | - | FREE | - | | - |
| **Utility payments** | - | FREE | - | | - |
| **Balance inquiry** | - | 100 | 300 | | 300 |
| **Mini-statement** | - | 200 | 300 | | 300 |
| **Full account statement request** | - | 500 | 500 | | 500 |
| **Cheque book request** | - | 600 | 600 | | 600 |
| **AMBT internal transfers (same account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 1 - 999 | - | - | FREE | | - |
| 1,000 - 1,999 | - | 10 | FREE | | - |
| 2,000 - 2,999 | - | 11 | FREE | | - |
| 3,000 - 3,999 | - | 19 | FREE | | - |
| 4,000 - 4,999 | - | 39 | FREE | | - |
| 5,000 - 6,999 | - | 70 | FREE | | - |
| 7,000 - 9,999 | - | 88 | FREE | | - |
| 10,000 - 14,999 | - | 224 | FREE | | - |
| 15,000 - 19,999 | - | 427 | FREE | | - |
| 20,000 - 29,999 | - | 672 | FREE | | - |
| 30,000 - 39,999 | - | 770 | FREE | | - |
| 40,000 - 49,999 | - | 1,050 | FREE | | - |
| 50,000 - 99,999 | - | 1,435 | FREE | | - |
| 100,000 - 199,999 | - | 1,771 | FREE | | - |
| 200,000, 299,999 | - | 2,058 | FREE | | - |
| 300,000 - 399,999 | - | 2,450 | FREE | | - |
| 400,000 - 499,999 | - | 2,870 | FREE | | - |
| 500,000 - 599,999 | - | 3,640 | FREE | | - |
| 600,000 - 699,999 | - | 4,480 | FREE | | - |
| 700,000 - 799,999 | - | 4,970 | FREE | | - |
| 800,000 - 899,999 | - | 5,264 | FREE | | - |
| 900,000 - 1,000,000 | - | 6,230 | FREE | | - |
| 1,000,001 - 3,000,000 | - | 6,580 | FREE | | - |
| **AMBT internal outgoing transfers (other account holder)** | **To Govt** | **Old Customer Fee** | **To AMBT** | | **New Customer Fee** |
| 1 - 2,999 | 10 | 510 | 500 | | 510 |
| 3,000 - 3,999 | 14 | 511 | 500 | | 514 |
| 4,000 - 4,999 | 27 | 519 | 500 | | 527 |
| 5,000 - 6,999 | 54 | 539 | 500 | | 554 |
| 7,000 - 9,999 | 56 | 570 | 500 | | 556 |
| 10,000 - 14,999 | 102 | 588 | 500 | | 602 |
| 15,000 - 19,999 | 195 | 724 | 500 | | 695 |
| 20,000 - 29,999 | 306 | 927 | 500 | | 806 |
| 30,000 - 39,999 | 351 | 1,172 | 500 | | 851 |
| 40,000 - 49,999 | 419 | 1,270 | 500 | | 919 |
| 50,000 - 99,999 | 573 | 1,550 | 500 | | 1,073 |
| 100,000 - 199,999 | 707 | 1,935 | 500 | | 1,207 |
| 200,000 - 299,999 | 821 | 2,271 | 500 | | 1,321 |
| 300,000 - 399,999 | 838 | 2,558 | 500 | | 1,338 |
| 400,000 - 499,999 | 982 | 2,950 | 500 | | 1,482 |
| 500,000 - 599,999 | 1,245 | 3,370 | 500 | | 1,745 |
| 600,000 - 699,999 | 1,532 | 4,140 | 500 | | 2,032 |
| 700,000 - 799,999 | 1,700 | 4,980 | 500 | | 2,200 |
| 800,000 - 899,999 | 1,500 | 5,470 | 500 | | 2,000 |
| 900,000 - 1,000,000 | 1,776 | 5,764 | 500 | | 2,276 |
| 1,000,001 - 3,000,000 | 1,875 | 6,730 | 500 | | 2,375 |
| 3,000,001 - 5,000,000 | 2,000 | 7,080 | 500 | | 2,500 |
| **FOREIGN EXCHANGE TRANSACTION** | | | **TZS** | **USD** | |
| Telegraphic Transfer - Normal Customer (SWIFT) | | | 55.00 | 55.00 | |
| TISS- Normal Customer | | | 10,000.00 | 4.20 | |
| TISS-Staff | | | 6,000.00 | 2.10 | |
| **LOAN PRODUCT LENDING RATES** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 66.00% | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 35,000,000 | | | from 46.8% to 54% with graduation for good repeat clients and with good account turnover. | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 35,000,000 | | | from 49.2% to 68.4% with graduation for good repeat clients and with good account turnover. | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | from 26.4% to 42% with graduation for good repeat clients and with good account turnover. | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20.40% | N/A | |
| **Loan Processing Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 3.40% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 3.40% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 3.70% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 2.90% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | from 1.5% to 3.40% Inclusive of excise duty and VAT | N/A | |
| **Application Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 200,000,000 | | | 20,000.00 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 20,000.00 | N/A | |
| **Insurance Fee** | | | **TZS** | **USD** | |
| MICRO LOANS (Rahisi Loans) TZS 500,000 to 10,000,000 | | | 0.02 | N/A | |
| MICRO LOANS TZS 10,000,001 to 50,000,000 | | | 0.02 | N/A | |
| AGRO LOANS TZS 500,001 TO 50,000,000 | | | 0.02 | N/A | |
| SME LOANS/ODs 35,000,000 to 150,000,000 | | | 0.02 | N/A | |
| Loans/OD Secured by Fixed Term Deposits | | | 0.02 | N/A | |

# BENKI YA NBC YAIPAMBA 'DADI' SIMBA, YANGA DAR

**Na Mwandishi Wetu**

WADHAMINI wakuu wa Ligu Kuu Tanzania Bara, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wamekonga nyoyo za mashabiki wa soka katika mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga iliyochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Kwa kutambua umuhimu wa mashabiki wa soka ambao ni wateja wao wakuu kibiashara, Benki ya NBC, iliandaa matukio kadhaa kwa ajili ya wapenzi wa mchezo huo kwa wateja wake wakubwa na wadogo sambamba na kukabidhi tuzo na zawadi kwa mchezaji bora wa ligi hiyo kwa mwezi Septemba.

Shughuli zote hizo ziliongozwa na maofisa waandamizi wa benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, ambaye alipata wasaa wa kukabidhi tuzo na zawadi ya fedha kiasi cha Sh. milioni moja, kwa mchezaji wa Klabu ya Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', aliyetangazwa mchezaji bora wa ligi hiyo kwa mwezi Septemba.

Tukio hilo lililoshuhudiwa na maelfu ya mashabiki waliojitokeza kutazama mechi hiyo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, lilitanguliwa na matukio mengine ambapo benki hiyo iliandaa mwaliko rasmi kwa ajili ya wateja wake wakubwa zaidi ya 50 waliopata wasaa wa kupata chakula cha mchana pamoja na viongozi wa NBC kisha kwa pamoja walielekea Uwanja wa Taifa kushuhudia mechi hiyo wakiwa katika msafara maalum.

Akizungumzia hatua ya benki hiyo, Kaimu Mkuu wa Idara ya Masoko wa Benki hiyo, David Kigwile, alisema mbali na wateja wakubwa, benki hiyo pia ilitoa tiketi 70 kwa ajili ya wateja wake wadogo wa tawi jipya la Kigamboni ili waweze kwenda kutazama mtanange huo ikiwa ni ishara ya kuwakaribisha waweze kufurahia huduma za benki hiyo wilayani humo. "Tumetumia mechi hii kubwa kuwakaribisha wateja wetu wa tawi letu jipya lililoko wilayani Kigamboni, lengo likiwa ni kufurahi nao katika mchezo huu pendwa. Zaidi ya wateja 70 wilayani humo walipata fursa ya kutazama mechi hiyo kwa udhamini wa Benki ya NBC ambapo tuliweza kuwakatia tiketi wote pamoja na kuwapatia usafiri wa kwenda uwanjani na kurudi majumbani mwao wakiwa salama kabisa," alisema.

Aidha, benki hiyo iliandaa 'Screen' kubwa kwenye baadhi ya maeneo wilayani humo ili kutoa fursa kwa wapenzi wa mchezo huo ambao hawakuweza kufika uwanjani kuweza kufurahia mechi hiyo.

"Mbali na kutoa fursa kwa wapenzi wa soka kufuatilia mechi hiyo kupitia screen kubwa, pia walipata fursa ya kupata huduma mbalimbali za kifedha kutoka Benki ya NBC kupitia maofisa wetu waliokuwa wakitoa huduma mbalimbali ikiwamo kufungua akaunti mbalimbali pamoja na kufanya miamala ya kifedha wakiwa maeneo hayo pamoja na viunga vya Uwanja wa Benjamin Mkapa," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ambayo ni Mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara, NBC Premiere League, Theobald Sabi (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni moja kwa mchezaji wa Klabu ya Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', aliyetangazwa mchezaji bora wa ligi hiyo wa Septemba. Makabidhiano hayo yalifanyika muda mfupi kabla ya kuanza mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Mayayi ampa Phiri mchezaji bora wa 'Dabi'

**Na Hadija Mngwai**

ALIYEKUWA nahodha wa Klabu ya Yanga na Timu Taifa (Taifa Stars), ambaye kwa sasa ni Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayayi Tembele, amempa alama zote mshambuliaji wa Simba, Moses Phiri kuwa ndiye nyota wa mchezo wa watani wa jadi kutokana na uwezo wake wa kumiliki mpira juzi.

Simba na Yanga juzi zilitoka sare ya bao 1-1 katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, shukran kwa Augustine Okrah na Stephanie Aziz Ki waliozifungia timu zao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mayayi, alisema licha ya mshambuliaji huyo wa Simba kutofumania nyavu, lakini mikimbio yake ilionekana kuwa na madhara zaidi kwa wapinzani wao.

"Kwangu mimi nyota wa mchezo alikuwa Moses Phiri, licha ya kutofunga, kwani ukimwangalia alikuwa ni mchezaji ambaye alikuwa ana madhara sana upande wa Yanga. "Mikimbio yake ilikuwa ikiwasumbua wapinzani, Aziz Ki amefanikiwa kufunga bao bora lakini hakuwa na madhara kama ilivyokuwa kwa Phiri, ambaye alikuwa na umiliki wa mpira kwenye safu ya ulinzi ya Yanga," alisema Mayai.

Akitathmini mchezo mzima wa juzi, Mayayi alisema: "Ukiangalia timu zote zilicheza 50 kwa 50, makocha walijifìcha sana kwenye tahadhari ya ulinzi kabla ya kwenda kushambulia, timu zote zilipoteza nafasi ya kufunga.

"Tahadhari ya ulinzi ilikuwa kubwa, kipindi cha pili, Yanga walitengeneza nafasi lakini hawakuwa na utulivu, hii ni kutokana na presha kuwa kubwa, Yanga ilikuwa na walinzi sita na Simba vilevile, hivyo utahadhari wao wa kujilinda ndio usababisha sare.

"Kwa upande wa makocha, Mgunda (Juma) na Nabi (Nasreddine), ni makocha wanaotumia falsafa zinazofanana kwa kutaka timu zao zichezee mpira, wana wachezaji wazuri wanaoweza kuwasaidia," alisema.

## Azam mikononi mwa Kali Ongala

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umeweka wazi kwamba kwa sasa hauna mpango wa kutafuta kocha mkuu na timu yao itakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Kalimangonga Ongala, akisaidiana na Aggrey Morris kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba keshokutwa, Alhamisi.

Azam FC wataikaribisha Simba katika mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Alhamisi majira ya saa moja usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Msemaji wa klabu hiyo, Hashim Ibwe, alisema kuelekea mchezo wao dhidi ya Simba benchi lao litaongozwa na Kali akisaidiana na Aggrey.

Alisema mchakato wa kutafuta kocha mpya upo na kwamba hawana mpango wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ambaye amekuwa akihusishwa kwenda kukinoa kikosi cha timu hiyo ambacho hadi sasa kimepoteza michezo miwili ya Ligi Kuu Bara msimu huu.

"Kikosi kinaendelea na maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Simba tukiwa na makocha wetu Kali Ongala na Aggrey, suala la kocha mkuu hilo linaendelea kufanyiwa kazi," alisema Ibwe.

Azam FC wiki iliyopita ilimtimua Kocha wake Mkuu, Denis Lavagne, baada ya kushindwa kufikia malengo yao katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na kupoteza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya KMC FC iliyoshinda bao 2-1.

## Pazi, Vijana Queens mabingwa Kikapu

**Na Saada Akida**

TIMU ya Pazi wanaume na Vijana Queens (wanawake), zimetwaa ubingwa wa Ligi ya Taifa ya Mpira wa Kikapu (NBL), baada ya kuibuka na ushindi katika fainali ya michezo hiyo iliyomalizika juzi kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Pazi imechukuwa ubingwa huo baada ya kuibuka na ushindi wa vikapu 62-55 dhidi ya bingwa mtetezi wa michuano hiyo, ABC huku timu ya Wakuda ikishika nafasi ya tatu.

Kwa upande wa wanawake, Vijana Queens iliibuka na ushindi vikapu 59-48 dhidi ya JKT Stars ambao wamekamata nafasi ya pili.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Rais wa Shirikisho la Kikapu Tanzania (TBF), Rwehabura Barongo, alisema baada ya ligi hiyo kumalizika sasa wanajiandaa na mashindano ya Klabu Bingwa Afrika.

"Ligi imemalizika na tumepata bingwa ni Pazi baada ya ABC kushindwa kutetea taji lao, lakini itatuwakilisha katika Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Barongo.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### MOUKOKO ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanaongoza katika mbio za kuwania kumsajili mchezaji wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 17 raia wa Ujerumani, Youssoufa Moukoko. ***(Sport, via Mail)***

### ARSENAL YAMPOTEZEA NDICKA

ARSENAL imesitisha mpango wake wa kutaka kumsajili, mlinzi wa Eintracht Frankfurt raia wa Ufaransa, Evan Ndicka, mwenye umri wa miaka 23, baada ya kumpa mkataba Gabriel Magalhaes. ***(Express)***

### AMORIM ATAKIWA VILLA

ITAWALAZIMU Aston Villa kulipa euro milioni 10 ili kumchukua kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim. ***(Telegraph)***

### KANE, SON WASIWASI SPURS

ALIYEKUWA Kocha wa Tottenham, Tim Sherwood, amesema wasiwasi kuhusu mustakabali wa kocha wa sasa, Antonio Conte, unamzuia mshambuliaji, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, na raia wa Korea Kusini, Son Heung-min, aliye na miaka 30, kusaini mikataba mipya. ***(Sky Sports, via Express)***

### DALOT AMULIKWA MADRID

BEKI wa kulia wa Manchester United, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23, analengwa na Real Madrid. ***(Mirror)***

### RONALDO HUYOOO CHELSEA

CHELSEA wana nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 wakati wa dirisha la Januari.***(Mirror)***

### SALIHAMIDZIC AMSIFIA KANE

MKURUGENZI wa michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amesema Harry Kane ni "mojawapo ya wachezaji bora duniani". ***(Talksport)***

### ZIYECH KUMBADILISHA RABIOT

HUENDA Chelsea ikamtumia winga, Hakim Ziyech, mwenye umri wa miaka 29, katika mkataba wa kubadilishana na kiungo wa Juventus, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 27. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL NA MARTINEZ

MTENDAJI Mkuu wa Ajax, Edwin van der Sar, amesema aliiambia Arsenal klabu hiyo haitomuuza mlinzi wake raia wa Argentina, Lisandro Martinez, wiki kadhaa kabla ya kujiunga na Manchester United. ***(Times)***


### VARANE NA KOMBE LA DUNIA

HUENDA mlinzi wa Manchester United, Raphael Varane, mwenye umri wa miaka 29, akawa imara kuichezea Ufaransa katika Kombe la Dunia kutokana na kuimarika kwa jeraha lake alilopata la msuli wa paja. ***(ESPN)***

### KENNY KAKATAA MKATABA

ALIYEKUWA mlinzi wa Everton, Jonjoe Kenny, mwenye umri wa miaka 25, amesema alikataa mkataba mpya na timu hiyo kutokana na kwamba alibidi aondoke Uingereza kuendelea na kampeni ya kujiimarisha na timu ya Hertha Berlin msimu uliopita wa majira ya joto. ***(Liverpool Echo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ATOA NENO KWA JESUS KUSHINDWA KUTUPIA

●●●Alipata nafasi, lakini alishindwa kufunga, kwa hakika hiyo imemkatisha tamaa...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta alikiri Gabriel Jesus "alikatishwa tamaa" kwa kushindwa kufunga wakati Arsenal ilipotoka sare ya bao 1-1 na Southampton, Jumapili.

'Washikabunduki' hao walitangulia kupata bao pale kwenye Uwanja wa St Mary's, huku Granit Xhaka akifunga dakika ya 11, likiwa ni la pili na kumfanya afunge katika mechi mbili mfululizo kwa mara ya pili katika maisha yake akiwa Arsenal.

Jesus angeweza kuongeza uongozi wa Arsenal mara mbili katika kipindi cha kwanza, lakini shuti lake kali lilipaa sentimita chache kabla ya golikipa Gavin Bazunu kuokoa walipobaki wawili tu.

Kocha wa Arsenal, Arteta alisema Jesus, ambaye alijaribu kupiga mashuti manne na kushindwa kumfunga Bazunu, alionekana kukatishwa tamaa na kutofurahia hali hiyo.

"Nina uhakika leo (juzi) alisikitishwa sana, namfahamu Gabi," alisema Arteta baada ya mchezo huo.

"Alipata nafasi, lakini alishindwa kufunga na kwa hakika hiyo imemkatisha tamaa."

Arsenal walisonga mbele kwa pointi mbili dhidi ya Manchester City kwenye kilele cha msimamo wa Ligi Kuu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,044,3

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 25,26 NA 27 OKTOBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/10/22 | 22:00 | RB Leipzig vs Real Madrid | 2.87 | 3.42 | 2.28 |
| 02. 26/10/22 | 02:00 | CA Platense vs Lanus | 2.30 | 3.13 | 3.38 |
| 03. 26/10/22 | 22:00 | Eintracht Frankfurt vs Marseille | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 04. 26/10/22 | 22:00 | Barcelona vs Bayern Munchen | 2.38 | 3.53 | 2.66 |
| 05. 27/10/22 | 02:30 | Botafogo RJ vs Bragantino SP | 2.43 | 3.11 | 2.72 |
| 06. 27/10/22 | 03:45 | Goias vs America Mineiro MG | 2.68 | 3.02 | 2.53 |
| 07. 27/10/22 | 19:45 | Ludogorets Razgrad vs Betis | 2.95 | 3.45 | 2.26 |
| 08. 27/10/22 | 19:45 | Fenerbahce vs Rennes | 2.59 | 3.19 | 2.69 |
| 09. 27/10/22 | 19:45 | AEK Larnaca vs Dynamo Kiev | 3.25 | 3.40 | 2.18 |
| 10. 27/10/22 | 19:45 | Austria Vienna vs Lech Poznan | 2.59 | 3.34 | 2.59 |
| 11. 27/10/22 | 19:45 | PSV Eindhoven vs Arsenal | 2.68 | 3.51 | 2.42 |
| 12. 27/10/22 | 22:00 | Nantes vs Karabakh | 2.42 | 3.40 | 2.75 |
| 13. 27/10/22 | 22:00 | Sivasspor vs CFR Cluj | 2.26 | 3.24 | 3.24 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa airtel money

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE ATAKA MASHABIKI SPURS KUWA NA SUBIRA



**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham, Antonio Conte, amewasihi mashabiki wa Spurs wawe na subira baada ya Jumapili kufungwa mabao 2-1 nyumbani na Newcastle United.

Mashuti ya Harry Kane na Son Heung-min yalizuiwa vizuri na golikipa, Nick Pope na Newcastle walikwenda mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 2-0.

Makosa mawili ya golikipa, Hugo Lloris yaliigharimu timu hiyo kwa kuwawezesha Callum Wilson na Miguel Almiron kuifungia Newcastle.

Mashabiki waliizomea timu yao kwa sauti kubwa wakati wa mapumziko na vijana wa Conte hawakuwa bora zaidi baada ya mapumziko, huku wakipata bao la kichwa la Kane kipindi cha pili.

Conte alisema baada ya mchezo huo akiiambia Sky Sports: "Mashabiki wanatakiwa kuelewa, tunafanya kila tuwezalo katika kila dakika na pia (dhidi ya Newcastle) tulijitolea vya kutosha.

"Kwa hakika, katika wakati huu lazima tukabiliane, ni wakati mgumu kwetu kwa sababu unapokuwa huna wachezaji watatu au wanne kwenye kikosi, unakuwa taabani.

"Tunapaswa kudhibiti hali hii na kuishinda kwa pamoja. Bila wachezaji wanne au watatu kuongezwa kwenye usajili, tunakuwa kwenye wakati mgumu.

"Siku zote nilisema kabla ya kuanza msimu huu, timu muhimu, timu zitakazopigania ubingwa, utaona timu katika kipindi hiki unacheza kila baada ya siku tatu. Unahitaji kuwa na kikosi kipana, kikosi imara chenye ubora wa hali ya juu.

"Nadhani ndio tumeanza mchakato wetu msimu uliopita tu. Kutoka Europa Conference League, sasa tunacheza Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Subira ilikuwa mada kuu ya mahojiano marefu ya Conte, na wakati Muitaliano huyo alikiri kwamba Spurs wanapitia hali ngumu, pia anahisi kwa ujumla wanafanya vizuri.

# Xavi asifia kiwango cha Dembele

**BARCELONA, Hispania**

XAVI alisifu kiwango cha Ousmane Dembele, baada ya winga huyo wa Ufaransa kung'ara katika ushindi wa mabao 4-0 wa Barcelona dhidi ya Athletic Bilbao kwenye Uwanja wa Camp Nou, Jumapili.

Barca walipunguza pengo la pointi hadi tatu dhidi ya Real Madrid waliopo kileleni mwa msimamo wa LaLiga kwa kuwafunga Athletic, huku Dembele akitangulia kufunga kabla ya kutengeneza asisti tatu.

Mabao mengine matatu yaliyofungwa na Robert Lewandowski, Sergi Roberto na Ferran Torres, yote yalitengenezwa na Dembele na kumfanya kuhusika katika mabao manne kwenye mchezo mmoja akiwa na Barca kwa mara ya kwanza, ikiwa ni mechi yake ya 165 na 'Blaugrana' hao.

Dembele amefikisha pasi tano za mabao katika LaLiga, ndio bora zaidi kwenye mashindano msimu huu, na Xavi alimtaja mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kama mleta tofauti baada ya ushindi huo wa Barca.

"Aliamua kujitoa sana kwa timu. Alikuwa na hamasa kubwa sana," alisema Xavi akiiambia Movistar.

"Alielewa kila kitu vizuri. Yuko hapa kuleta mabadiliko na ana uwezo wa kufanya mambo haya."

Barca walitangulia kwa mabao matatu ndani ya dakika 22 huku Athletic wakionekana kuzidiwa katika vipindi vyote.

"Tulidhani ulikuwa mchezo wa nguvu, tulielewa kwamba wangetuwekea shinikizo kubwa," alisema Xavi.

Barca huo ulikuwa ushindi wao wa kwanza katika mechi nne zilizopita mwezi huu, wakipoteza kwa wapinzani wao wa Clasico, Madrid na kushindwa kuwafunga Inter katika mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya.



303,118/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/10/22 | 17:00 | Hull City vs Blackburn | 2.59 | 3.19 | 2.74 |
| 02. 29/10/22 | 17:00 | Wigan vs Watford | 2.93 | 3.28 | 2.39 |
| 03. 29/10/22 | 17:00 | Preston vs Middlesbrough | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 04. 29/10/22 | 17:00 | Huddersfield vs Millwall | 2.99 | 3.24 | 2.37 |
| 05. 29/10/22 | 17:00 | Brighton vs Chelsea | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 06. 29/10/22 | 19:30 | Fulham vs Everton | 2.29 | 3.42 | 2.97 |
| 07. 29/10/22 | 19:30 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.52 | 2.25 |
| 08. 29/10/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.53 | 3.53 | 2.58 |
| 09. 30/10/22 | 15:00 | AJ Auxerre vs AC Ajaccio | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 10. 30/10/22 | 15:30 | Hannover vs Karlsruher SC | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 11. 30/10/22 | 15:30 | Sandhausen vs Eintracht Braunschweig | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 12. 30/10/22 | 15:30 | Paderborn vs Hamburger SV | 2.28 | 3.73 | 2.79 |
| 13. 30/10/22 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 14. 30/10/22 | 17:00 | Brest vs Reims | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 15. 30/10/22 | 18:30 | Boavista vs Vizela | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 16. 30/10/22 | 19:00 | Sandefjord vs Ham-Kam | 2.58 | 3.37 | 2.63 |
| 17. 30/10/22 | 19:05 | Lorient vs Nice | 2.57 | 3.26 | 2.67 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 25/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4113 | Wolkite City FC vs Sidama Bunna SC | 2.96 | 2.91 | 2.39 |
| 14:30 | 5094 | Wuhan Three Towns FC vs Dalian Aerbing | 1.32 | 4.85 | 7.37 |
| 14:30 | 5764 | Shahrdari Hamedan vs Esteghlal Mollasani | 2.95 | 2.65 | 2.85 |
| 15:00 | 2305 | Pars Jonoubi Jam vs Khosheh Talaei | 2.31 | 2.63 | 3.50 |
| 16:00 | 2194 | Fasil Kenema vs Saint George FC | 2.85 | 3.00 | 2.60 |
| 16:00 | 3555 | Tanzania Prisons vs Polisi Tanzania | 2.30 | 2.75 | 3.70 |
| 16:00 | 4776 | AL Bataeh (UAE) vs Al Sharjah SC | 5.05 | 4.08 | 1.52 |
| 16:00 | 5238 | Dodoma FC vs Mtibwa Sugar | 2.25 | 2.85 | 3.70 |
| 16:00 | 5363 | Ittihad AL Ramtha vs Kfarsoum | 1.39 | 4.60 | 7.60 |
| 16:30 | 2636 | Nasaf Qarshi vs Bunyodkor | 1.54 | 3.81 | 5.27 |
| 16:30 | 2771 | Uthongathi vs Platinum City Rovers | 2.11 | 2.78 | 3.75 |
| 16:30 | 3556 | Metallurg Bekabad vs Neftchi Fargona | 2.03 | 2.87 | 3.84 |
| 17:00 | 3205 | USM Alger vs Paradou AC | 1.53 | 3.63 | 5.82 |
| 17:00 | 4578 | ASO Chlef vs JS Saoura | 3.84 | 2.92 | 2.01 |
| 17:00 | 4675 | CSA Steaua Bucuresti vs FC Otelul Galati | 1.77 | 3.40 | 4.17 |
| 17:55 | 5132 | AL Qaisoma vs Ohud Medina | 2.77 | 2.86 | 2.57 |
| 18:00 | 2435 | Smouha Club vs National Bank | 2.53 | 3.07 | 2.83 |
| 18:00 | 5236 | Ararat Yerevan vs Shirak Gyumri | 1.75 | 3.30 | 4.46 |
| 18:05 | 3910 | AL Hazm vs AL Akhdood | 1.84 | 3.20 | 4.08 |
| 18:15 | 3396 | Namungo vs Kagera Sugar | 2.30 | 2.75 | 3.65 |
| 19:00 | 4892 | AL Wahda Scc (UAE) vs Al Dhafra | 1.17 | 6.20 | 11.63 |
| 19:45 | 1362 | RB Salzburg vs Chelsea | 4.46 | 3.77 | 1.69 |
| 19:45 | 5514 | Sevilla FC vs Copenhagen | 1.48 | 4.16 | 6.15 |
| 20:00 | 1242 | Talaea El Gaish vs Enppi Club | 2.64 | 2.69 | 3.09 |
| 20:00 | 3295 | Brommapojkarna vs IK Brage | 1.70 | 3.99 | 4.54 |
| 20:00 | 5308 | Halmstads BK vs Orebro SK | 1.52 | 4.33 | 5.84 |
| 20:30 | 5133 | Maritzburg Utd vs Mamelodi Sundowns | 5.53 | 3.26 | 1.69 |
| 21:45 | 1444 | Portsmouth vs Oxford Utd | 1.95 | 3.46 | 3.61 |
| 21:45 | 1725 | Bradford City vs Swindon Town | 1.97 | 3.42 | 3.57 |
| 21:45 | 1734 | Barnsley vs Lincoln | 1.77 | 3.57 | 4.27 |
| 21:45 | 1933 | Coventry vs Rotherham | 1.76 | 3.52 | 4.36 |
| 21:45 | 2529 | Derby vs Exeter | 1.89 | 3.47 | 3.82 |
| 21:45 | 2800 | Tranmere vs Rochdale | 1.96 | 3.27 | 3.77 |
| 21:45 | 2909 | Plymouth vs Shrewsbury | 1.71 | 3.57 | 4.66 |
| 21:45 | 3237 | Peterborough vs Accrington | 1.68 | 3.82 | 4.46 |
| 21:45 | 3425 | Bolton vs Burton | 1.71 | 3.70 | 4.45 |
| 21:45 | 3824 | Fleetwood Town vs Forest Green | 1.96 | 3.37 | 3.66 |
| 21:45 | 3826 | Charlton vs MK Dons | 1.74 | 3.61 | 4.36 |
| 21:45 | 3868 | AFC Wimbledon vs Crewe | 2.09 | 3.21 | 3.46 |
| 21:45 | 4158 | Wycombe vs Cambridge Utd | 1.83 | 3.61 | 3.91 |
| 21:45 | 4478 | Ayr United vs Partick Thisle | 2.35 | 3.30 | 2.80 |
| 21:45 | 4701 | Cheltenham vs Morecambe | 2.02 | 3.37 | 3.47 |
| 22:00 | 1115 | Benfica vs Juventus | 1.94 | 3.48 | 3.62 |
| 22:00 | 1672 | Dinamo Zagreb vs AC Milan | 4.16 | 3.62 | 1.77 |
| 22:00 | 2686 | Paris St Germain vs Maccabi Haifa | 1.12 | 7.81 | 17.46 |
| 22:00 | 3618 | Borussia Dortmund vs Manchester City | 4.53 | 4.06 | 1.63 |
| 22:00 | 3869 | Burnley vs Norwich City | 2.14 | 3.32 | 3.22 |
| 22:00 | 4245 | Celtic vs Shakhtar Donetsk | 1.80 | 3.71 | 3.91 |
| 22:00 | 5398 | RB Leipzig vs Real Madrid | 2.82 | 3.37 | 2.33 |
| 23:00 | 2815 | Ayacucho vs Alianza Lima | 3.79 | 3.69 | 1.77 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# CHAMA, AZIZ KI KIVUTIO WASHINDI WA 'BETIKA MTOKO WA KIBINGWA'

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wa Simba, Clatous Chama na Stephane Aziz Ki wa Yanga ni miongoni mwa wachezaji waliowavutia mabingwa 48 wa Betika Mtoko wa Kibingwa ambao waliungana na maelfu ya mashabiki wa soka nchini kuishuhudia 'dabi' ya watani hao wa jadi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Dabi hiyo ilimalizika kwa sare bao 1-1, shukran kwa Agustine Okrah aliyeitanguliza Simba dakika ya 15 na Aziz Ki ayeisawazishia Yanga sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko.

Baada ya mechi hiyo, mashabiki wa timu hizo ambao ni washindi wa Betika Mtoko wa Kibingwa, waliwayaja Chama na Aziz Ki kuwa kivutio zaidi katika mchezo huo.

Wakizungumza baada ya mechi hiyo juzi jioni, washindi hao kwa nyakati tofauti waliuelezea mchezo huo huku wale wa Simba wakimtaja Chama kuwakosha zaidi wakati wa Yanga wakilitaja jina la Aziz Ki.

Julius Kiria na Kanjinura Said wote wa Ruvuma ambao dabi hiyo ni ya kwanza kwao kuishuhudia mubashara, kwa nyakati tofauti walieleza kuvutiwa zaidi na kumshuhudia Aziz Ki akiokoa timu yake kwa kipigo.

"Mimi ni Yanga damu, binafsi nimevutiwa na kiwango cha timu yangu, lakini Aziz Ki amenikosha zaidi hasa baada ya kufunga bao la kusawazisha," alisema Kiria ambaye ni mnazi wa Yanga.

Issa Seleman wa Shinyanga, alisema uwezo wa wachezaji wa Simba ulimvutia, akimtaja Chama kuwa nyota aliyemkosha zaidi kwa kutengeneza pasi iliyozaa bao kwenye mechi hiyo ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu.

Mashabiki wengine wa Mtoko wa Kibingwa walioishuhudia mubashara mechi hiyo wakiwa VIP sanjari na marafiki zao, waliowachagua kwenye mabano ni Onesmo Ramadhan (Aloyce Msokele) na Isack Lyelu (Daud Sanga) wa Iringa na Issa Seleman (John Venge) wa Shinyanga.

Mtahangwalwa Salabai (Isaya Mateku) wa Mwanza, Erick Lutaiwa (Joseph Kabaitilaki) wa Bukoba, Abdulkarim Kisuda (Emmanuel Lawena) na Adamson Auson (Upendo Mbeaje) wa Mbeya, Richard Docho (Aidan Docho) wa Dodoma.

Wengine ni Ntacho Makungu (John Bosco Mabongo) wa Kigoma, Julius Kiria (Kanjinura Said) wa Ruvuma, Onesmo Ramadhan (Aloyce Msokele).

Washindi wa Dar es Salaam ni Moses Andrea (Simon Mwanfeya), Abraham Mandala (Jimmy Joseph), Erick Mongi (Hanzuruni), Erasto Margwe (Meckson Martin), Frank Haule (Lueiegad Njovu), Dennis Changanyikeni (Abdul Said), Ally Salum (Jacq Mkandala), Felix Charles (Frank Bushaijabwe) na Jevon Mhaluka (Adam Khalfani).

"Betika kama tulivyoahidi mabingwa wote 48 walikula bata la msimu juzi kwa ajili ya kusindikiza dabi ya watani wa jadi jana (juzi) na leo wameondoka kwa ndege kurudi kwenye mikoa yao," alisema Juvenalius Rugambwa, Ofisa Habari wa Betika.



Washindi wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa', wakifuatilia mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1 juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Hasira za Simba SC kwa Azam

INATOKA UK. 32

kuwashangilia muda wote, licha ya ugumu wanaopata.

"Cha kujivunia sisi Simba ni mshabiki wetu walijaa kuliko wenzetu ambao walikuwa wenyeji wa mechi, walikuja na kushangilia muda wote wametuonyesha kuwa hawakati tamaa licha ya kwamba hatukupata ushindi kwenye mechi zilizopita, lakini, wanatupa kinachotahili kutoka kwao, lakini kwa matokeo sisi hatujawapa kile wanachostahili kutoka kwetu," alisema.

# Micho afunguka Yanga

INATOKA UK. 32

ya bao alilofunga la 'free kick' (mpira uliokufa), nimemfuatilia tangu dakika ya kwanza mpaka mwisho," alisema Micho.

Alisema anawapongeza sana makocha wazawa wanaokinoa kikosi cha Simba, Juma Mgunda na Selemani Matola kwa timu yake kucheza mpira mzuri na kutawala mchezo licha ya mechi hiyo kumalizika kwa sare ya bao 1-1.

Katika mechi hiyo, Simba ilimiliki mpira zaidi vipindi vyote viwili na kama safu ya ushambuliaji ingekuwa makini, ingeweza kumaliza kipindi cha kwanza ikiwa mbele kwa mabao matatu.

Nipashe pia ilibisha hodi kwa Shirikisho la Soka la Uganda (Fufa), kutaka kujua endapo Micho amemaliza mkataba wa kuinoa timu hiyo ama la, ambapo lilizungumza na Ofisa Habari wa Fifa, Ahmed Hussein Marsha na kueleza si rahisi kocha huyo kuondoka.

Marsha alisema "'He can't join'" (hawezi kujiunga Yanga) na kwamba, kwa kuwa bado ana mkataba wa kuinoa timu hiyo ya taifa.

# Michezo

Jumanne Oktoba 25, 2022

Nipashe




UKURASA 29

## Arteta atoa neno kwa Jesus

UMESOMA CUBA?...




Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Uganda, Milutin Sredojevic 'Micho' (kulia), akionyesha jezi aliyokabidhiwa jana na Rais wa Yanga, Hersi Said, ikielezwa kwamba ni zawadi tu. **MPIGAPICHA WETU**

# *Micho afunguka Yanga, amtaja Mgunda, Matola*

●●●Amshusha presha Nabi anayedaiwa kukalia kuti kavu, FA ya Uganda yatoa kauli...

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Uganda, Milutin Sredojevic 'Micho', akihusishwa na kuja kurithi mikoba ya Mtunisia Nasreddine Nabi katika kikosi cha Yanga, Mserbia huyo ameanika kila kitu kuhusu tetesi hizo zilizosambaa kwa kasi baada ya kuonekana Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi akiwa na viongozi wa klabu hiyo juzi.

Micho alikuwa miongoni mwa wageni kutoka nje waliohudhuria 'Dabi' ya Simba na Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, shukran zikiwaendea, Agustine Okrah aliyewatanguliza Wekundu wa Msimbazi dakika ya 15 na Stephane Aziz Ki aliyeisawazishia timu yake sekunde chache kabla ya kuelekea mapumziko.

Tetesi za Micho kuandaliwa kuja kuchukua mikoba ya Nabi, inachagizwa na madai ya kukosekana maelewano katika benchi la ufundi la Yanga, ikidaiwa kuwa haelewani na msaidizi wake, Cedric Kaze, lakini kubwa likiwa ni kushindwa kuipa timu hiyo mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kutofikia malengo ya kufuzu hatua ya makundi kwa kutolewa na Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1.

Hata hivyo, Micho ambaye amewahi kuinoa Yanga mwaka 2007 na kuipa taji la Ligi Kuu Bara wakati timu hiyo ikiwa chini ya Mwenyekiti, Imani Madega, amekanusha taarifa hizo za kuwa njiani kurejea kuinoa.

Kocha huyo ambaye ana rekodi ya kushiriki 'dabi' nne kubwa ikiwamo Kariakoo Dabi (Yanga na Simba), Omdurman Dabi (Al Hilal dhidi ya El Merrick), pamoja na Cairo Dabi, (Zamalek na Al Ahly), bado ana mkataba na Timu ya Taifa ya Uganda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Micho alisema kilichomleta nchini ni kuangalia mchezo wa dabi ya timu hizo kongwe mbili, Simba na Yanga ambao ulipigwa juzi.

Alisema hakuja nchini kwa sababu ya taarifa za kufanya mazungumzo na Yanga, kwani lengo lake lilikuwa ni kushuhudia mchezo huo pamoja na mchezaji wa timu yake ya taifa, Khalid Aucho.

"Licha ya kuja kuangalia moja ya kati ya dabi bora kwa sasa Afrika Mashariki na Kati, pia Yanga ni familia yangu, nilikuja kumwangalia mmoja wa viungo wangu, Khalid Aucho.

"Mchezo ulikuwa mzuri ila Aziz Ki kwangu alikuwa mchezaji bora licha

INAENDELEA UK. 31

# Hasira za Simba SC sasa kwa Azam FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema haikupata ilichostahili kwenye mechi dhidi ya Yanga, hivyo sasa hasira zao wanazihamishia kwenye mechi dhidi ya Azam FC keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, amesema mioyo ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo imekunjamana na hawana furaha hata kidogo kutokana na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Yanga kwenye mechi ambayo waliitawala kwa kiasi kikubwa, hivyo hasira zote zitaelekezwa kwa Azam FC.

"Hatujapata kile ambacho tulikistahili na kukitaka, tunaheshimu matokeo ya 'dabi' na mpira wa miguu, lakini hatujapendezwa nayo, ni matokeo ambayo hatukustahili kutokana na ubora wa timu yetu, ukiangalia dakika 90 zote tulikuwa bora sana, lakini mwisho wa siku tumeambulia alama moja, licha ya kwamba ni sare, lakini hatujapendezwa nayo kwa sababu tulistahili zaidi ya hii sare. Niseme tu mpinzani wetu ana bahati kubwa, alistahili kipigo kikubwa sana," alisema Ahmed.

Alisema kwa sasa nguvu zote zinaelekezwa kwenye mechi dhidi ya Azam FC.

"Anayefuata ni Azam FC, ina kazi kubwa, tuna hasira na sare ya Yanga, mioyo imekunjana, hatuna furaha hata kidogo, timu bora haistahili kupata matokeo hasa kwa mechi ambayo tumeitawala, tunakwenda kukukutana na mpinzani mgumu, lakini tunafahamu wapi pakumshika. Tunajua wameshamfukuza kocha wao, lakini hilo sisi si kazi yetu, kazi yetu ni kuzichukua pointi tatu kwenye mechi hiyo," alisema.

Ahmed pia aliwapongeza na kuwashukuru mashabiki wao kwa kuwapa sapoti,

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >